Utawala wa Kanisa
Paulo na Watendakazi Wenzake
Yesu kama Mwelimishaji Mkuu
Wito wa Mitindo Mbadala ya Elimu kwa ajili ya Kanisa na Misheni
Je, Ukatoliki wa Kirumi Umebadilika?



Schirrmacher ni Profesa wa Theolojia (katika Ethics, missions, world religions), Rais wa Martin Bucer Theological Seminary na wa Giving Hands (Mikono itoayo), ambalo ni shirika hai la kimataifa la misaada; na mmiliki wa shirika la uchapaji (Publishing House). Ameandika na kuhariri vitabu 40 na anatajwa kwenye Marquis "Who's Who in the World", katika "International Who is Who of Professionals", katika "Who is Who in der Bundesrepublik Deutschland" na katika "International Who's Who in Distance Learning". Anazo shahada zifuatazo: M.Th. (STH Basel, Switzerland), Drs. Theol. (Theologische Hogeschool, Kampen, Netherlands), Drs.Theol. (Missiology, Johannes Calvin Stichting, Kampen, Netherlands), Ph.D (Cultural Anthropology, Pacific Western University, Los Angeles), Th.D (Ethics, Whitefield Theological Seminary, Lake-land, D.D. (Honorary doctorate, Cranmer Theological House, Shreveport).

ISBN 978-9987-718-06-1 (TASCM)
ISBN 978-3-928936-03-3 (RVB)

TASCM RVB INTERNATIONAL

TRANS - AFRICA SWAHILI CHRISTIAN MINISTRIES TANZANIA

Thomas Schirrmacher Mafunzo Yahusuyo Uongozi wa Kanisa TASCM | RVB

# Mafunzo Yahusuyo Uongozi wa Kanisa

Muundo wa Kanisa wa Agano Jipya – Paulo na Watendakazi Wenzake – Elimu ya Theolojia Mbadala – Uhakiki wa Sheria ya Kanoni ya Kikatoliki



Thomas Schirrmacher

**Mafunzo Yahusuyo Uongozi wa Kanisa**

**RVB** International
Volume 21

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Thomas Schirrmacher: | GOD Wants You to Learn Labor and Love |
| 2 | Thomas Schirrmacher: | Legends About the Galileo-Affair |
| 3 | Thomas Schirrmacher: | World Mission – Heart of Christianity |
| 4 | Thomas Schirrmacher: | Law or Spirit – an alternative View of Galatians |
| 5 | Thomas Schirrmacher: | Human Rights Threatened in Europe |
| 6 | Thomas Schirrmacher: | Be keen to get going – William Carey's Theology |
| 7 | Thomas Schirrmacher: | Love is the Fulfillment of the Law |
| 8 | Thomas Schirrmacher: | Studies in Church Leadership |
| 9 | Monte Wilson: | The Most Important Rule for Living |
| 10 | Monte Wilson: | Principles of Success in Business |
| 11 | Th. Schirrmacher (Ed.): | A Life of Transformation – From Politician to Good Samaritan – A Festschrift for Colonel Doner |
| 12 | Thomas Schirrmacher: | DIOS Quiere Que tu Aprendas, Trabajes y Ames |
| 13 | Christine Schirrmacher: | La Vision Islamica de Importantes Enseñanzas Cristianas |
| 14 | Thomas Schirrmacher: | Sheria au Roho |
| 15 | Thomas Schirrmacher: | Upendo ni Utimilifu wa Sheria |
| 16 | Thomas Schirrmacher: | Mateso ya Wakristo Yanatuhusu Sisi Sote |
| 17 | Monte Wilson: | Sheria Muhimu Zaidi katika Kuishi |
| 18 | Thomas Schirrmacher: | Mungu Akutaka Ujifunze, Ufanye kazi, na Upende |
| 19 | Christine Schirrmacher: | Mtazamo wa Kiislamu juu ya Mafundisho Makuu ya Kikristo |
| 20 | Thomas Schirrmacher: | Tumaini kwa Afrika |
| 21 | Thomas Schirrmacher: | Mafunzo Yahusuyo Uongozi wa Kanisa |

Thomas Schirrmacher

# Mafunzo Yahusuyo Uongozi wa Kanisa

Kimetafsiriwa na Joseph M. S. Ipimilo

Kimehaririwa na Emmanuel E. Buganga

TASCM | RVB International

**Bibliographic information published by the Deutsche Nationalbibliothek**

The Deutsche Nationalbibliothek lists this publication in the Deutsche Nationalbibliografie; detailed bibliographic data are available in the Internet at http://dnb.d-nb.de

ISBN 978-3-928936-03-3

© Copyright 2001, 2011 by
Reformatorischer Verlag Beese
www.rvbeese.de / info@rvbeese.de
Printed in Germany

ISBN 978-9987-718-06-1

© Kwa Toleo la Kiswahili, 2011
Trans-Africa Swahili Christian Ministries
P.O. Box 772,
Mwanza, Tanzania

Toleo la Kwanza 2011, Nakala 2,000

Maandiko Matakatifu:
The Holy Bible in Kiswahili
Union Version, 1994

Mistari ya Biblia iliyokolezwa ni tafsiri ya mwandishi mwenyewe kutoka katika Maandiko Matakatifu asilia ya Kigriki.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kurudufu au kutoa kitabu hiki kwa njia yoyote ile bila idhini ya Trans-Africa Swahili Christian Ministries, Idara ya Maandiko.

---

Kimepigwa Chapa na: Inland Press, P.O. Box 125, Mwanza, Tanzania (East Africa) TEL. +255 28 2560175 inlandpress@yahoo.com

# Yaliyomo

Utawala wa Kanisa: Ngazi Tatu za Utawala katika Kanisa la Agano Jipya 7
Ofisi katika Agano Jipya ........ 7
Ngazi ya Pili ya Utawala: Wazee (Wachungaji) ........ 12
Ngazi ya kwanza ya Utawala: Wahudumu wa Kiume na Wahudumu wa Kike ........ 15
Mapitio: Wajibu wa Kijamii katika Kanisa la Agano Jipya kwa Mujibu wa Matendo 6 ........ 21
Ngazi ya Tatu ya Uongozi (Sehemu ya Kwanza): Ukanisa–mtaa na Upresbaiteria ........ 24
Ngazi ya Tatu ya Uongozi (sehemu ya pili): Uepiskopo ........ 28
Hoja Tisa kuhusu Muundo wa Kanisa na Uongozi ........ 35
Paulo na Watumishi Wenzake: Jinsi 'Wamishenari wa Agano Jipya' Hufanya Kazi Pamoja ........ 44
Kujifunza kutoka kwa Paulo ........ 44
Tukio la 1: Paulo anampa Tito umuhimu wa kwanza ........ 46
Tukio la 2: Usia kwa Mtume ........ 49
Tukio la 3: Paulo Anakataa Kupanda Kilele cha Kiroho ........ 51
Tukio la 4: Kufundisha kwa Kielelezo ........ 53

Yesu kama Mwelimishaji Mkuu ........ 59
1. Mafundisho na Maisha ........ 59
2. Mafunzo ya Mitume Kumi na Wawili ........ 61
3. Paulo na Watendakazi Wenzake ........ 66
4. Kuwa na Kielelezo cha Kuigwa, Kuwa Kielelezo cha Kuigwa ........ 71

Wito wa Mitindo Mbadala ya Elimu kwa ajili ya Kanisa na Misheni: Hoja 21 ........ 77

Je, Ukatoliki wa Kirumi Umebadilika? ........ 97
Mapitio ya Sheria ya Kanoni ya Hivi Karibuni ........ 97
Au: Uondoaji Mamlaka ya Baraza kwa njia ya Upapa (1990) ........ 97
I. Mahali pa Kuanzia: Matumizi ya Neno "Mapokeo" katika Maandiko ........ 97
A. Mapokeo katika Agano la Kale ........ 97
B. Mapokeo katika Agano Jipya ........ 98
II. Kiini cha Sheria ya Kanisa Katoliki ........ 100
A. Sheria za Kanisa Katoliki kwa ujumla ........ 100

B. Tofauti kati ya Haki ya Mungu na ya Kibinadamu katika Sheria ya Kanisa ... 102
III. Sheria Mpya ya Kanoni ya Kikatoliki ya 1883 ... 104
A. Sheria ya Kanisa kama Uelezi wa Upapa ... 104
B. Uhalisia wa Sheria ya Kanoni ... 105
C. Usuli wa Kihistoria wa Sheria Mpya ya Kanoni ... 105
D. Tofauti kati ya Sheria za Kanisa za 1917 na 1983 ... 106
E. Maoni ya Jumla juu ya Sheria Mpya ya Kanisa ... 107
F. Mwendo Kuielekea Biblia? ... 107
G. Makuzi katika Sheria Mpya ya Kanisa? ... 108
H: Mifano ya Uhifadhi wa Mafundisho ya Kikatoliki katika Sheria Mpya ya Kanisa ... 113
I. Hitimisho ... 116
IV. Ibara Muhimu za Sheria Mpya ya Kanisa ... 117

Visawe na Maelezo ya Maneno ... 123
Vifupisho vya Maneno ... 129

# Utawala wa Kanisa: Ngazi Tatu za Utawala katika Kanisa la Agano Jipya

*Zimefupishwa kutoka katika sura ya Maadili [‘ethik’, 2001, toleo sahihishwa la 2, kit. 3; 2002, toleo sahihishwa la 3, kit. 5]*

## Ofisi katika Agano Jipya

Mitume na waandishi wote wa Agano Jipya hukubali kuwa Kristo ndiye Kichwa kikuu cha Kanisa, na kwamba hakuna mtu mwingine awaye yote awezaye kudai jukumu hilo. Kwa sababu hii, anaweza kubeba cheo chochote cha uongozi: ‘*mtumwa*’ (Flp. 2:7, na pia katika Mathayo na Matendo ya Mitume), ‘*Mhudumu*’ (Rum. 15:8; Luk. 22:27), ‘Mtume’ (Ebr. 3:1, linganisha na Mk. 9:37; Luk. 10:16; Yoh. 3:34), ‘*Mwalimu*’ (Mat. 23:8; Yoh. 13:13). Neno la Kigriki ‘didaskalos’ hujitokeza mara 58 katika Injili, neno la Kiaramu ‘rabbi’ hujitokeza mara 15.), ‘*Mwangalizi*’ au ‘*Askofu*’ (1 Pet. 2:25), ‘*Mchungaji*’ (1 Pet. 2:25; Ebr. 13:20; Yoh. 10:11-14), ‘*Mchungaji Mkuu*’ (1 Pet. 5:4), ‘*Kiongozi*’ (Mat. 23:10), ‘*Bwana*’ (limetajwa takribani mara 100 hivi katika Agano Jipya), ‘***Mkuu***’ (mara 7 katika Injili nne. *Neno hili kwa Kiingereza ni ‘Master’, limetafsiriwa kwa Kiswahili kama ‘Mwalimu’* [maneno yaliyolazwa mahali hapa ni nyongeza ya mtafsiri]). Zaidi ya yote, Yesu ni kuhani mkuu (‘Kuhani wa juu kabisa’ au ‘Kuhani Mkuu’) wa Kanisa lake (Ebr. 2:17; 4:14-15; 5:10; 6:20; 7:26-27; 8:1; 9:11; 10:21).

Fahamu kuwa Yesu si tu Mkuu wa Kanisa lote ulimwenguni, bali pia wa kanisa la mtaa, kama 1 Wakorintho 12:14-21 inavyoweka wazi jambo hili. Uongozi wake una matokeo ya kivitendo kwa kanisa la mtaa na kwa muundo wake (Angalia 1 Pet. 5:1-4; Yoh. 13:13-17; Mat. 23:8-12). Hata hivyo, hapa tunapata mfano halisi usiopatana waziwazi. Waandishi wote hukubali kuwa Yesu anaweza kutumia cheo chochote, lakini hutumia vyeo tofauti katika mazingira tofauti. (Mbali na hayo, hatufahamu ni vyeo vipi vingine ambavyo viliweza kutumika, lakini havionekani katika maandishi tuliyorithishwa).

Katika Agano Jipya, kanisa la mtaa daima lilianza kwa utangazaji wa injili uliofanywa na waumini wasafirio huku na huko (ama kwa kukimbia mateso au kwa kuhama tu), na wainjilisti, mitume au wasaidizi wao. Ulikuwa ni wajibu wa mitume kuwawekea mikono wazee wa kanisa, ambao baadaye waliongoza kanisa la mtaa chini ya usimamizi wa viongozi

waliowajibika kwa makanisa kadhaa, wakati mitume wakijaribu kufikia maeneo mapya kwa injili (angalia 1 Thes. 1 na Rum. 15:14-33[1]).

Mtume, watendakazi wenzake na warithi wao waliongoza makanisa mpaka wazee walipoteuliwa, lakini waliendelea kushikilia nafasi za kimamlaka, zilizotambuliwa kama ‘*baba*’ (1 Kor. 4:14-16; 3 Yoh. 4). Kwa upande mmoja, kanisa la mtaa lilijitawala lenyewe; lakini kwa upande mwingine, liliwajibika kwa mitume na wasaidizi wao na warithi wao. Uhusiano wa Paulo na kanisa huko Korintho kwa ubora unadhihirisha kanuni hii.

Tangu mwanzo kabisa, utawala wa kanisa la mtaa la Agano Jipya ulijumuisha wazee na wahudumu kadhaa walichaguliwa kushika vyeo hivyo kwa msingi wa sifa njema au ushuhuda mwema (Matendo 6:3; Tito 1:5-9; 1 Petro 5:1-4). Kwa sababu hii, Paulo, Luka na Petro walitambua na kuorodhesha sifa stahili. Mbali na sifa njema, karama za kiroho zilihitajika. Kwa kuwa hizi haziwezi kueleweka kwa akili, tunapata vipande vya orodha vinavyotofautiana daima, vikijumuisha mifano tu[2]. Wote wawili, Paulo na Petro wanazungumza juu ya karama za roho (1 Pet. 4:10-11), ambazo huamua juu ya huduma ya mtu binafsi (1 Kor. 12:4-7). Kwa kuwa baadhi ni muhimu kwa uongozi (“*wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu;*” Efe. 4:11), vyeo mbalimbali vinatajwa kuhusiana nao (kwa mfano, “*mitume na wazee*” katika Matendo 15:6 na 23; 16:4; na “manabii na walimu” katika Matendo 13:1-3).

Maandiko hayatofautishi kati ya huduma ya kitaalamu na huduma isiyo ya kitaalamu. Hata hivyo, jambo hili huelezea uteuliwaji wa watumishi kwa ‘huduma ya kudumu’ kwa mantiki kwamba Wakristo wenye vipawa na waliothibitishwa waliwekewa mikono na viongozi wa kiroho na kanisa ili kushika ofisi na majukumu ambayo yalihitaji muda wote na nguvu zote za mhusika. Kama ilivyo katika Agano la Kale[3] (1 Kor. 9:13, Law. 6:16, 26; Law. 7:6, 31 na kuendelea, Hes. 5:9 -10; 18:8-20, 31[hususani mstari wa 10]; Kumb. 18:1-4; linganisha na ‘zaka’[4]) watumishi hawa wa kanisa la Agano Jipya walilipwa na kanisa la mtaa (1 Kor. 9:1-8, hususani mstari wa

---

1 Tazama komentari kuhusiana na kifungu hiki katika Thomas Schirrmacher, *Der Römerbrief,* vol. 2, Hänssler: Neuhausen, 1994, pp. 291-297.

2 Tazama Thomas Schirrmacher, *Ethik,* vol. 2, Chapter 24, Hänssler: Neuhausen, 1994, pp. 87-98.

3 Tazama Walter C. Kaiser. „The Current Crisis in Exegesis and the Apostolic Use of Deuteronomy 25:4 in 1 Corinthians 9:9-10“, *Journal of the Evangelical Theological Society* 21 (1978) 1: 3-18.

4 Tazama Thomas Schirrmacher, *Ethik,* vol. 2, op. cit., pp. 432-441.

14, 1 Tim. 5:17-18, 2 Tim. 2:4, 6). Paulo anamwandika Timotheo kwa uwazi kabisa (2 Tim. 2:4), "*Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari*". Hata hivyo, haukuwa mshahara uliomtofautisha mtumishi mwenye taaluma, bali kipaumbele alichokiweka katika huduma hiyo, ambacho kiliamua matumizi ya muda wa mtu huyo. Kwa mfano, kwa wa mujibu wa fasili yetu ya sasa, Paulo alikuwa mfanyakazi wa kawaida kama kiongozi wa umishenari, kwa sababu Paulo alijipatia mahitaji yake ya maisha yeye mwenyewe na kwa ajili ya watendakazi wenzake (Mdo. 20:33-35; 1 Thes. 2:9; 1 Kor. 9:12; 2 Kor. 11:5-9, Mdo. 18:3). Kwa hiyo, watendakazi wenzake wangeweza kuchukuliwa kuwa ni watumishi "wa kudumu", lakini ni Paulo ambaye tunamwona kama mfano halisi wa mtumishi wa Kikristo "wa kudumu".

Ninaamini kuwa tuna watumishi wa kudumu wachache sana kanisani na katika misheni. Katika Agano la Kale, kabila lote, yaani Walawi, waliteuliwa kuwatumikia watu wa Mungu kwa muda wote. Wengi wao walikuwa makuhani, wengine walimu, wanamuziki au washauri wa mambo ya kisheria. Waliishi kwa kutegemea zaka. Kiwango cha zaka, yaani asilimia kumi, hudhihirisha tathmini ya Mungu ya mahitaji kwa ajili ya watumishi wa muda wote.

Hebu tuchukue kanuni ya kuwalipa makuhani na Walawi na kuileta kanisani. Je, hakuna mkanganyiko kati ya kuwalipa wahudumu na wazee (wachungaji), na ukuhani wa waumini wote? Wote wawili, Petro na Yohana wanazungumzia ukuhani unaojumuisha waumini wote: "*Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu ...*" (1 Pet. 2:9). Yesu ame'**tufanya wafalme na makuhani** …" (Ufu. 1:6), katika ukweli halisi, jambo hili ni kufanywa upya kwa ukweli wa Agano la Kale, kwa kuwa sheria ya Musa ilishawatangaza tayari watu wa Mungu kuwa wao ni ukuhani wa jumla. "Nanyi mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani, na taifa takatifu" (Kut. 19:6, angalia Isa. 61:6). Ukuhani wa waumini wote katika Agano Jipya haupingi umuhimu wa wahudumu, wachungaji, na maaskofu, kama ambavyo ukuhani wa Wayahudi wote walioamini usivyopinga umuhimu wa Walawi, makuhani na makuhani wakuu katika Agano la Kale. Kama taifa, Israeli walikuwa na huduma ya ukuhani kwa ulimwengu, lakini ni kundi fulani tu la watu lililotekeleza jukumu hilo katika msingi wa weledi [kitaalamu]. Kanuni ile ile ni halali katika Agano Jipya.

Kwa sababu hii, Agano Jipya husisitiza nafasi maalumu ya ofisi za uongozi wa kanisa. Katika Wafilipi 1:1, kwa upande mmoja Paulo anawasalimu "*watakatifu wote katika Kristo Yesu, walio Filipi*", na kwa upande mwingine, (anawasalimu) kipekee "*maaskofu (au waangalizi) na*

*mashemasi*". Usihi unaotolewa kwa kanisa kujinyenyekeza chini ya watumishi wa muda wote uko wazi kabisa: "***Watiini wale wanaotawala juu yenu, na mwe wanyenyekevu, kwa kuwa wanafanya ulinzi wa roho zenu, kama watu watoao hesabu. Waacheni wafanye hivyo kwa furaha na si kwa huzuni, kwa kuwa hilo halitakuwa lenye faida kwenu*" *(Ebr. 13:17). "**… na kwamba wamejitoa nafsi zao kwa huduma ya watakatifu – hivyo ninyi pia jinyenyekezeni kwao, na kwa kila mmoja afanyaye kazi na kujitaabisha pamoja nasi**" (1 Cor. 16:15-16). "**Ndugu, tunawasihi mwatambue wale wajitaabishao miongoni mwenu, na walio juu yenu katika Bwana na kuwaonyeni, mkiwastahi sana katika upendo kwa ajili ya manufaa ya kazi yao***" (1 Thes. 5:12-13).

Akipinga maana ya neno "kiongozi wa kanisa" katika Kanisa Katoliki, John Calvin alipinga matumizi ya neno hilo, lakini aliandika:

> "Hata hivyo, ndani yake kulikuwa na taasisi takatifu sana na yenye kufaa sana, kiasi kwamba wale waliotaka kujitoa wenyewe na utumishi wao kwa Kanisa walipaswa kulelewa chini ya usimamizi wa askofu; ili kwamba hakuna mtu yeyote ambaye angeweza kutumika kanisani isipokuwa awe amefunzwa vema hapo mwanzo, isipokuwa katika maisha yake ya mwanzo amefunzwa mafundisho yafaayo, isipokuwa kwa njia ya nidhamu ya hali ya juu awe amejijengea tabia zenye mvuto mkubwa na maadili ya hali ya juu, akiwa amejiondoa katika masuala ya kawaida, na kujizoeza katika uangalizi na mafunzo ya kiroho.[5]

Katika Waefeso 4:1-16, aliongeza:

> "Kwa maneno haya alionesha kuwa huduma ya wanadamu, ambayo Mungu anaitumia katika kutawala kanisa, ni kifungo cha msingi ambacho waumini huwekwa pamoja katika mwili mmoja. Pia anatangaza waziwazi kuwa, Kanisa haliwezi kutunzwa kwa usalama, isipokuwa lisaidiwe na wale walinzi ambao Bwana amependezwa kuweka usalama wake juu yao …"[6]

Uasi wa Kora ni mfano katika Agano la Kale wa uelewa usio sahihi wa demokrasia. "*Wakainuka*' (au '***wakakusanyika pamoja***') dhidi ya Musa (Hes. 16:2, 11) kwa kuhoji madai ya ukuu wa Musa na sheria yake kwa kigezo kilichoeleweka kimakosa kuwa "wote ni watakatifu" (Hes. 16:1-13). Kanisa la mtaa hushiriki katika kuwateua wahudumu, wazee na maaskofu kupitia njia ya uchaguzi, lakini hili si tukio kuu, na haliwezi

---

5 John Calvin. *Institutes of the Christian Religion.* Translated by Henry Beveridge. Grand Rapids, Mich..: Willliam Eerdmans Publishing Co., 1994. p. 333 (Book IV, Ch. 4, Section 9)

6 *Ibid*., p. 317 (aus Book IV, Ch. 3. Section 2).

kamwe kupuuza muundo wa utawala uliobuniwa na Mungu. Hata hivyo, Yohana anamtumia Diotrefe kama mfano hasi wa kiongozi mmoja wa kidikteta, ambaye alitaka kulitawala kanisa (3 Yohana). Kwa hiyo, uongozi wa kiroho siyo leseni (angalia 1 Pet. 5:3, "***Kamwe si kama mabwana juu ya urithi wa Mungu, bali kama vielelezo kwa kundi***"). Kama tutakavyoona, pia inawezekana kuchukua hatua dhidi ya mzee.

Kwa mfano, baraza la kitume lilijumuisha viongozi wa muda wote wa makanisa ya mitaa. "***Basi mitume na wazee wakakusanyika kulishughulikia suala hili***" (Matendo 15:6). Hata hivyo, bado "kanisa lote" lilishiriki jukumu fulani bega kwa bega na wazee na mitume pia (Matendo 15:4, 22). Mwishoni mwa sinodi ya kwanza ya Kikristo tunaambiwa, "*Basi ikawapendeza mitume na wazee na kanisa lote kuwachagua watu miongoni mwao …*" (Matendo 15:22).

Hapa tena kuna makosa mawili ya kuepuka[7], kuinua mno ofisi ya uongozi wa kiroho na kuishusha hadhi sana ofisi hiyo. Ninaamini kwamba muundo wa kanisa wa Agano Jipya ulijumuisha ngazi tatu za uongozi (wahudumu, wazee na mkutano wa kikanda),[8] ingawa ni ngazi mbili tu zinazotumika. Juu ya wahudumu walikuwepo wapresbaiteri au wazee – viongozi wa kanisa la mtaa – na juu yao walikuwepo wale waliowajibika kwa makanisa kadhaa, kama vile Timotheo au Tito, ambao hawakuwa na 'ofisi' maalumu iliyofafanuliwa na Maandiko.

Madhehebu ya Kikatoliki, Kiothodoksi, Kianglikana, Kilutheri na baadhi ya yale ya Kimatengenezo wameendelea kutumia istilahi hii ya zamani "Ngazi za vyeo ni uaskofu [uepiskopo], uzee wa kanisa [upresbaiteri] na uhudumu [udaikoni]."[9] (Wakati matamko mbalimbali ya ukiri yanafasili kwa namna tofauti ngazi ya tatu, yaani ngazi ya juu kuliko kanda; na mimi ninaielewa ngazi hii kwa namna tofauti kabisa kuliko makanisa yaliyotajwa hapo juu yanavyoielewa).

---

7 Tazama Sura ya 5.B.2 Kuhusiana na Mkamilishano wa Wazo la Kibiblia.

8 Namshukuru Ray R. Sutton kwa kunipa nakala yake ya muswada ambayo haijachapwa iitwayo *Captains and Courts: A Biblical Defense of Episcopal Government,* 96 pp, Philadelphia (PA), 1992. Mbali na somo hili la Kimatengenezi na Kiepiskopo tazama mtazamo wa Kilutheri kuhusu maaskofu katika Karsten Bürgener, *Amt und Abendmahl und was die Bibel dazu sagt,* Selbstverlag: Bremen, 1985.

9 *Codex Iuris Canonici: Codex des kanonischen Rechtes: Lateinisch-deutsche Ausgabe,* Verlag Butzon & Bercker: Kevelaer, $1984^2$. p. 451 (Catholic Canon Law Can. 1009 § 1). Hata hivyo, kuna tofauti za kina kati ya mtazamo wa asili ya ofisi katika makanisa ya Kikatoliki, Kiothodoksi na Kiprotestanti kuhusiana na ofisi hizo tatu.

Ningependa kuanza na ngazi ya pili; kwa kuwa ofisi hii inawakilisha uongozi wa kanisa la mtaa, na kwa kuwa madhehebu mengi yanakubaliana katika mambo mengi yanayohusiana na ngazi hii. Kisha tutachunguza ngazi ya kwanza, yaani uhudumu, ambayo kwa ujumla nayo inakubalika sawia, ingawa itabidi tuingie kwa kina kidogo zaidi tunaposhughulika na suala la wahudumu wa kike. Hatimaye, tutajadili ngazi ya tatu na kuchunguza suala la uwepo wa mamlaka ya juu kuliko kanda juu ya makanisa-mtaa ya Agano Jipya. Suala hili litachukua sehemu kubwa zaidi, kwa sababu ya utofauti mkubwa wa fasili na utendaji miongoni mwa madhehebu mbalimbali.

## Ngazi ya Pili ya Utawala: Wazee (Wachungaji)

Agano Jipya hurejea kwenye ngazi ya tatu ya utawala kwa njia mbalimbali tofauti: ‘watawala’ (Ebr. 13:17), ‘wale walio juu yenu’ (1 Thes. 5:12). ‘wachungaji’ hawa ni wale ‘wanaochunga’ (Efe. 4:11), ‘wazee’ (Tito 1:5), na ‘waangalizi’ au ‘maaskofu’ (1 Tim. 3:1; Flp. 1:1). Vyeo vya ‘waangalizi’ na ‘maaskofu’ vinaweza kutumiwa kwa mbadilishano. Matendo ya Mitume sura ya 20 huwalezea ‘wazee’ (20:17) ambao wameteuliwa kama ‘waangalizi’ na ambao, sawasawa na wachungaji, wanapaswa kuliangalia kundi (20:28). 1 Petro 5:1-4 inawasihi wazee “kuchunga kundi la Mungu”; Mchungaji Mkuu ni Kristo na Petro ni mzee mwenzao. Tito 1:7 huzungumza juu ya ‘wazee’ wanaopaswa kuteuliwa, lakini katika mstari wa 5, Paulo anaelezea sifa zinazohitajika za ‘mwangalizi’.

Wazee walishiriki katika huduma ya muda wote, si tu katika kufundisha; na kwa kawaida walipokea mshahara. Hoja za kuwalipa watumishi wa kanisa walio katika nafasi za uongozi kwa kawaida katika mtazamo huu zilianzishwa na mitume, wazee na watumishi wasafirio. Wazee katika Kanisa la Agano Jipya walikuwa sawa na wachungaji wetu wa sasa, lakini hawakuwa sawa na watu wa kawaida tu waliohudumia kanisa kwa wakati wao wanapokuwa huru. Maandiko yanaweka usawa wa mshahara wa makuhani na walawi. Katika 1 Wakorintho 9:13-14, mishahara ya makuhani na walawi inatumika kuhalalisha ulipwaji wa wazee na mitume (Linganisha na Law. 6:16+26, 7:6+31 kuendelea, Hes. 5:9-10, 18:8-20+31) na hasa mstari wa 10, Kumb. 18:1-4. Linganisha na zaka.) Katika 1 Wakorintho 9:7-10, Paulo anarejea kwenye Kumb. 25:4, “**Au ni nani achungaye kundi na hanywi maziwa ya kundi hilo? Je, nasema mambo haya kama mtu wa kawaida tu? Au sheria haisemi vivyo hivyo pia? Maana imeandikwa katika sheria ya Musa,**

**“Usimfunge kinywa ng’ombe wakati apurapo nafaka.’ Je, Mungu anajishughulisha na ng’ombe mahali hapa? Au anasema hayo yote kwa manufaa yetu?**” Vile vile, katika 1 Timotheo 5:17-18, anarejea kwenye kifungu hicho hicho na kwenye maneno ya Yesu katika Mathayo 10:10, “**Acheni wazee watawalao vema wahesabiwe kuwa wenye kustahili heshima maradufu, hususani wale wajishughulishao na neno na mafundisho. Kwa kuwa Maandiko husema, ‘Usimfunge kinywa ng’ombe wakati apurapo nafaka.’ na mfanyakazi anastahili mshahara wake.**’” Kwa mujibu wa matamko haya, si tu wazee [mapresbaiteri] waliopaswa kulipwa, bali kimsingi ni kwa yeyote yule aliyeshiriki katika huduma na kubeba wajibu mkubwa zaidi na kupokea mshahara mkubwa zaidi.

Katika lugha asilia za Agano la Kale na Jipya, neno lililotumika kama ‘heshima’ lingeweza pia kurejea mshahara au fedha, kama ilivyo dhahiri katika suala hili mahali hapa. Tazama mifano ya matumizi ya neno hili katika umoja: Mat. 27:6; Matendo 5:2; 7:16; 1 Kor. 6:20, 7:23; katika wingi angalia: Matendo 4:34, 19:19). Mbali na hayo, Maandiko kwa kurudiarudia husisitiza kuwa fedha au vitu vinaweza kutumiwa ili kuonesha heshima. “**Mheshimu BWANA kwa utajiri wako, kwa mazao yako ya kwanza ya mazao yako yote**…!” (Mith. 3:9). Paulo anataja matoleo yaliyotolewa “**Kumheshimu Bwana mwenyewe**;” (2 Kor. 8:19), na anamsihi Timotheo kuwaheshimu wajane halisi kwa kuwapa kiinua mgongo[10] (1 Tim. 5:1-2) na anahusianisha kodi na forodha katika kuiheshimu Serikali (Rum. 13:7).

Mapokeo ya Kipresbaiteria ya zamani, ambayo mimi ni miongoni mwayo, mbali na uhakiki-kinzani wangu, hutofautisha kati ya ‘mzee afundishaye’ – mchungaji wa muda wote – na ‘mzee atawalaye’. Siamini kuwa utofauti huu unahalalishwa na mafundisho ya Agano Jipya, ambayo huwafanya wazee wote kuwajibika katika kufundisha na kushauri. Kihalisia, majukumu ya kijamii yanayotumia muda mwingi yaliachwa kwa wahudumu, ili kwamba wazee waweze kutumia nguvu zao katika kufundisha.

Pia Calvin anatofautisha kati ya mamlaka ya kinidhamu na mamlaka ya kimafundisho: kwa maoni yake hatua za kinidhamu katika Mathayo 18:15-18 zilipaswa kuchukuliwa na kanisa zima, likiwakilishwa na wazee walei,

---

10 Vgl. zur Altersversorgung als Ehrung der Eltern Lektion 15.5. zum 5. Gebot und Lektion 28.4.

wakati mamlaka ya kimafundisho yaliyofafanuliwa katika Mathayo 16, 19 na Yohana 20:23 yaliwekewa mpaka kuwa ya wachungaji tu.[11]

> "Kutoka kwenye ngazi ya uzee (upresbaiteri), baadhi yao walichaguliwa kuwa wachungaji na walimu, wakati wale waliobaki walipewa wajibu wa kutoa makaripio katika mambo ya mwenendo na nidhamu. Kwa wahudumu, walipewa kuwajali masikini na kugawa misaada.[12]

Elsie Anne Mckee amedhihirisha kuwa sababu ya msingi ya utofauti kati ya ofisi za muda wote na za muda uko katika ukweli kuwa, Waefeso 4:11 ilieleweka kuwa ilielezea ofisi badala ya wajibu au karama za kiroho.[13]

Tangu wakati huo, 1 Timotheo 5:17-18 imekuwa ikitumiwa kuwaainisha wazee katika makundi haya: wazee wanaotawala, wazee walei na wale wenye kufundisha, kwa sehemu kubwa wote hawa ni wazee wafanyao kazi muda wote; huu ni mtazamo ulioasisiwa na Calvin na ambao umekuwa sifa ya muda mrefu ya makanisa ya Kipresbaiteria ya kimatengenezo. Kabla ya Calvin, kifungu hiki kilikuwa kikifasiliwa kuonesha utofauti kati ya wazee wanaolipwa na wazee wanaolipwa vizuri zaidi, yaani wachungaji.[14] Homer A. Kent, akiandika juu ya 1 Timotheo 5:17, anasema:

> "Mstari huu hautoi kibali cha kutosha kwa mtazamo wa Kimatengenezo wa madaraja mawili ya wazee, wale walitawala na wale waliofundisha. Kila mzee huhusishwa katika kufundisha (3:2). Hata hivyo, wengine wangefanya hivyo kwa nguvu na kwa ubora zaidi kuliko wengine. Utofauti uliopo katika mstari huu ni kati ya wale wafanyao kazi kwa kuwa ni kazi tu na wale wanaojishughulisha hadi mwisho wa nguvu zao wakiendelea kutekeleza jukumu lao."[15]

Makanisa ya Matengenezo yameanza kuhoji fasili ya Kimatengenezo ya zamani ya 1 Timotheo 5:17, mbali na ukweli kwamba hiyo imekuwa sehemu muhimu na halisi ya theolojia yao.[16] Mwanatheolojia wa

---

11 Elsie Anne McKee. *Elders and the Plural Ministry: The Role of Exegetical History in Illuminating John Calvin's Theology*. Travaux d'Humanisme et Renaissance Librairie 223. Droz: Genf, 1988. pp. 28+33+62.

12 Johannes Calvin. *op. cit*., p. 328 (Book IV, Ch. 4, Section 1).

13 Elsie Anne McKee. *Elders and the Plural Ministry.* op. cit., pp. 162-165.

14 Ibid., pp. 88-89. Kitabu hiki hujumuisha kwa kina historia ya uhakiki-chimbuzi wa 1 Tim. 5:17 hadi mwisho wa Matengenezo.

15 Homer A. Kent. *The Pastoral Epistles.* Moody: Chicago, 1977 (repr 1958). pp. 181-182.

16 Elsie Anne McKee. *Elders and the Plural Ministry.* op. cit., pp. 103-114.

Kimatengenezo wa Agano Jipya Jan van Bruggen hakubaliani na mapokeo ya ki-Calvin katika hoja hii, kwa kuwa Agano Jipya, ukijumuisha na 1 Timotheo 5:17, hutaka tu kwamba wazee wote ni lazima wafundishe, na si kwamba kuna madaraja mawili ya wazee.[17]

Ulinganifu[18] wa sifa za wazee na waangalizi (Tito 1:6-9; 1 Tim. 3:2-3) na wahudumu (1 Tim. 3:8-12) unaonesha kwamba sifa pekee iliyohitajika tu kwa wazee, ilikuwa ni uwezo wa kufundisha: "**Hivyo, ni lazima askofu … aweze kufundisha**," (1 Tim. 3:2). Paulo anamweleza mzee kama mtu anayepaswa "**kushika kikamilifu neno aminifu [la kuaminiwa] kama alivyokwisha kufundishwa; ili kwamba, kwa mafundisho yafaayo, aweze kuwasihi na kuwashawishi wale wenye kuchanganya mambo**."

Agano Jipya kamwe haliwaiti maofisa wa kanisa, hususani wazee, 'makuhani', ingawa Paulo hutumia lugha ya kidini ya Agano la Kale kuelezea huduma yake (kwa mfano, Warumi 15:15-16), neno analolitumia kwa Wakristo wote (kwa mfano, Warumi 12:1. Angalia pia 1 Petro 2:5-9).

## Ngazi ya kwanza ya Utawala: Wahudumu wa Kiume na Wahudumu wa Kike

Ngazi ya kwanza ya uongozi hujumuisha wahudumu wa kiume na wa kike. Neno la Kigriki 'diakonos' mara nyingi linatafsiriwa kama '*mtumishi*' katika tafsiri mbalimbali, na kwa mujibu wa wahakiki-chimbuzi wengi, linatumika kama cheo rasmi cha 'mhudumu' katika matukio matatu tu. Kwa asili neno hili lilitumika kwa mtu aliyetumika kuhudumia mezani wakati wa chakula au aliyewahudumia wengine. Neno hili la Agano Jipya kwa ukaribu linahusishwa na kutumikia na utumishi kwa ujumla, na linaweza kueleweka tu kwa maneno hayo.

*Maana ya 1: Maana Asilia*: Neno '*mtumishi*' hujitokeza mara thelathini katika Agano Jipya, lakini ni mara chache tu linapoakisi maana yake ya

---

17 Jan van Bruggen. *Ambten in de Apostolische Kerken: Een exegetisch mozaik.* J. H. Kok: Kampen, 1984². pp. 98-104 und Jakob van Bruggen. „Apostolischer Gemeindebau: Widersprüchliche Ekklesiologien im Neuen Testament?". pp. 57-82 in: Helge Stadelmann (Ed.). Bausteine zur Erneuerung der Kirche. TVG. Brunnen: Gießen & R. Brockhaus: Wuppertal, 1998. p. 69. Ihm stimmt der Presbyterianer Reinhold Widter. *Evangelische Missionskirchen im nachchristlichen Europa.* Theologische Schriften 3. Evangelisch-Reformierte Medien: Neuhofen, 1999. pp. 85-86 zu.

18 Vgl. die Tabelle in William Hendriksen. *I & II Timothy & Titus.* New Testament Commentary. Banner of Truth Trust: Edinburgh, 1976 (Nachdruck von 1960/1957). pp. 347-349.

asili. Mathayo 22:13 na Yohana 2:5 ilitumia neno hili kuelezea juu ya wahudumu katika harusi. Katika Warumi 13:4, Paulo anawaita wenye mamlaka ya kiserikali 'watumishi'. Hata hivyo, mtazamo wa huduma za vitu na watu, haviachwi kabisa katika matumizi ya Agano Jipya, na hususani wakati wa kumteua '*mtumishi*' (mhudumu).

*Maana ya 2: Ufuasi kama Huduma:* Yesu alikuwa mfano halisi wa mtumishi, pamoja na kwamba Biblia haikutumia neno hili kwa uwazi kama cheo (Katika Warumi 15:8, Yeye ni "mtumishi wa Wayahudi (Kigriki: Tohara)", [neno] ambalo huelezea utii wake kwa desturi ya Kiyahudi). Kwa sababu hii, ufuasi hulinganishwa na huduma: "Yeyote anitumikiaye ni lazima anifuate; na mahali nilipo, na mtumishi wangu atakuwepo. Baba yangu atamheshimu yule ambaye hunitumikia". Hata hivyo, huduma za Wakristo kwa kiasi kikubwa ni tofauti sana na utawala wa kidunia (Mathayo 20:26; 23:11; Marko 9:35; 10:43; angalia pia Petro 5:2-4). Jinsi ambavyo utumishi au huduma humfurahisha Mungu au la hutegemeana na mtu ambaye huduma hiyo imewekwa wakfu kwake. Kuna watumishi wa Dhambi (Wagalatia 2:17) na watumishi wa Shetani ambao "**hujigeuza wawe kama watumishi wa haki.**"[19]

*Maana ya 3: Mhudumu:* Wakati kila Mkristo ni mtumishi, wajibu maalumu unaweza kubeba neno 'Huduma'. Paulo, ambaye anawajumuisha wasaidizi wake, yeye mwenyewe anajiona kama mhudumu, aliyewaongoza Wakorintho kwa Kristo (1 Kor. 3:5), kama mhudumu wa Agano Jipya (2 Kor. 3:6), kama mhudumu wa Mungu (2 Kor. 6:4), kama mhudumu wa Kristo (2 Kor. 11:23) au kama mhudumu wa Injili (Efe. 3:7; Kol. 1:23) au wa Kanisa (Kol. 1:25). Anatumia cheo hicho hicho kwa Tikiko ambaye pia ni mtumishi mwaminifu katika Bwana (Efe. 6:21) na "**mtumishi mpendwa** … katika Bwana" (Kol. 4:7). Epafra ni "**mtumishi mwenzetu mpendwa ambaye ni mhudumu mwaminifu wa Kristo kwa niaba yenu**," (Kol. 1:7), na Timotheo anashauriwa kuwa "**mhudumu mwema wa Yesu Kristo**" (1 Tim. 4:6). Katika mazingira haya neno 'mtumishi' au 'mhudumu' humaanisha mtumishi mwenza wa muda wote mwenye jukumu la uongozi katika kazi ya kanisa na ya umisheni.

*Maana ya 4: Ofisi ya Uongozi wa Kanisa.* Tukichukulia kuwa vifungu vinavyoelezea watumishi wa muda wote kama watumishi wa Mungu havirejei kwa ofisi maalumu, tunapata mifano michache ambapo "mhudumu" alishikilia kazi rasmi. Wafilipi 1:1 pamoja na salamu zake "***kwa watakatifu wote … pamoja na maaskofu na wahudumu***" ni ushahidi pekee wa wazi kuwa Kanisa la Agano Jipya lilikuwa na ofisi ya

---

[19] Tazama: 2 Cor. 11:14.

wahudumu sambamba na nafasi ya uongozi halisi wa wazee na waangalizi. Isivyotarajiwa, kifungu hakifafanui kwa uwazi zaidi juu ya ofisi hii. Katika 1 Timotheo, Paulo anaorodhesha si tu sifa za waangalizi, bali pia za wahudumu (1 Tim. 3:8-13). Sambamba na sifa za wazee na waangalizi (maaskofu), mhudumu anapaswa kuonesha tabia njema kwa huduma zao, uongozi mzuri wa familia zao na maisha yasiyo na lawama. Hata hivyo, Paulo anashindwa kufafanua wajibu wa wahudumu.

Je, “wanawake” katika 1 Timotheo 3:11 walikuwa ni wake wa wahudumu au walikuwa wahudumu wa kike? Naona hoja zenye kupendelea kuwa ni wahudumu wa kike kuwa zenye kushawishi zaidi[20]. Inaonekana muhimu kwangu kuwa Paulo hatupi orodha ya sifa za wake wa wazee wa kanisa. Kulikuwa na nini chenye kuhitajika zaidi kwa wake wa wahudumu kuliko wake wa wazee?[21] Ukweli kuwa Paulo anawapa wahudumu wa kike sifa za ziada kando na zile za wahudumu wa kiume, lakini si kwa ajili ya maaskofu au waangalizi wa kike; unaoana na Agano Jipya lote: wanawake waliweza kubeba kazi zenye wajibu, lakini hawakuwekwa wakfu [hawakuwekwa mikono] kama mababa wa kanisa moja au zaidi.

Warumi 16:1 huthibitisha kuwa kanisa lilikuwa na wahudumu wa kike. Foibe [Fibi] anaelezwa kama *“**dada, aliye mtumishi (au mhudumu) wa kanisa la Kenkrea**”*. Kwa vile mtindo wa kiume wa neno ndio umetumika, unaonekana kuelezea ofisi mahususi kuliko kutumika kama neno la jumla, ofisi iliyo wazi kwa wanawake. Mbali na hilo, nyongeza, “***wa kanisa la Kenkrea***” hudokeza kuwa Paulo anamaanisha ofisi katika kanisa maalum la mtaa, siyo aina ya huduma ya ujumla.[22] Mbali na hilo, pia Foibe anaitwa

---

[20] Tazama hoja katika Gerhard Lohfink, „Weibliche Diakone im Neuen Testament“, *Diakonia* 11 (1980) 1: 385-400 na Hermann Cremer, Julius Kögel, *Biblisch-Theologisches Wörterbuch des neutestamentlichen Griechisch,* F. A. Perthes: Stuttgart, 1923, p. 290. Thomas R. Schreiner, „The Valuable Ministries of Women in the Context of Male Leadership: A Survey of Old and New Testament Examples and Teaching“, pp. 209-224 katika: John Piper, Wayne Grudem (ed.), *Recovering Biblical Manhood and Womanhood,* Crossway Books: Wheaton (IL), 1991, huorodhesha katika kr. 213-214 hoja kwa ajili ya wahudumu wa kike, lakini [pia] zinafuata hoja dhidi ya hilo (kr. 219-221), ingawa anathibitisha katika uk. 220 kuwa tofauti kati ya ofisi ya wazee na wahudumu ni kwamba wazee hufundisha na kutawala wakati sivyo kwa wahudumu (1 Tim. 3, 2, 5).

[21] Tazama Gerhard Lohfink, *„Weibliche Diakone im Neuen Testament“*, op. cit., p. 396.

[22] Tazama Hermann Cremer, Julius Kögel, *Biblisch-Theologisches Wörterbuch des neutestamentlichen Griechisch,* op. cit., p. 290 na Thomas Schirrmacher, Der Römerbrief, vol. 2, op. cit., pp. 310-311.

προστάτις/prostatis (Kigiriki) ('Msaidizi' [=Mlezi wa kike]: Warumi 16:2), jambo ambalo husisitiza jukumu lake la kiofisi. Neno la Kigriki humaanisha 'mlinzi wa kike' au 'mlezi'[23]. Muundo wenye kufanana na huo uliashiria mlezi, mwenyekiti, [au] mshauri wa kisheria.[24]

Ofisi ya wahudumu wa kike ilikuwa ikijulikana vema katika Kanisa la Kibinzantini mpaka karne ya 11[25], na huko Rumi, Italia na katika Kanisa la Magharibi mpaka karne ya 5 na 6[26]. Pia kuna kumbukumbu za maandishi kwa ajili ya ofisi hii huko Magharibi mpaka karne ya 11[27]. Wamonofisti walikuwa na ofisi hii hadi karne ya 13[28], na kanisa la Mashariki lilitetea ofisi hii, wakimfuata Johannes Chrysostoms; wakati Katika la Magharibi liliiacha ili kukwepa kuwaweka wakfu wanawake, kwa mujibu wa Ambrosiaster na Erasmus Von Rotterdam[29].

Wahudumu hawa wa kike kwa dhahiri kabisa walifanya kazi za kiroho. Elsie Anne Mc Kee kwa usahihi anasema kuwa kuna ushahidi mkubwa, kwamba wahudumu wa kike waliajiriwa na kanisa na walihesabiwa miongoni mwa maofisa wa kanisa[30]. Hivyo basi, walishiriki hadhi, maslahi na mipaka ya watumishi wa kanisa kama haki ya kupewa mahitaji[31], kuwekwa wakfu[32] na useja[33], na wanatajwa katika Kanoni ya 19 ya Baraza la Nicea kwa sababu hii[34].

---

23 Walter Bauer, Kurt und Barbara Aland. *Griechisch-deutsches Wörterbuch zu den Schriften des Neuen Testaments* ... W. de Gruyter: Berlin, 1988[6]. Col. 1439

24 G. E. Benseler, Adolf Kaegi. *Benselers Griechisch-Deutsches Schulwörterbuch.* B. G. Teubner: Leipzig, 1926[14]. p. 794.

25 Adolf Kalsbach. Die altkirchliche Einrichtung der Diakonissen bis zu ihrem Erlöschen. *Römische Quartalsschrift*. Supplementheft 22. Herder: Freiburg, 1926, hususani kr. 63-71, ambamo mwandishi anajadili matatizo ya ujane, ubikra na ofisi ya uhudumu wa kike katika Kanisa la Kwanza.

26 Vgl. L. Duchesne. *Christian Worship: Its Origin and Evolution:* A Study of the Latin Liturgy up to the Time of Charlemagne. Soceity for Promoting Christian Knowledge: New York, 1931. pp. 342-343.

27 *Ibid.*, pp. 79-94 kwa kina.

28 Adolf Kalsbach. Die altkirchliche Einrichtung der Diakonissen ... op. cit., pp. 59-60.

29 Alles nach Elsie Anne McKee. John Calvin on the Diaconate and Liturgical Almsgiving. op. cit., pp. 161-163.

30 *Ibid*., p. 65.

31 *Ibid.*, p 66.

32 *Ibid.*

33 Wahudumu wa kike, sawa na makuhani, walitakiwa kubaki waseja, jambo ambalo Waprotestanti huliona kama [suala la] uwezekano [tu], lakini hawawezi kulichukulia kama sheria. Umuhimu wa kubaki mseja huthibitisha kuwa ofisi ya uhudumu wa kike ilieleweka kama ofisi ya kiroho.

34 *Ibid*., 46-49.

Tangu kipindi cha kanisa la kwanza, majukumu maalumu ya wahudumu wa kiume na wahudumu wa kike yamechukuliwa kutoka katika Matendo 6. Mitume wanatofautisha kati ya majukumu yao "tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile neno" (Matendo 6:4) na wajibu wa "kuhudumu mezani" na kuongoza shughuli hii (Matendo 6:2). Sifa kadhaa zinahitajika na uchaguzi unafanywa. Kwa hakika inaamriwa kutumia mfano huu kwa ajili ya mhudumu wa kiume, kwa kuwa mambo mengine katika Maandiko pia hujadili wajibu bila kuainisha wazi ofisi "husika". Wajibu wao ni muhimu, wala si cheo ambacho chaweza kubadilika.

Ulinganishi[35] wa sifa za lazima za wazee na waangalizi (Tit. 1:5-9, 1 Tim. 3:4-5) na wa wahudumu wa kiume (1 Tim. 3:8-12) huonyesha kwamba sifa pekee inayotakiwa kwa wazee juu na zaidi ya zile za wahudumu, ilikuwa ni uwezo wa kufundisha; "***aweze kufundisha***" (1 Tim. 3:2); [na] "***kushika kikamilifu neno aminifu [la kuaminiwa] kama alivyokwisha kufundishwa; ili kwamba, kwa mafundisho yafaayo, aweze kuwasihi na kuwashawishi wale wenye kuchanganya mambo***." Pamoja na hayo yote, wahudumu katika Matendo 6 waliteuliwa ili mitume na wazee wasiache "***maombi na huduma ya neno***".

Huduma ya kijamii ilikuwa ni kipaumbele cha kwanza cha wahudumu, lakini hili haliondoi uwezekano wa majukumu mengine. Wahudumu pekee katika Agano Jipya lote ambao kwao tunajifunza mengi ni Stefano (Matendo 6:8-7:60) na Filipo (Matendo 8:4-40). Wote walikuwa wainjilisti wachapakazi. Filipo alibatiza akiwa ni mhudumu (Matendo 8:12, 16, 36), lakini ni wazi hakufanya kazi ya kuwekea mikono iliyofuata baada ya ubatizo (kwa mfano, rejea Ebr. 6:2), kwa mitume, Petro na Yohana walikuja kama wawakilishi wa mitume wote huko Samaria kwa kusudi hili (Matendo 8:14-17). Pia walikuwa ni hawa mitume wawili, siyo Filipo, waliomtenga Simoni Magusi kutoka kanisani (Matendo 8:18-24).

Ulinganishi na Walawi wa Agano la Kale unabainisha zaidi jukumu la wahudumu. Chini ya makuhani, ambao ni viongozi halisi wa kiroho wa watu wa Mungu; Walawi walisaidia katika huduma na katika kufundisha, katika kuratibu ugawaji wa zaka na mahitaji kwa masikini, walishughulikia pia muziki na kazi nyingine.

Chini ya Clement wa Rumi na Ignatius wa Antiokia, kanisa liliendelea kutumia cheo 'mhudumu' kwa njia ya jumla lakini baadaye likakiwekea mpaka kwa ajili ya wajibu rasmi wa kutoa mahitaji kwa masikini, au kwa wasaidizi wakati wa Meza ya Bwana [Ekaristi], mara kwa mara wakisahau

---

[35] Tazama jedwali katika William Hendriksen, *I & II Timothy & Titus*, New Testament Commentary, Banner of Truth Trust: Edinburgh, 1976 (reprint from 1960/1957), pp. 347-349.

jinsi majukumu haya yanavyohusiana kwa ukaribu sana (chakula kwa wenye njaa na ulishaji wa kiroho kwa ajili ya kanisa wakati wa Ushirika [Meza ya Bwana]). Ni mpaka karne hii ofisi ya mhudumu ndipo ilipohuisha tena jukumu lake kwa ajili ya ushughulikiaji wa kivitendo wa mahitaji ya kanisani. Utendaji wa kanisa la sasa unachota jukumu la wahudumu wa kiume na wahudumu wa kike kutoka kwenye kazi zilizoelezwa katika Agano Jipya, ingawa muundo halisi wa Kibiblia mara nyingi haupo.

Katika makanisa mengi, uhudumu umekuwa maandalizi tu ya kazi ya uzee wa kanisa [upresbaiteri]. Hata hivyo, katika mwaka 1967 wakati wa Mtaguso wa Pili wa Vatikani, hata Kanisa Katoliki liliunda upya uhudumu kama ofisi inayojitegemea, ambayo inaweza kushikiliwa kwa muda mrefu au hata kwa maisha yote.[36] Kimsingi kutokana na maendeleo haya, wanawake hawakuruhusiwa kuwa wahudumu, kwa sababu uwekaji wakfu wa uhudumu kiuhalisia ungewaruhusu [wanawake] kuwa makuhani [wachungaji] au wazee vilevile.[37] Kwa hakika, uhudumu ni utangulizi wa kawaida kuelekea kwenye ukuhani, japo si lazima uelekeze huko. Kama Calvin alivyofanya, tunaweza kuuchukulia uhudumu kama "hatua kuelekea ukuhani"[38] pasipo kuufanya ukuhani kuwa matokeo ya lazima au kumtaka mhudumu kutafuta ukuhani siku chache zijazo.

Watengenezi hurejea kwa Calvin kama chanzo cha mafundisho yao ya ofisi ya kanisa, lakini tathmini yake ya kina ya ofisi ya mhudumu wa kiume na mhudumu wa kike imesahaulika kwa kiasi kikubwa.[39] Alichukua mwelekeo huu kutoka kwa Martin Bucer, na kwa mara ya kwanza alikutana nao huko Strassburg.[40] Sawa na Kanisa la Kwanza, aliichukulia Matendo 6:1-6 si tu kama taarifa, bali kama kanuni ya wakati wote.[41]

---

36 Tazama Rudolf Weigand, "Der ständige Diakon", p. 229-238 katika: Joseph Listl, Hubert Müller, Heribert Schmitz (ed.), *Handbuch des katholischen Kirchenrechts*, F. Pustet: Regensburg, 1983, p. 229.

37 Pia Leon Morris. "Church Government". pp. 238-241 katika: Walter Elwell (Hg.). *Evangelical Dictionary of Theology*. Baker Book House: Grand Rapids (MI), 1986 (Nachdruck von 1984).

38 Johannes Calvin. *Institutes of the Christian Religion,* op. cit., p. 349, (Book IV., Ch. 5, Section 15; Tazama pia Vol. IV, Ch. 3, Section 9).

39 Pia hususani Elsie Anne McKee. *John Calvin on the Diaconate and Liturgical Almsgiving*. a. a. O. p. 13; vgl. etwa Jean Calvin. Calvin-Studienausgabe. Bd. 2: Gestalt und Ordnung der Kirche. Neukirchener Verlag: Neukirchen-Vluyn, 1997. pp. 257-259 (aus Ordonnances ecclésiastiqes [1541/1561] pp. 227-279).

40 Elsie Anne McKee. *John Calvin on the Diaconate and Liturgical Almsgiving*. op. cit., pp. 129+153; Tazama pia dokezo kwenye kitini cha Bucer cha 1538, 'Von der Waren Seelsorge' katika uk. 179. McKee pia humtaja John Chrysostomos kama mtu aliyeshawishi mawazo ya Calvin kuhusiana na ofisi ya uhudumu (uk. 153).

Kwa makusudi, Calvin aliifufua ofisi ya mhudumu wa kike,[42] ambayo aliihalalisha kwa rejea za vifungu vya Agano Jipya ambavyo huzungumzia wahudumu wa kike,[43] lakini imeachwa kipindi chote cha Zama za Kati, kama ilivyo katika makanisa mengi ya Kiinjili ya sasa, ambapo mchungaji ndiye kiongozi halisi wa kanisa, ingawa kwa nadharia yeye ni mzee tu wa kanisa miongoni mwa wengi.

Kwa maoni yangu, makanisa mengi yatafanya vizuri kuongeza idadi ya wachungaji na kupunguza idadi ya wazee, kwa kuwa viongozi wengi walei hufanya wajibu wa kiutawala kwa ufasaha sawa na wahudumu au sawa na kamati ya kanisa. Kusimamia majengo, utunzaji vitabu vya fedha na ulipaji mishahara sio wajibu wa wazee wa kanisa, lakini [ni mambo] yanayochukua muda mwingi wa wazee wa kanisa katika makanisa mengi. Makanisa yanapaswa kuteua kamati, ambazo kwa msaada wa wahudumu, huhudumia masuala ya “kidunia”, ili kwamba wazee, ambao wanapaswa kuchaguliwa kufuatana na muda na uwezo wao wa kufundisha na kushauri, ni lazima waweze kujiweka wakfu wao wenyewe kwenye maeneo haya. Jambo hili lingemaanisha kuwa tungekuwa na wachungaji wengi zaidi, wanaolipwa mshahara au wasiolipwa, lakini tukawa na wazee wachache.

## Mapitio: Wajibu wa Kijamii katika Kanisa la Agano Jipya kwa Mujibu wa Matendo 6

Uteuzi wa wahudumu katika Matendo 6 na katika Kanisa la Agano Jipya kwa ujumla ni wenye umuhimu mkubwa. Inashangaza kuwa mbali na ofisi za waangalizi (maaskofu) na wazee, ambao walikuwa wanawajibika kwa uongozi na kufundisha, kanisa lilikuwa na ofisi nyingine moja tu, ile ya wahudumu wa kiume na wahudumu wa kike, ambao wajibu wao ulikuwa umetengwa kuwa wa kijamii kabisa. Wajibu wa kijamii wa kanisa kwa waumini wake umetaasisiwa zaidi katika ofisi ya wahudumu, hivyo kanisa bila wao ni kitu kisichofikirika kama ilivyo kwa kanisa bila uongozi au mafundisho ya Kibiblia.

1) **Kanisa hubeba kikamilifu wajibu wa kijamii kwa waumini wake, pale ambapo familia binafsi haiwezi kufanya hivyo**. Jukumu hili

Pia anaonehsa kuwa, kwa kumfuata Bucer, Calvin alitumia Warumi 12:8 kwa ofisi ya uhudumu, ambapo hakuna mtu yeyote afanyaye hivyo leo (uk. 185-204).

41 Elsie Anne McKee. *John Calvin on the Diaconate and Liturgical Almsgiving*. op. cit., p. 156.

42 *Ibid*, pp. 213-217.

43 *Ibid.,* pp205-210.

hujumuisha zaidi ya utoaji au msaada kwa ajili ya wachache, bali ni katika kuwajibika kwa wote.

2) Kwa hiyo kanisa ni lazima litofautishe waziwazi kati ya wajibu wake wa kijamii kwa Wakristo wenzao na wajibu wake wa kijamii kwa wengine. Wajibu ule wa kwanza umekwishataasisiwa katika ofisi ya wahudumu na ni jambo la daima, kwa kadri ya fedha na uwezekano uliopo (ikichukuliwa kuwa mtu hajaileta hali hiyo yeye mwenyewe). Mithali 3:27 huzungumzia matukio yote, "Usiwanyime watu mema yaliyo haki yao, ikiwa [yako] katika uwezo wa mkono wako kuyatenda". Wagalatia 6:10 huzungumzia wajibu wetu kwa watu wote, lakini husisitiza kipaumbele kwa mwamini. "Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waamini".
   Amri katika Mathayo 25:45 inapaswa pia kueleweka katika maana hii. Yesu anazungumzia waamini siyo kila mmoja. Kama "ndugu" waliotajwa katika mstari wa 40 walikusudiwa kumaanisha watu wote, basi hiki kingekuwa kifungu pekee katika Agano Jipya kinachotumia neno hili kwa lugha ya mafumbo kumaanisha mtu yeyote mbali na waamini wa kanisa au Wakristo wenzao.[44]
   Ulinganishi na suala la uletaji amani utasaidia kufafanua jambo hili. Maandiko yanawataka Wakristo kuishi kwa amani na waamini wenzao. Wasipofanya hivyo, basi uongozi wa kanisa unapaswa kuingilia kati. Kwa kadri uhusiano na wale wasio Wakristo unavyohusika, Paulo anasema, "Kama yamkini, kwa upande wenu, mkae katika amani na watu wote" (Rum. 12:18). Kanisa la Agano Jipya limejengwa juu ya agano linalowafunga waamini wote. Matarajio ambayo waamini wanatakiwa kuwajali watu wote huchipuka kutoka kwenye uelewa potovu wa uungwana na haki, kwa kuwa Biblia humtaka mwamini kuihudumia kwanza familia yake, kisha waamini wa kanisa la mtaa, na hatimaye kwa kanisa ulimwengu mwote. Ni pale tu wajibu huu unapotimizwa, ndipo anapokuwa na wajibu kwa watu wengine.

3) Matendo 6 hutoa kipaumbele kwa wajibu wa kijamii wa kanisa kwa waamini wake, lakini wajibu wa kutangaza Neno la Mungu na maombi hubaki kuwa muhimu zaidi na umetaasisiwa katika ofisi za wazee wa kanisa na mitume.
   Mitume wanatoa sababu ifuatayo ya kukataa kupokea "huduma" hii (Matendo 6:3), "na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia Neno" (Matendo 6:4). Maombi na utangazaji Neno la Mungu, mambo ambayo huwa pamoja daima, yana kipaumbele zaidi ya ushiriki wa kijamii na

[44] Kurt Hennig, „Beim Wort kommt es auch auf die Worte an“, *Das Fundament*, (DCTB) 1, l991, pp. 9-24 (uhususani kr. 22 na 19-24).

hayapaswi kuachwa. Mchanganyiko wa maombi na mafundisho si jambo jipya. Kwa mfano, hapo zamani ilikuwa ni huduma ya nabii Samweli “kuomba” na “kufundisha” (1 Sam. 12:23).[45]
Huduma kwa walio dhaifu kijamii pia ilichukuliwa kama suala muhimu katika Kanisa la Kwanza, ambapo kiulimwengu [kanisa] lilihifadhi fedha kwa ajili ya malengo ya kijamii.[46] Huduma kwa wajane ilikuwa ni mfano dhahiri.[47] Ukweli ni kwamba fedha nyingi zilitumiwa kwa mambo ya kijamii kuliko kwa mishahara ya wazee na wachungaji. Kwa mfano, kwa mujibu wa Baba wa Kanisa aitwaye Eusebius, kanisa katika Rumi mnamo mwaka 250 B.K., lilihudumia watumishi wa kanisa 100 na watu masikini 1500, hususani wajane na yatima. Alois Kehl anaandika, “Kamwe, katika zama zote za hapo kale, hakujakuwa na jamii au kikundi cha kidini ambacho kiliwahudumia waamini wake kama Kanisa la Kikristo lilivyofanya.”[48]

Arnold Angenendt anaongeza:

> “Kuwa Mkristo moja kwa moja humaanisha kufanya huduma za jamii. Kila kanisa la Kikristo lina “huduma zake za kijamii” na askofu hana budi kujithibitisha mwenyewe kuwa ni baba wa masikini. Hili lilikuwa jambo jipya katika ulimwengu wa kale – katika ulimwengu wote wa Kigriki na Kirumi, hakuna agizo lolote la kisheria lililowekwa wakfu kwa ajili ya mahitaji ya masikini.[49]

Hata hivyo, zaidi ya yote, wajibu wa matajiri kwa ajili ya huduma ya masikini, hauwapatii watoaji haki ya kipekee katika kanisa. Kwa sababu hii, Yakobo 2:1-13 inashambulia majaribio yao ya kuhujumu nafasi yao kanisani kwa nguvu.

---

45 Linganisha mwunganiko wa maombi na kukesha katika Neh. 4:9.

46 Adolf von Harnack, *Die Mission und Ausbreitung des Christentums in den ersten drei Jahrhunderten* (VMA-Verlag: Wiesbaden, o. J., reprint 1924$^4$), pp. 178-183, na sura, „Das Evangelium der Liebe und Hilfsleistung“, pp. 170-220.

47 *Ibid*. pp. 184-186.

48 *Ibid.* pp. 182-184.

49 Arnold Angenendt. *Heilige und Reliquien: Die Geschichte ihres Kultes vom frühen Christentum bis zur Gegenwart*. C. H. Beck: München, 1997$^2$. p. 48.

## Ngazi ya Tatu ya Uongozi (Sehemu ya Kwanza): Ukanisa–mtaa na Upresbaiteria

Katika hatua hii, tunahitaji kuchunguza ngazi ya tatu ya uongozi wa kanisa ya juu zaidi ya kanisa la mtaa. Hebu tuangalie miundo katika madhehebu ya Kiinjili.[50]

Makanisa yenye mwelekeo wa Kibaptisti kwa ujumla ni ya **ukanisa–mtaa**[51] katika muundo wake, hii humaanisha, "yanachukulia kanisa la mtaa kuwa kiini msingi na muhimu cha kanisa.[52]" Uongozi wa kanisa hujumuisha mfumo msonge wenye sehemu mbili tu, ambazo ni wahudumu na wazee, mara chache ofisi hizi hufanya kazi katika msingi wa muda wote. Juu ya kanisa la mtaa hakuna ngazi nyingine zaidi bali ni ile ya muungano wa juu juu wa makanisa (ambayo hutwaa kiasi fulani cha mamlaka yasiyokusudiwa kwa kuajili na kufundisha wahariri wa maandiko ya kanisa, marais wa seminari za kanisa n.k.).

Kuna miundo miwili tofauti ya ukanisa–mtaa. Ule wa hali ya juu sana unaweza kupatikana katika madhehebu kama vile ya Udugu, ambayo kinadharia hayakubali kabisa muundo wa juu zaidi ya kanisa la mtaa, lakini ukweli ni kwamba huruhusu kiwanda kimoja cha uchapaji au mchapaji na seminari moja kuamua juu ya theolojia yake na utendaji kazi wake. Mbali na hilo, ukweli kwamba makanisa ya mtaa yote yako chini ya dhehebu moja hudokeza dhana fulani ya uwajibikaji miongoni mwa makanisa hayo. Baadhi ya makanisa haya hayana viongozi kabisa, maamuzi yote hufanywa na waamini (ndugu). Katika makanisa mengine, walei hutumika kama maofisa, lakini wanaweza kuondolewa na kanisa muda wowote na kwa mara chache huajiriwa kama msingi wa utumishi wa wote. Watumishi wachache wa muda wote kwa kawaida ni "ndugu wanaotembea hapa na pale" ambao huhubiri katika makanisa mbalimbali, lakini hawana mamlaka juu ya kanisa la mtaa.

Aina ya pili ya muundo wa ukanisa–mtaa huruhusu ushirikiano wa juu juu wa makanisa ya mtaa (madhehebu), ambao huzaa vyuo, viwanda vya

---

[50] Kwa ulinganifu mzuri na mfupi ulio bora, tazama; Leon Morris, „Church Government," p. 218-241 katika Walter Elwell (ed.), *Evangelical Dictionary of Theology*. Baker Book House: Grand Rapids, Mich., 1996, kilichorudiwa kuchapwa tangu 1984.

[51] 'Ukanisa-mtaa' kutoka kwenye 'kanisa la mtaa', yaani kanisa la mtaa lina mamlaka ya mwisho katika mambo yote.

[52] John Huxtable. „Kongregationalismus." 452-462 katika: Gerhard Müller (Ed.). *Theologische Realenzyklopädie*. Vol. 19. de Gruyter: Berlin, 2000/1990 (Studienausgabe), p. 452. Kwa ajili ya historia ya Ukanisa-mtaa, tazama makala yote.

uchapaji au sinodi, lakini hudumisha uhuru asilia wa kanisa la mtaa. Wahudumu, wazee na wachungaji waliochaguliwa na kanisa hujitwalia mamlaka halisi kwa muda wote watakapokuwa kwenye ofisi hizo. Hivyo muundo huu hutumika kama mpito kuelekea kwenye mfumo wa kipresbaiteria.

Kwa kuwa Kanisa linaloonekana hujumuisha waamini wote wanaokubaliwa kwa msingi wa ukiri wa imani yao, mamlaka ya kanisa la mtaa kuchagua maofisa wake hayawezi kupingwa, lakini kama tulivyoona, ofisi ya mzee ni muhimu kwa uongozi wa kanisa, muundo usio na wazee ni ule usiohimilika. Kwa wakati ule ule, wazee hao kwa hakika ni maofisa wakuu kabisa kama ilivyo katika Agano Jipya na hawahitaji kuwekwa wakfu wala kuthibitishwa kimamlaka na kiongozi yeyote wa juu. Na wala kanisa la mtaa la Agano Jipya kwa wazi halimo katika mwungano mkubwa au kujitiisha chini ya mamlaka ya juu ili liwe "Kanisa" katika maana kamili ya neno. Mtazamo huu wa ukanisa-mtaa ni ukweli usiopingika wala usiopaswa kuachwa. Hata hivyo, tutaona kuwa, dhana hii haikatai uwezekano wa ushirikiano wa zaidi ya kanisa la mtaa kati ya makanisa ya kimtaa na ushirikiano wa uongozi wao wa kiroho; wala haizuii aina yoyote ya mwelekeo wa zaidi ya kanisa la mtaa unaozidi wazee wa kanisa na wachungaji. Ukweli ni kuwa, madhehebu mengi ya kimtaa yana muundo wa kiushauri wa Sinodi ambao hujumuisha wawakilishi wanaotumwa na kanisa la mtaa na hufanya kazi kama bodi ya uongozi–shirikishi.

**Makanisa ya Kipresbaiteria**[53] yana utawala wa kanisa wenye sehemu mbili tu (wazee na wahudumu), lakini huunda ngazi ya tatu ya uongozi kwa kuwakusanya wazee watokao katika sinodi mbalimbali za makanisa, pasipo kumpa mtu mmoja mamlaka kuu.[54] 'Katiba ya Sinodi ya Kipresbaiteria'

> "hueleza kanuni ya kikanisa ambayo imechimbukia ndani ya mapokeo ya Matengenezo ya karne ya 16, ambayo kwayo mamlaka ya kikanisa (utawala

---

53 Istilahi hii huonesha muundo wa utawala wa kanisa, lakini mara nyingi hutumika kuashiria Utengenezi (Reformed) tangu muundo huo ulipoimarishwa katika mapokeo hayo. Tazama; James K. Cameron. „Presbyterianism," pp. 340-359 katika: Gerhard Müller (ed.) *Theologische Realenzykopädie*. Vol 27. de Gruyter: Berlin, 2000/1997 (toleo la kitabu cha kufundishia).

54 Gerhard Troeger. „Bischof III: Das evangelische Bischofsamt". pp. 690-694 katika: Gerhard Krause, Gerhard Müller (ed.). *Theologische Realenzyklopädie*. vol. 6. Walter de Gruyter: Berlin, 1980, p. 693 anaandika, akimnukuu Hans Dombois: „Ukataaji wa Calvin wa ofisi ya askofu bado upo hai katika Kanisa la Matengenezo [Reformed Church], sawa na mzio dhidi ya kila aina ya mfumo wa kiofisi unaomtegemea mtu mmoja.

> wa kanisa) hukitwa katika bodi–shirikishi, ambamo wanatheolojia na wasio wanatheolojia hujadili na kutatua mambo nyeti."[55]
>
> "Kusudio la kitheolojia la katiba ya sinodi ya kipresbaiteria linapatikana kwa ushawishi unaokitwa katika Mathayo 18:15-20, kuwa kanisa linaweza kuongozwa na viongozi walei bila maaskofu au wafalme wa kanisa la mtaa. Yesu Kristo mwenyewe hutawala Kanisa lake kupitia Neno lake kwa njia ambayo huyakabidhi makanisa kazi fulani, hivyo basi Injili hufikishwa kwa watu wote kwa njia mbalimbali. Maofisa hawa na ofisi hizi zina mamlaka sawa, na kwa kuwa kila kanisa la mtaa ni Kanisa katika maana kamili ya neno, hakuna kanisa lenye nguvu juu ya jingine lolote. Sinodi mbalimbali zinazojumuisha wajumbe kutoka katika makanisa yote ya mtaa hutatua mambo yote ya kati ya kanisa na kanisa ili kukwepa kuruhusu ukuu wa ofisa yeyote au kanisa binafsi la mtaa."[56]

Mamlaka ya sinodi hutofautiana kutegemea kiwango cha mambo ambayo maamuzi yake huyafunga makanisa yote ya mtaa. Mipaka kati ya Ukanisa–mtaa na Upresbaiteria ni wa kubadilikabadilika katika hali hii. Katika baadhi ya vikundi vya Kipresbaiteria, wawakilishi kutoka katika sinodi hufanya ziara ili kuchunguza hali ya makanisa au kupima wanaotaka kuongoza pastoreti, lakini maofisa hawa hufanya kazi kama wawakilishi tu mkutano mkubwa na hawana mamlaka binafsi.

Wazo la sinodi kujumuisha maofisa na wawakilishi walei halikutokana na Calvin wala sinodi za mwanzo za Watengenezi,[57] ambazo zilikuwa makusanyiko tu ya wazee wa makanisa ya mtaa. Sinodi ya kwanza yenye mchanganyiko ilifanyika mwaka 1559 huko Paris, na Ujerumani ilifanyika mwaka 1571 huko Emden. Kuanzia mwaka 1610, sinodi za mchanganyiko zilifanyika huko Julich, Cleve, Berg na Mark.[58] Zote mbili, yaani sinodi na sinodi za mchanganyiko zilikuwa na msingi wa Kibiblia katika Baraza la Mitume la Matendo ya Mitume 15, ambamo mitume, wazee na kanisa walishiriki. "Basi ikawapendeza mitume na wazee na kanisa kuwachagua watu miongoni mwao na kuwapeleka…" (Mdo. 15: 22).

Ikiwa ni tukio la kipekee la kihistoria, Baraza la Mitume linatumika kama taswira halisi ya sinodi, lakini haliwezi kutumika kuidhinisha sheria

---

55 Joachim Mehlhausen. „Presbyterial-synodale Kirchenverfassung". pp. 331-340 katika: Gerhard Müller (Ed.). *Theologische Realenzyklopädie*. Vol. 27. de Gruyter: Berlin, 2000/1997 p. 331, Kuhusu asili na historia, tazama makala nzima.

56 *Ibid*., p. 331.

57 Irmtraut Tempel. Bischofsamt und Kirchenleitung in den lutherischen, reformierten und unierten deutschen Landeskirchen. Jus Ecclesiasticum: Beiträge zum Staatskirchenrecht 4. Claudius Verlag: Munic, 1966. p. 54.

58 *Ibid*., pp. 54-55.

isiyopingika. Hata hivyo, kumbuka kuwa Baraza lilikuwa na muundo wa kiutawala. Simoni Petro (Mdo. 15:7-10) na Yakobo (Mdo. 15:13-21) walikuwa na [kura ya] veto – Yakobo, kama mwenyekiti alifanya maamuzi ya mwisho (15:1-20), ambayo wengine walikubaliana nayo. Wazee wote waliotumika kwa muda wote na maofisa zaidi ya wale wa kanisa la mtaa walikuwepo: “Mitume na wazee wakakusanyika wapate kulifikiri neno hilo.” (Mdo. 15:6. Angalia pia Gal. 2:9 ambapo Yohana, Petro na Yakobo wanaitwa “nguzo”. Angalia pia 1 Kor. 9:5). Matendo ya Mitume 21:18 pia hutaja mkutano kati ya Paulo na sinodi ya wazee na Yakobo, kiongozi (askofu) wa kanisa huko Yerusalemu; “Hata siku ya pili yake Paulo akaingia kwa Yakobo pamoja nasi, na wazee wote walikuwapo”. Katika kiwango cha juu kabisa kunaweza kuwa na ngazi zaidi – kwa mfano, Yakobo aliliongoza Baraza, lakini hatujui kama alikuwa akiwawakilisha wengine au kama alikuwa na mamlaka juu ya wengine. Watumishi wenzake na Paulo akina Sila na Timotheo pia walipokea amri kutoka kwake (Mdo. 17:15). Mara kwa mara Agano Jipya hutaja ukweli kuwa, Paulo katika wajibu wa ‘kiepiskopo’, anatuma wasaidizi wake kwenye maeneo mapya ya huduma (kwa mfano, Timotheo katika Flp. 2:23 au 1 Thes. 3:2).

Kanuni ya kisinodi ya makanisa ya Watengenezi imechukuliwa na makanisa takribani yote duniani,[59] na ndiyo inayoamua wawakilishi wa mabaraza ya kikanda ya madhehebu ya Ukanisa–mtaa na wa mabaraza ya Kiaskofu.

Katika makanisa yote ya Kipresbaiteria na ya Ukanisa-mtaa, mchungaji wa muda wote hufanya wajibu maalumu, na wa kiungwana tofauti na wazee ‘wa kawaida’ wanaoongoza, na si kama ulivyokusudiwa katika muundo asilia, kama vile wa mzee mfundishaji katika kanisa la Kipresbaiteria; ingawa kinadharia na kisheria mchungaji yuko katika nafasi sawa kama wazee wengine.

Elsie Anne McKee ameonesha kuwa kwa hakika Wakalvini waliasisi ofisi tatu za uongozi: wachungaji, wazee na wahudumu;[60] na ofisi ya nne, ya mwalimu katika kanisa la Geneva.[61] Katika mwunganiko huu, mara kwa mara mchungaji hufanya kazi sawa na ile ya askofu, wakati kanisa hupinga rasmi wazo la uongozi wa kiepiskopo. Walau katika makanisa makubwa ya kimtaa, ofisi na kazi wa mchungaji mkuu huoana kwa ukaribu sana na

---

[59] Joachim Mehlhausen. „Presbyterial-synodale Kirchenverfassung”. op. cit., pp. 331-332.

[60] Elsie Anne McKee. *John Calvin on the Diaconate and Liturgical Almsgiving*. Travaux d‘Humanisme et Renaissance Librairie 197. Droz: Geneva, 1984. p. 134.

[61] *Ibid*., p. 135.

wajibu wa askofu katika Kanisa la Kwanza. Mbaptisti Johannes Jansen katika mwaka 1931 aliandika:

> Makanisa mengi yamemkomboa mhubiri kutoka katika mzigo wa kutawala kwa kuchagua wazee wawili au zaidi, ili yeye awajibike tu na mwelekeo wa kiroho.[62]

Makanisa mengi ya Kibaptisti yametatua tatizo kwa kumfanya mchungaji pekee kuwa mzee na kuwaita wale walio katika muundo wa utawala kama wahudumu, kama ilivyo katika makanisa ya Kikatoliki, Kiothodoksi na ya Kianglikana, ambapo mchungaji ni "kuhani" (imechukuliwa kutoka katika neno "Presbyter" lenye maana ya "mzee"). Maofisa wengine wote, kwanza wako chini ya mchungaji, kisha wako chini ya wahudumu. Katika hali zote, kanisa moja huwa na mzee mmoja tu, jambo linalowezekana, japo halipendekezwi.

Ukweli kuwa kitabu cha Ufunuo hutaja "Malaika wa kanisa" mara saba (Ufunuo 2:1+8+12+18; 3:1+7+14) mara kwa mara hutumiwa kuhalalisha utawala wa mtu mmoja, iwe ni mchungaji wa kanisa la mtaa au askofu. Maana ya neno imekuwa ikibishaniwa na kutafsiriwa kwa njia nyingi kiasi kwamba kifungu hicho hakiwezi kutusaidia kama hoja toshelevu.

## Ngazi ya Tatu ya Uongozi (sehemu ya pili): Uepiskopo

Mtazamo kuwa kanisa la kwanza lilikuwa na viongozi wataalamu waliowajibika kwa makanisa mengi na kwa wazee wao, unaitwa wa 'kiepiskopo', kwa sababu kanisa la kwanza lilikuwa limeanza kuipa kazi hii miongoni mwa makanisa jina la 'askofu'. (kihalisia, 'mwangalizi': Kigriki, 'episcopos' ambalo ni asili ya neno 'bishop' = 'Askofu'), tofauti na neno 'mzee' (Kigriki, 'presbyter', ambayo ni asili ya neno 'priest' = 'Kuhani', ambalo humaanisha wachungaji wa kanisa la mtaa).[63]

---

62 Johannes Jansen. Gemeinde und Gemeindeführung: Episkopat, Presbyterium oder Demokratie? Gemeinde und Gegenwart 2. J. G. Oncken: Kassel, 1931. p. 5.

63 Juu ya maendeleo ya neno 'askofu' katika Dini ya Kiyahudi, katika Agano Jipya na katika Kanisa la Kwanza, tazama: Hermann Beyer. „episkeptomai ... episkopos ... ". pp. 595-619 katika: Gerhard Kittel (Ed.). Theologisches Wörterbuch zum Neuen Testament. Bd. II. W. Kohlhammer: Stuttgart, 1990 (repr from 1935), hapa ni kr. 604-617; na Theo Sorg, F. O. July. „Bischof/Bischofsamt". pp. 279-281 katika: Helmut Burkhardt, Uwe Swarat (Ed.). Evangelisches Lexikon für Theologie und Gemeinde. Vol. 1. Brockhaus: Wuppertal, 1992.

Ndani ya makanisa ya Kiepiskopo, mamlaka ya askofu hutofauiana. Mamlaka haya hupungua kadiri tunavyoendelea kutoka katika uwezo wa kisakramenti na kisheria wa askofu wa kanisa la Katoliki la Rumi kwenda kwa askofu wa Kiothodoksi, Kianglikana,[64] Kilutheri hadi kwa wa Kimethodisti, ambao kazi zao ni za kiuwakilishi na ushauri kuliko zile za kisheria.

Kama tulivyoona, vyeo vya ‘mzee’ na ‘mwangalizi’/‘askofu’ vinaweza kutumika kwa mbadilishano. ‘Mwangalizi’ huelezea kazi ya uongozi ya wazee (Matendo 20:28, 1 Tim. 3:2, Tito 1:7, Flp. 1:1- “maaskofu na mashemasi” bila uanishaji zaidi. Katika 1 Pet. 2:25, Yesu anaitwa “Mchungaji na mwangalizi wa roho zenu”. Pia tunapata neno “ofisi ya mwangalizi” (Kiyunani, ‘episcope’) inatumiwa kuelezea ofisi ya mtume (Matendo 1:20) na vilevile kuelezea ofisi ya mzee (1 Timotheo 3:1, “mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema.”).

Adolf Schlatter anadhani kuwa Tito 1:5+7 ilitofautisha kati ya maaskofu na wazee, na kuwa Paulo aliwachagua maaskofu kutoka miongoni mwa ofisi ya uzee wa kanisa.[65] Leonard Goppelt, katika kujifunza Nyaraka za Kichungaji, anafikia hitimisho kuwa kila kundi la wazee liliongozwa na mwangalizi (‘askofu’).[66] Vilevile, Ray R. Sutton anaamini kuwa Tito 1 inaelezea sifa za maaskofu, ambao wanapaswa kuwa vielelezo kwa wazee na wanawajibika kwao.[67] A. M. Farrer anapinga kuwatofautisha wazee na waangalizi katika Agano Jipya na anaweka kazi ya uangalizi iliyotajwa katika Matendo 20:17-18+28 kwa wazee. Anaona wazo hili kwa uwazi zaidi katika 1 Petro 1:5-4 na katika Waebrania 12:14-15,[68] mahali pekee ambapo kitenzi ‘kuangalia’ kinatumika. Anaigawa Tito

---

64 ‘Makanisa yanayoendelea’, yaani makanisa huru ambayo yamechukua yenyewe ofisi yao ya askofu kutoka kwa Kanisa Anglikana na kuwaweka wakfu maaskofu wao kwa kuwawekea mikono. Kwa kiasi fulani, makanisa haya hulazimisha aina ileile ya utii kwa askofu kama Kanisa Katoliki lifanyavyo.

65 Adolf Schlatter. Die Kirche der Griechen im Urteil des Paulus: Eine Auslegung seiner Briefe an Timotheus und Titus. Calwer Verlag: Stuttgart, 1958². p. 182 (tazama pia: pp. 181-183).

66 Leonhard Goppelt. „Kirchenleitung und Bischofsamt in den ersten drei Jahrhunderten”. pp. 9-33 katika: Ivar Asheim, Victor R. Gold (Ed.). Kirchenpräsident oder Bischof? Untersuchungen zur Entwicklung des kirchenleitenden Amtes in der lutherischen Kirche. Vandenhoeck & Ruprecht: Göttingen, 1968. p. 21.

67 Ray Sutton. Captains and Courts, op. cit., p. 84.

68 A. M. Farrer. „The Ministry in the New Testament”. p. 113-182 in: Kenneth E. Kirk. The Apostolic Ministry: Essays on the History and the Doctrine of Episcopacy. Hodder & Stoughton: London, 1957 (expanded repr. from 1946). pp. 134-141.

1:5-7 katika orodha moja ya sifa za wazee na orodha nyingine kwa ajili ya sifa za waangalizi, lakini anapendekeza kuwa mstari wa 6 hauhusiani na wazee, bali uko katika sehemu inayofuata, kwa kuwa maelezo “ikiwa mtu…” (Kigriki: ei; ti,j) yametumiwa mara nne katika Nyaraka za Kichungaji kutambulisha aya mpya (1 Tim. 3:1; 5:4+16; 6:3).[69] Mitazamo hii inaweza kuwa halali, lakini haishawishi – hoja zao kwa kiasi ni jaribio lazimishi la kusoma istilahi mpya kwenye Agano Jipya. Kuteuliwa kwa Timotheo kama mwangalizi kungeweza kuwa uthibitisho wenye ushawishi zaidi kwa uwepo wa ngazi ya mamlaka zaidi ya ile ya kanisa la mtaa iliyo juu ya wazee katika karne ya kwanza.

Septuaginta, ambayo ni tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale, hutumia neno lile lile, ‘episkopos’ au “mwangalizi” kuwaita ‘waangalizi’ wa wana wa Benyamini. Waangalizi wa wana wa Benyamini (Neh. 11:9, 14, 22), na vile vile waangalizi wa wajenzi wa Hekalu (2 Nya. 2:2; angalia pia 2 Nya. 34:17 na linganisha kitenzi katika mstari wa 12.) na maofisa wa kisiasa.[70] Katika hali hizi, ‘episkopos’ huashiria ofisi ya kawaida, siyo ofisi kuu katika mfumo msonge.

Hivyo, ushahidi wa Agano Jipya kamwe hauthibitishi wala haupingi matumizi wa neno ‘askofu’ au ‘episkopo’, lakini jina au cheo hiki daima kimekuwa chenye kukanganya miongoni mwa Wakristo. Kwa upande mwingine, muundo unaovuka mipaka ya kikanda ulidumishwa kwa karne kadhaa baada ya matengenezo, na hata kwa makanisa ya Kianabaptisti, waliodumisha aina fulani ya muundo unaovuka mipaka ya kikanda ili kutoa usimamizi muhimu wa wachungaji wake. Suala si, kama *neno* lenyewe ni la Kibiblia, bali ni kama *ofisi* hii ilikuwepo katika kanisa la Agano Jipya.

Mara kwa mara Agano Jipya hutumia cheo kimoja kuashiria aina mbalimbali za ofisi, na Yesu mara kwa mara alipewa vyeo vilivyotumiwa kwenye ofisi nyingine na majukumu mengine katika Kanisa. Mitume ni “wazee wapendwa” tu lakini wana mamlaka juu ya wazee wengine, lakini pia kwa urahisi waliweza kujiweka katika kundi la wazee. Wazee walipokea kiwango fulani cha mamlaka kutoka kwa Mungu, lakini walibaki kama ndugu tu: “Nawasihi wazee walio kwenu… lichungeni

---

69 Ibid., p. 160.

70 Tazama: Johannes Neumann. „Bischof I: Das katholische Bischofsamt“. pp. 653-682 in: Gerhard Krause, Gerhard Müller (Ed.). Theologische Realenzyklopädie. Vol. 6. Walter de Gruyter: Berlin, 1980. p. 653 und Hermann Beyer. *„episkeptomai ... episkopos...”*. op. cit., p. 611. Neumann ananukuu mifano kutoka katika utamaduni wa Kigriki.

kundi la Mungu… wala si kama wajifanyao mabwana… bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi." (1 Pet. 5:1-5).

Hakuna anayebisha ukweli kuwa mitume walikuwa viongozi wa kanisa waliowajibika katika eneo kubwa la kijiografia, na ya kuwa walichagua wazee wa kwanza katika kila eneo. "Na walipokwisha kuwachagulia wazee katika kila kanisa, na kuomba pamoja na kufunga, wakawaweka katika mikono ya Bwana waliyemwamini." (Mdo. 14:23).

Kwa kuwa wengi hudhani kuwa ofisi ya kitume iliishia kwa wale mitume kumi na wawili, tunapaswa kujiuliza iwapo wajibu unaovuka mipaka ya kikanda ulikuwa ni wa kwao tu au angalau ulienda mpaka kwa warithi waliowafuatia au kama ulichukuliwa na ngazi ya tatu ya uongozi. Kwa sababu, kwa kiasi karibu chote hatujui lolote juu ya wasaidizi wa mitume, isipokuwa kwa washirika wa Paulo waitwao Timotheo na Tito, na hakuna chochote juu ya shughuli zao za baadaye, tunaweza kuuliza tu wajibu upi Timotheo na Tito waliokuwa nao na ni wajibu upi wa Paulo, ambao waliuchukua baadaye. Cha kusikitisha, hili ni jambo ambalo halijachunguzwa kiasi cha kutosha katika mijadala ya ngazi za kanisa.

Utendaji kazi wa kitume na hasa ule wa kanisa la Yerusalemu, kwa kadiri maandiko yanavyotaarifu, huchukuliwa kuwa kielelezo kwa makanisa yote ya Yesu Kristo, kama Paulo anavyoliandikia kanisa huko Thesalonike, "*Maana ninyi, ndugu, mlikuwa wafuasi wa makanisa ya Mungu yaliyo katika Uyahudi, katika Kristo Yesu"*(1 Thes. 2:14). Kando ya hilo, hatupati tu taarifa za Agano Jipya kuelezea muundo wa kanisa na masuala ya uongozi, bali – hasa katika nyaraka za kichungaji (Waraka wa Kwanza na wa Pili wa Timotheo, Tito) – pia tunapata maelekezo halisi juu ya maelezo ya sifa muhimu ya kanisa katika muundo na masuala ya uratibu. Ni kwa namna gani mitume walivyojishughulisha na ukweli kuwa hawakuwa na uwezo wa kufanya uangalizi juu ya baadhi ya maeneo kwa sababu walishiriki kufanya uinjilisti kila mahali? Walifanya nini katika kulipatia kanisa uongozi wakati wa vifo vyao? Kwa uwazi, waliwaweka wakfu warithi wao kwa kuwawekea mikono juu yao, ili watu hawa waweze kuyaangalia makanisa na wazee wake. Warithi wanaojulikana sana ni wale waliopokea Nyaraka za Kichungaji, yaani Timotheo (Mdo. 16:1-3; 17:13-15; 19:21-22; 20:3-4; Rum. 16:12; 1 Kor. 4:17; 15:10-11; 2 Kor. 1:1; Flp. 1:1; 2:19-21: Kol. 1:1 ;1 Thes. 1:1; 3:1-8; 1 Tim. 1:1-2+18; 3:14-15; 5:23; 2 Tim. 1:1-2+5-6+8; 3:10; 4:9-22; Flm. 1:1 ; Ebr. 13:23) na Tito (2 Kor. 2:12-13; 7:6-7+12-16; 8:16-24; 12:16-18; Gal. 2:1-4; 2 Tim. 4:10; Tito 1:1-5; 1:1+15; 3:9+15).

Kimsingi, Timotheo aliwekwa wakfu kwa kuwekewa mikono na wazee (1 Tim. 4:13-15; Angalia pia 1:18), lakini inawezekana baadaye aliwekwa

wakfu na Paulo katika ofisi ya juu (2 Tim. 1:6) – ama sivyo mistari yote iwe inarejea kwenye tukio lile lile – kama ilivyo kuwekwa wakfu mara zote hufanywa na ofisa wa juu (Mdo. 1:24; 6:6; 13:3).[71] Kuwekwa kwake wakfu na Paulo kunaonesha wazi kuwa alichukua wajibu wa mtume. Katika Agano la Kale warithi waliwekwa wakfu kwa kuwekewa mikono (mf. Musa na Yoshua; Eliya na Elisha).[72]

Tito alipaswa "**kuteua wazee**" (Tito 1:5) na kuwapinga walimu wazushi ndani ya makanisa, na aliwajibika kwa makanisa yote ya Krete (Tito 1:5). Timotheo alikuwa na kazi ile ile na aliwajibika huko Efeso na maeneo yaliyoizunguka (1 Tim. 1:3).

Neno lililotumika kwa ajili ya "teua" (Kigriki, 'cheirotonoeein') laweza kumaanisha 'mtu kuinua mkono wake wakati wa kupiga kura' au 'kumnyooshea [kidole] mtu', ikimaanisha 'kumchagua mtu' au 'kuteua'.[73] Katika 2 Wakorintho 8:19, neno hili huashiria uchaguzi wa mwakilishi uliofanywa na kanisa. Matendo 14:23 hutumia neno hilo hilo kuelezea uchaguzi na uwekaji wakfu wa wazee uliofanywa na mitume, inawezekana linakusudiwa kwa uchaguzi ufanywao na kanisa, na uthibitishaji na uwekaji wakfu unaofanywa na mitume.[74] Ni dhahiri mitume walipendekeza wagombea kadhaa, ambao kutoka miongoni mwao kanisa lilimchagua mtu ambaye aliwekwa wakfu na mitume. Mchakato huu unatumiwa mara kwa mara katika Biblia wakati ofisi za kikanisa au kisiasa zinapotakiwa kujazwa: Mkubwa hupendekeza wagombea, kisha wafuasi wake humchagua ofisa mhusika. Mfano bora ni ule wa uteuzi wa wahudumu wa kwanza katika Matendo 6:1-6.

Wajibu wa Timotheo kwa makanisa mbalimbali na hasa kwa wazee wa makanisa hayo unaweza kuonekana katika 1 Tim. 5:19-21: "Usikubali mashitaka juu ya mzee, ila kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu. Wale wadumuo kutenda dhambi uwakemee mbele ya wote, ili na wengine waogope. Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, na mbele

---

71 Tazama pia: Eduard Lohse. *„cheir, ... cheirotoneo".* pp. 413-427 katika: Gerhard Kittel (Ed.). Theologisches Wörterbuch zum Neuen Testament. Vol. II. W. Kohlhammer. Stuttgart, 1990[2], hapa ni kr. 417-418+420-423.

72 *Ibid.,* p. 418.

73 Walter Bauer, Kurt und Barbara Aland. Griechisch-deutsches Wörterbuch zu den Schriften des Neuen Testaments... W. de Gruyter: Berlin, 1988[6]. Col. 1757; Eduard Lohse. *„cheir, ... cheirotoneo".*op. cit., p. 426-427.

74 Josef Bohatec. Calvins Lehre von Staat und Kirche: mit besonderer Berücksichtigung des Organismusgedankens. Untersuchungen zur Deutschen Staats- und Rechtsgeschichte 147. M. & H. Marcus: Breslau, 1937 [=Josef Bohatec. Calvins Lehre von Staat und Kirche: mit besonderer Berücksichtigung des Organismusgedankens. Scientia: Aalen, 1968 (Repr of 1937)]. p. 478.

za malaika wateule, uyatende hayo pasipo kuhukumu kwa haraka; usifanye neno lolote kwa upendeleo". Hapa Timotheo, kama mzee mkuu (askofu) juu ya makanisa mengi, anashughulika na mashtaka dhidi ya wazee wa makanisa ya mtaa. Jukumu hili lina mtazamo wa unaomhusu mtu binafsi [na] halifai kwa kamati au sinodi. Askofu Timotheo yuko juu ya wote, yaani walimu na washauri na hata wachungaji (wazee). Ni nani anayejishughulisha na uongozi wa kanisa? Ni nani anayewapatia 'uangalizi wa roho' ikiwa mamlaka yavukayo mipaka ya kikanda yamejumuishwa tu kwenye kamati, ambazo hufanya maamuzi, lakini haziwezi kujishughulisha na mahitaji binafsi ya mtu na ya kiroho?

Timotheo na Tito walitekeleza kazi hii ya kiepiskopo wakati wa maisha ya mitume. Kabla ya Paulo, wengine walikuwa wameshafanya hivyo. Kwa mfano, Barnaba aliwaweka wakfu wazee pamoja naye (Matendo 14:23). Kuwapo kwa chombo kinachoongoza makanisa mbalimbali kunaweza kuonekana huko Yerusalemu, ambapo Yakobo ni askofu na mwenyekiti wa baraza la Kiepiskopo. Wale kumi na wawili waliongoza kanisa lote chini ya uelekezi wa Petro; Yakobo na wazee walioongoza kanisa huko Yerusalemu,[75] na Yakobo kama mchungaji mkuu wa kanisa–mama huko Yerusalemu, alikuwa ni mheshimiwa mwenyekiti wa Baraza la Kitume.

Kwa ujumla nyaraka za Kichungaji hupewa tarehe za baadaye, lakini mfumo ya Kiepiskopo tayari unafanya kazi[76] (jambo ambalo lina ukweli zaidi, iwapo tutazipa Nyaraka za Kichungaji tarehe za baadaye).

Nimejishughulisha na kushindwa kwa Uprotestanti, siyo tu wa kambi ya Kilibelali, [bali] kwa kujifunza kwa bidii nyaraka za Kichungaji na wazo lao la baadaye la mfumo wa kikanisa usio wa ki–Paulo 'katika tasnifu yangu ya Kitheolojia[77], kwa kuwa ukataaji wa Emil Bruner wa jinsi

---

[75] Leonhard Goppelt. „Kirchenleitung und Bischofsamt in den ersten drei Jahrhunderten". op. cit., p. 13.

[76] Z. B. Gerhard Tröger. Das Bischofsamt in der evangelisch-lutherischen Kirche. Jus Ecclesiasticum: Beiträge zum Staatskirchenrecht 2. Claudius Verlag: München, 1966. pp. 20-21; Leonhard Goppelt. „Kirchenleitung und Bischofsamt in den ersten drei Jahrhunderten". op. cit., pp. 19-20.

[77] Thomas Schirrmacher. Das Mißverständnis des Emil Brunner: Emil Brunner's Bibliologie als Ursache für das Scheitern seiner Ekklesiologie. Theologische Untersuchungen zu Weltmission und Gemeindebau. ed. von Hans-Georg Wünch and Thomas Schirrmacher. Arbeitsgemeinschaft für Weltmission und Gemeindebau: Lörrach, 1982. 54 p.; Revised and abbreviated in: „Das Mißverständnis der Kirche und das Mißverständnis des Emil Brunner". Bibel und Gemeinde 89 (1989) 3: 279-311 and „Zur neutestamentlichen Gemeindestruktur: Ergänzungen zu 'Das Mißverständnis der Kirche und das Mißverständnis des Emil Brunner'". Bibel und Gemeinde 90 (1990) 1: 53-62.

Agano Jipya linavyoshughulika na ofisi ya kanisa, hutegemea sana na ukataaji wake wa Nyaraka za Kichungaji. Hili limenifanya mimi kushughulikia nyaraka hizi kwa umakini wa kina, ukweli wake na mafunzo yake kuhusu kanisa.[78] Bado sijapata sababu ya kushindwa kwake kabisa kutambua jukumu la Timotheo na Tito kama maofisa wa kanisa juu ya maofisa wa makanisa ya mitaa, na kushusha hadhi ya jukumu la ofisi ya uhudumu, kama nitajavyo katika toleo langu la kwanza la *Ethik.*[79] Jambo hili linahitaji utafiti zaidi, na natumaini kuwa mawazo yangu yatachochea mjadala zaidi.

Tunaweza kuhitimisha nini kutoka katika uelewa wetu wa Timotheo na Tito?

1) Timotheo na Tito walikuwa na mamlaka ya kiroho na wajibu wa kushauri ndani na juu ya makanisa ya mtaa, lakini shughuli zao hazikufungwa na ofisi yoyote maalumu. Vilevile tunaweza kuonesha kwa uwazi kuwa wahudumu na wazee/waangalizi (Kigriki: ‘presbyteros’, ‘episkopos’) zilikuwepo kama ofisi maalumu ambazo hazikuundwa kwa majina maalumu, Maandiko kamwe hayaundi ofisi yoyote ya tatu yenye aina yoyote ya jina iliyobebwa na watu hawa wawili. Kwa sababu hii, nayachukulia majukumu yao kama hoja dhidi ya uundaji wa ofisi ya tatu yenye kazi dhahiri na yenye maeneo ya mamlaka, japo nauamini wajibu wao kwa ulinzi wa kiroho kuwa ni muhimu, hususani kwa usambazaji wa Injili.
2) Ingawa hakuna neno la mwisho linaloweza kutajwa juu ya jambo hili, naamini kuwa kazi zao huko Krete na Efeso inawezekana zilifanana na majukumu yaliyofanywa baadaye na wachungaji. Hawakuwa maaskofu katika maana ya sasa ya neno bali wachungaji. Hilo linaweza kueleza ukweli kuwa hakuna nyaraka za kihistoria za mfumo wa kiepiskopo katika Kanisa la Kwanza uliotolewa kutoka nyaraka za kichungaji. Maaskofu wa Kanisa la Kwanza walijipatia ofisi zao kutoka katika warithi wa mitume, lakini wanaoonekana kuwa walikuwa maofisa wa kanisa la mtaa juu ya wazee, na siyo maaskofu wa kikanda wenye mamlaka ya kisakramenti.

---

78 Tazama: Thomas Schirrmacher: „Die Pastoralbriefe Factum” 3+4/1984: 9-10 and „Plädoyer für die historische Glaubwürdigkeit der Apostelgeschichte und der Pastoralbriefe”. a. 181-235/254 in: Heinz Warnecke, Thomas Schirrmacher. War Paulus wirklich auf Malta? Hänssler: Neuhausen, 1992.

79 Thomas Schirrmacher. Ethik. Band 2. Lektion 44. Hänssler: Neuhausen, 1994[1]. pp. 525-566, especially pp. 532-546, Abbreiviated as article: „Die drei Ebenen der neutestamentlichen Leitungsstruktur”. Anstöße – Beilage zu Neues vom Euroteam 1/1994: 1-4.

3) Ninaamini kuwa majukumu ya Timotheo na Tito nje ya kanisa la mtaa ndani ya mfumo wa vuguvugu la kimishenari linalokua zinapaswa kueleweka kama sura moja ya upanuzi wa dhana ya utume ya Agano Jipya, ambazo tunapaswa kuzichunguza kwa umakini mkubwa.

## Hoja Tisa kuhusu Muundo wa Kanisa na Uongozi

Ningependa kuhitimisha kwa hoja tisa juu ya somo hili, na [kwa] wito wa uongozi wa kiroho.

1) **Suala la muundo wa kanisa la Agano Jipya kipekee halitegemei msamiati** uliotumiwa katika Maandiko: suala siyo kumwita mchungaji mkuu, askofu, mwangalizi, Mtembeleaji au kutokuwa na jina kabisa; bali ni kama taasisi hiyo yaweza kupatikana katika Maandiko. Kama ni hivyo, je, ni wajibu gani na mamlaka gani mtu huyo anapaswa kuyabeba?
   Mkristo mwenye cheo cha "Ndugu" anaweza kuwa dikteta, wakati mwingine mwenye cheo cha "Baba" au "Askofu" anaweza kuthibitisha kutokuwa na mamlaka kabisa wakati wa maamuzi, wakati ambapo uovu unapaswa kupingwa. Mtu asiye na mamlaka nyumbani [kwake] anaweza kuwa mkaidi katika matakwa yake ya wanawake kutii. Mwingine, anayeunga mkono haki za wanawake mbele ya hadhara, anaweza kuwa katili nyumbani [kwake].
2) Suala la mfumo sahihi wa utawala wa kanisa haliwezi kuamuliwa kwenye karatasi au kwa nadharia, bali katika uhalisia wa kila siku wa maisha ya kanisa. Hatupaswi kusahau kuwa nadharia na vitendo mara nyingi vinakinzana. Papa, ambaye mamlaka yake ya kinadharia ni makuu hapa duniani,[80] ana ushawishi mdogo katika makanisa mengi ya mitaa ya Kikatoliki [vigango]; lakini nina uzoefu wa mamlaka yasiyo na mipaka yafanywayo na wahariri wa moja ya makampuni ya uchapaji ya Udugu, mara nyingi ni kiongozi wa siri wa dhehebu lote. Ingawa dhehebu [lenyewe] hukataa rasmi kwa nguvu sana wazo lolote la aina yoyote ya uwezo au mamlaka nje ya kanisa la mtaa, makanisa yote

80 Tazama: Thomas Schirrmacher. „Has Roman Catholicism Changed? An Examination of Recent Canon Law". Antithesis: A Review of Reformed/Presbyterian Thought and Practice 1 (1990) 2 (März/Apr): 23-30. For the Roman Catholic position, see: Knut Walf. „Knut Walf. " „Kollegialität der Bischöfe ohne römischen Zentralismus? ". Diakonia: Internationale Zeitschrift für die Praxis der Kirche 17 (1986) 3: 167-179, here pp. 167-173; and Joseph Kommonchak. „Das ökumenische Konzil im neuen Kirchenrechtskodex". Concilium (German edition) 19 (1983) 8/9: 574-579.

katika dhehebu lile yalikubali amri yake kuwa Mkristo mgeni hakupaswa kuzungumza katika makanisa hayo.

3) Matumizi ya neno kama vile “kiepiskopo” ‘kipresbaiteria’ au ‘ukanisa–mtaa’ yanaushiriki mdogo katika uhalisia uliomo ndani ya kanisa au ndani ya dhehebu. Majengo ya baadhi ya makanisa ya kimtaa yako chini ya dhehebu, na yale ya baadhi ya makanisa ya kiepiskopo yako chini ya kanisa la mtaa. Katika muundo huu wa mwisho wa kiepiskopo, kanisa la mtaa linakuwa linalojitegemea zaidi kuliko yale ya mwanzo ya ukanisa–mtaa. Iwapo kanisa la kiepiskopo linachagua wachungaji wake (na iwapo dhehebu hili halina seminari yake lenyewe), linajitegemea zaidi kuliko kanisa la ukanisa–mtaa ambalo linaweza kuchagua tu wachungaji waliofundishwa katika seminari yake lenyewe.
   Utawala wa seminari, [ambao ni] watu wanaoamua ni mwanafunzi yupi anayeweza kusoma katika seminari ile, na wanaowatuma wahitimu wao kwenye makanisa, mara nyingi wana ushawishi zaidi kwenye dhehebu husika kuliko maaskofu. (Jukumu la mkurugenzi wa seminari kwa sehemu linalingana lile la maaskofu wa Kanisa la Kwanza).
4) Hata wakati ambapo muundo na yaliyomo hukubaliana, na hata kama miundo inayoonekana ya maisha ya kanisa ina umuhimu fulani, malengo ya kiroho yanapaswa kupewa kipaumbele cha kwanza. Mara zote tuko katika hatari ya kuangalia zaidi tofauti zinazoonekana kuliko zile zisizoonekana, lakini unyenyekevu wa kiroho wa kweli ni wenye umuhimu zaidi kuliko mipaka ya kimamlaka iliyo kwenye karatasi. Mtu mwenye kiburi hataharibu ofisi yoyote ile, lakini mtu mnyenyekevu kamwe hataitumia vibaya hata kama ni mamlaka yaliyozidishwa sana. Yeyote anayekusudia kutumia nguvu zake binafsi kanisani atafanya hivyo – kwa mamlaka au bila mamlaka ya katiba ya kanisa. Mtu ambaye kipaumbele chake cha kwanza ni mambo ya kiroho ya kanisa hatalidhuru kanisa, hata kama katiba itampa mamlaka yote.
5) **Agano la Kale na Jipya yote yanaweka mpaka wa mamlaka yaliyogawiwa kutokea chini hadi kwa mamlaka yanayogawiwa kutokea juu**. Ufupisho wa ufanyaji maamuzi[81] wa Agano Jipya unadhihirisha kuwa njia sahihi hutegemea mazingira; wakati mwingine mamlaka hufanya kazi kutokea juu, wakati mwingine kutokea chini.

---

81 Joost Reinke, Jürgen Tischler. Dynamisch leiten. Missiologica Evangelica 10. Verlag für Kultur und Wissenschaft: Bonn, 1998. pp. 68-70 in Anlehnung an Johannes Jansen. Gemeinde und Gemeindeführung: Episkopat, Presbyterium oder Demokratie? J. G. Oncken: Kassel, 1931. p. 49. Kwa ajili ya mtazamo kinzani, tazama: Jeff Brown. Gemeindeleitung nach dem Neuen Testament. VTR: Nürnberg, 2000. pp. 14-15.

Baadhi ya maamuzi hufanywa kwa makubaliano, baadhi hufanywa na mtu binafsi. Johannes Jansen anaandika:
"Si vielelezo vya uongozi ya kiepiskopo, kipresbaiteria wala ukanisa–mtaa huelewa kikamilifu upana wa katiba za makanisa ya mwanzo, kibinafsi au kwa ujumla wao. Tunapata utawala kwa njia ya watu binafsi wenye sifa stahili (uepiskopo wa mtawala mwenye nguvu), vilevile kwa njia ya ushirikiano kati ya wazee, makundi ya mitume, mtume mmoja na wazee wa Yerusalemu (upresbaiteria) na mamlaka yanayofanywa na kanisa la mtaa (kanisa la kidemokrasia). Hata hivyo, katika vielelezo [hivi] vyote, kila mmoja hunyenyekea kwa mwenzake, na kwa Kristo. Agano Jipya hutoa umoja wenye furaha wa uhuru na utii, kama mwunganisho wa kanuni zote tatu. Hakuna ofisi ya utume au uaskofu, wala mzee mwenye mamlaka yote, wala demokrasia kamilifu ya kanisa yenye maofisa waliochaguliwa."[82]

**Ufanyaji Maamuzi katika Agano Jipya**

| Kifungu | Tatizo | Washiriki | Hatua | Muundo |
|---|---|---|---|---|
| Matendo 1:15-26 | Upanuaji wa ofisi ya utume | Mitume 11 na Wanaume 120 (+Wanawake?) | Petro anaanzisha, wagombea wawili wanapendekezwa. Uchaguzi unafanywa kwa kupiga kura | Kidemokrasia, kanisa la mtaa |
| Matendo 5:2+6:1-2 | Hazina ya kanisa na utunzaji wa masikini | Mitume 12 | Ugawaji na Utawala unafanywa na mitume pekee | Kipresbaiteria, timu ya uongozi |
| Matendo 6:1-7 | Utunzaji wa masikini ni jambo zito zaidi kuliko Mitume 12 wanavyoweza kuhudumia. | Mitume 12, kanisa (>1000?), Wahudumu 7 | Uanzishaji: ushauri wa kitume, uchaguzi unaoambatana na kuthibitishwa | Kipresbaiteria, kidemokrasia |
| Matendo 10:48 | Kuokolewa - na ubatizo | Petro na ndugu wengine kadhaa kutoka Yafa | Petro anaamuru ubatizo | Kiepiskopo, kiimla |
| Matendo 14:23 | Uwekaji wakfu wa wazee | Paulo na Barnaba | wote walichaguliwa | takribani ni kiepis-kopo kabisa, lakini pia kipresbaiteria (kwa kuwa yote miwili ilihusishwa) |

82 Johannes Jansen. Gemeinde und Gemeindeführung. op. cit., p. 49. Katika uk. 3, anafupisha: mmoja huongoza, baraza la ndugu huongoza, wote huongoza.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Matendo 15:1-35 | Baraza la Mitume, Ushirika baina ya Wayahudi na Mataifa | Paulo, Barnaba, mitume na wazee, makanisa ya Antiokia na Yerusalemu | Kanisa na mkutano wa mwisho wa wazee na mitume – maamuzi ya kanisa | Kipesbaiteria, Kidemokrasia |
| Matendo 15:36-40 | Sifa stahili za Yohana Marko kwa ajili ya safari iliyopangwa ya kimishenari | Barnaba, Paulo (Kizuizi: Barnaba, yawezekana pia Sila) | Mabishano – kutengana. Kazi ya misheni inaendelea pamoja na kutengana. Upatanisho [ulifanyika] hapo baadaye | ? Kiepiskopo? (Maaskofu wawili katika hali ya kutopatana??) |
| Matendo 21:17-25 | Safari ya Paulo huko Yerusalemu. Tetesi kuwa Paulo anapingana na sheria za Kiyahudi | Paulo, Yakobo, wazee wa kanisa huko Yerusalemu | Mkutano wa wazee unaongoza kwenye maamuzi, ambayo yanafanywa na kanisa | Kipresbaiteria |
| 1 Kor. 14:26 k | Maelekezo ya muundo wa ibada | Paulo na kanisa la Korintho | Maelekezo yaliyoandikwa | Kiepiskopo |
| 2 Kor. 13:2-4,10 | Dhambi ndani ya kanisa | Paulo na kanisa la Korintho | "**msimhurumie mwenye dhambi**" Paulo anatumia mamlaka yake | Kiepiskopo |

6) **Agano la Kale na Jipya, yote huweka mpaka wa mamlaka ya uongozi kufanya maamuzi na [mpaka wa] mamlaka ya kundi**. Robert Woodward Barnwell huonesha kuwa Agano Jipya huthamini katika hali sawa mamlaka ya mtu mmoja mmoja na yale ya wengi.[83] Kwa usahihi husema, upapa umekuza mamlaka kwa kiasi kikubwa hata maamuzi ya wengi yakafa, wakati mfumo wa kanisa–mtaa ulisisitiza sana maamuzi ya wengi, kiasi kwamba mamlaka yakafa.[84] Kwa hiyo, mabaraza ya Sinodi ni muhimu, lakini hayajaonesha utendaji, juhudi na umuhimu wa kuthubutu kwa kuukuza Ufalme wa Mungu. Wamishenari wakuu na wajenzi wakuu wa makanisa daima wamekuwa ni watu binafsi. Monte E. Wilson aandika:[85]

[83] Robert Woodward Barnwell. *The Analysis of Church Government.* The Franklin Press Company Publ.: Petersburg (VA), 1907. pp. 250+269+279.

[84] *Ibid.,* p. 252.

Katika Biblia tunaweza kupata aina hizo zote zilizotajwa hapo juu za mifumo ya uongozi wa kanisa. Kila mfumo una historia iliyotukuka. Pia kila mmoja una udhaifu wake unaowezekana. Ukanisa–mtaa kudorora hata kugeuka kuwa demokrasia ambapo twapigia kura mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa, na kila mmoja hufanya kile anachoona ni sawa machoni pake mwenyewe; kama inavyojulikana, utawala huria. Upresbaiteria unaweza kujifinyanga kuwa tabaka la watawala [jamii] bora lililojitenga na lisilojali mahitaji ya kiroho ya kanisa la mtaa. Uepiskopo unaweza kuongoza kwenye udikteta ambao umetenganishwa kabisa na kanisa la mtaa ambalo [uepiskopo] hudai kuliongoza.[85]

*Kitovuni mwa mfumo wa kanisa wa kibiblia zipo ofisi za mhudumu na mzee, wanaohitaji kupewa mamlaka na ushirika wa waamini. Wahudumu wanahusika kwa mahitaji ya kimwili na kijamii ya kikanisa; wazee ambao hutawala kanisa, wanahusika kwa mafundisho na uongozi wa kiroho. Kando ya mifumo hii ndani ya makanisa husika, makanisa ya Agano Jipya yalidhihirisha hali ya kuhusika kiroho kila moja kwa jingine, jambo lililomaanisha ushirikiano uvukao mipaka ya kikanda na usaidizi wa pamoja.*

Mimi binafsi, ninaona mwunganiko wa mambo yaliyomo katika [mifumo] vielelezo [hivyo] vitatu kuwa suluhisho la tatizo. Kimsingi Biblia haimaanishi mwunganiko wa mambo yaliyomo katika ukanisa–mtaa, upresbaiteria na uepiskopo, na kwa kweli, kunaweza kuwa na njia nyingine za kukabiliana na suala hili. Mambo muhimu kwa ajili ya suluhisho ni pamoja na 1. Kanisa la mtaa linalojitegemea kwa kiasi fulani na lililo imara, ambalo wazee wake wa kanisa wana mamlaka na pia [wana] uwajibikaji. 2. [mabaraza ya] sinodi ambamo ndani yake watumishi wa muda wote, wazee wa kanisa na makanisa, wote hukosoana na huhamasishana wenyewe kwa wenyewe, na 3. viongozi wenye madaraka kuliko ya kikanda, watu walio vielelezo vya kiroho ambao huangalia maendeleo ya jumla na hushughulikia misheni, lakini hawana mamlaka ya kisakramenti au ya kisheria.

7) Mamlaka, ama yawe yanatokea juu au chini, hatimaye lazima yawe chini ya Neno la Mungu – si ofisi wala katiba yenye neno [mamlaka ya] la mwisho, bali ni Maandiko. Mamlaka huwa kwa mtu ambaye mamlaka yake huchotwa kutoka katika Biblia na kwa Roho Mtakatifu. Wakati Paulo anawaacha wazee wa kanisa wa Efeso, hakuwaachia sheria za kanisa wala ofisi. Bali aliwasihi tu, “Basi, sasa nawaweka

[85] Monte E. Wilson. „Church Government: The Problem of Tyranny and Anarchy within the Local Church.” Chalcedon Report Nr. 416 (March 2000), pp. 18-19, hapa ni uk. 18.

katika mikono ya Mungu, na kwa neno la neema yake, ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa” (Matendo 20:32). Kanisa liko kwa ajili ya hilo. Kanisa lishindwapo katika majukumu yake ya kimishenari, huhitaji viongozi waliojaliwa vipawa vya kiroho, wanaojitegemea na wenye ujasiri wa kusihi na kuliita tena kwenye majukumu yake, kama manabii wa Agano la Kale walivyofanya. Hawakuwajali makuhani wa Kilawi, wakati maofisa hawa walipotupilia mbali majukumu yao au walipozitumia vibaya nafasi zao. Kwa upande mwingine, viongozi katika kanisa lao la mtaa mahali pao hapana budi kuchukuliwa na wengine pindi wanapotumia vibaya mamlaka yao au wanapoweka urasimu mahali pa mtazamo ya kimishenari. Katika hali kama hiyo, ushirika, basi kadri unavyosukumwa na Neno la Mungu na Roho Mtakatifu, unaitwa [unatakiwa] kuushutumu uongozi.

Hakuna katiba au muundo, hata viwe bora kwa kiwango gani, visivyoweza kukosea. Hata kama umetoa ushirikiano na makubaliano ya mipaka yake kutoka juu na chini, utawala wa kanisa waweza kukosea, wakati unapofuata mafundisho ya yasiyo ya kibiblia au viongozi wasio wa kiroho. Mungu husimama kwa Neno lake na kwa kazi ya Roho wake. Katika mgogoro wowote, atawasaidia wale wanaoelekeza kwa kufuata Neno lake au pasipo haki ya kisheria ya katiba au desturi ya kanisa, kama alivyofanya kwa manabii wa Agano la Kale. Kwa sababu Maandiko yalikuwa upande wao, Paulo (na Barnaba) walikuwa sawa katika kuthubutu kumkemea hata Petro (“nalishindana naye uso kwa uso,” Gal. 2:11-14+18) kwa kuisaliti injili (“**… Hawakwenda sawasawa na kweli ya Injili,**” Gal. 2:14).

Baadaye Paulo anaandika kwa mtindo ule ule wakati awakemeapo Wakorintho kuhusu mabishano yao juu ya mafundisho. “Basi ndugu, mambo hayo nimeyafanya kuwa mfano wa mimi na Apolo kwa ajili yenu, ili kwamba kwa mfano wetu mpate kujifunza kutokupita yale yaliyoandikwa; ili mmoja wenu asijivune kwa ajili ya huyu, kinyume cha mwenziwe.” (1 Kor. 4:6). Yeyote aendaye kupita Maandiko anafanya ubatili na analihatarisha kanisa, iwe ameidhinishwa na katiba ya kanisa lake au la.

Kama ambavyo Serikali ni lazima iwe chini ya Sheria (katiba)[86] na siyo chini ya mtu yeyote, kanisa la Agano Jipya halimtambui mtu yeyote, ama awe katika mtaa au katika ngazi inayovuka kanda asiye chini ya Biblia. Maandiko ndiyo katiba pekee iliyotolewa kwa mwili wa Kristo,

[86] Tazama: Thomas Schirrmacher. Ethik. Vol 2, Lektion 59 and 60, op. cit.

hata kama madhehebu na makanisa ya mtaa yataona ni suala la kivitendo kuunda taratibu halisi au matamko ya imani.

8) Wachungaji wanahitaji washauri na wanasihi. Waangalizi, maaskofu n.k. wako juu ya wachungaji na washauri wa wachungaji wote (Kilatini: pastor pastorum), sio juu ya wakuu wa kiutawala au maofisa. Wachungaji wanahitaji kutiwa moyo na kupata nasaha kwa kadri ile ile sawa na Wakristo wengine, lakini wanasihi hawa hawapaswi kuwa washiriki wa kanisa la mchungaji mwenyewe. Katika Agano Jipya, kosa la mchungaji mmoja halikulihusu kanisa lake tu bali pia makanisa mengine. Hata hivyo, wakati mchungaji au mzee wa kanisa alipokuwa kwenye magumu, kwanza alifuatwa na mtu, siyo na Sinodi, kamati au mahakama [baraza la maamuzi] ya kanisa sawasawa na ilivyo kwa suala la mwumini wa kanisa atendaye dhambi katika Mathayo 18:15.[87]

   Katika makanisa ya kiepiskopo, ofisi huendeshwa na "Uaskofu wa Kisinodi" ambamo askofu huchaguliwa na Sinodi kama mwangalizi, na hivyo huwa chini ya Sinodi. Katika makanisa mengine, rais wa sinodi, mhudumu au mwangalizi hufanya majukumu haya. Ofisa huyu ni lazima awe na angalau mamlaka ya kuitaka sinodi kufikiria tena juu ya maamuzi yaliyokosewa, lakini sinodi lazima iwe na nguvu ya kumwita mwangalizi katika uwajibikaji, kumwondoa au kurekebisha mipaka ya mamlaka yake.

   Marie M. Fortune husisitiza kuwa wazee wa kanisa wa mfumo wa ukanisa–mtaa wana mamlaka ya kuingilia kati, wakati wachungaji wanapotumia vibaya ofisi zao. Analaumu ukosefu wa mipaka hiyo kwa masuala yanayojirudiarudia ya wachungaji wanaoendekeza mahusiano ya kingono na wanawake wanaotafuta msaada wa ushauri.[88]

9) Kanisa halina budi kuwa na washauri wa kutosha kutoa mwongozo wa kutosha ulio wa binafsi na wa kiroho. Haya yanapaswa kuwa hai katika kanisa la mtaa pia. Hakuna mtu anayeweza kuwafahamu vema kiasi cha kutosha wachungaji 50 na wazee 300 wa kanisa vema (kwa mfano) ili kutoa 'uangalizi wa kiroho' wa kiroho wanaouhitaji.

   Makanisa machache ya kiepiskopo yana maaskofu wa kutosha [wanaoweza] kutambua yote yanayoendelea katika makanisa ya mtaa. Isipokuwa kwa kazi ya kivitendo za kiutawala na mambo ya kitaasisi, kama vile kuitisha sinodi, n.k., kanisa halihitaji ngazi ya juu zaidi ya maaskofu. Makanisa ya kiepiskopo yanahitaji kujifunza kutoka kwa Kanisa la Kwanza, ambalo lilikuwa na maaskofu 1. kama 'wachungaji'

---

87 Ibid., Lektion 57.

88 Marie M. Fortune. Is Nothing Sacred? When Sex Invades the Pastoral Relationship. Harper & Row: San Francisco, 1989. p. 98.

wa maeneo madogo na 2. kama mmoja wa watumishi–wenza, waliosaidiana na kutiana moyo kila mtu na mwenzake.

Kwa kuhitimisha, ningependa kumnukuu Monte E. Wilson. Baada ya kujadili mifumo mitatu ya msingi ya uongozi wa kanisa, anaandika:[89]

Katika Biblia tunaweza kupata aina hizo zote zilizotajwa hapo juu za mifumo ya uongozi wa kanisa. Kila mfumo una historia iliyotukuka. Pia kila mmoja una udhaifu wake unaowezekana. Ukanisa–mtaa kudorora hata kugeuka kuwa demokrasia ambapo twapigia kura mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa, na kila mmoja hufanya kile anachoona ni sawa machoni pake mwenyewe; kama inavyojulikana, utawala huria. Upresbaiteria unaweza kujifinyanga kuwa tabaka la watawala [jamii] bora lililojitenga na lisilojali mahitaji ya kiroho ya kanisa la mtaa. Uepiskopo unaweza kuongoza kwenye udikteta ambao umetenganishwa kabisa na kanisa la mtaa ambalo [uepiskopo] hudai kuliongoza.

Kwa sababu ya matumizi ya neno, *'mtume'*, katika Agano Jipya, ninadhani kuwa kulikuwa na mitume waanzilishi, kama vile Petro au Paulo *("Mitume wa Yesu Kristo")*, ambao Mungu alikuwa amewathibitisha kwa ishara na miujiza, na ambao maelekezo yao yalikuwa kifungo kikamilifu [mambo ya kutekelezwa] kwa makanisa yote. Ofisi hii haipo tena, lakini karama ya kiroho na ofisi ya mtume kwa maana ya jumla bado inafanya kazi ("*mitume [au wajumbe wa makanisa"]*, 2 Kor. 8:23, Flp. 2:25)[90]. Mitume hawa walikuwa na bado ni wamishenari wenye karama ya kipekee ya kuanzisha makanisa mahali ambapo hapo kabla hayakuwepo na mahali ambapo hakuna waamini. Kwanza, wanafunzi kumi na wawili wa Yesu wanaitwa mitume. Baadaye, Mathayo, mbadala wa Yuda, na Paulo anaongezwa. Wote hawa walimwona Yesu (Paulo katika maono), waliteuliwa na Yeye, alithibitisha mamlaka yao ya kitume kwa ishara na miujiza na aliwasaidia katika ufunuo na kuhifadhi kumbukumbu za ujumbe wa Agano Jipya.

Mara kadhaa, watumishi wengine katika makanisa ya Agano Jipya huitwa mitume, kwa majina ni nduguze Yesu, yaani Yakobo na Yuda (1 Kor. 9:5, 15:7, Gal. 1:19) na yawezekana Barnaba (Matendo 14:4, 14) na wengine (1 Kor. 15:7, yawezekana Matendo ya Mitume 1:25). Kumhusu

---

[89] Monte E. Wilson. „Church Government: The Problems of Tyranny and Anarchy within the Local Church". Chalcedon Report Nr. 416 (March 2000): 18-19, hapa ni kr. 18-19. Makala yote ni bora kabisa.

[90] Tazama orodha yangu na majadiliano yangu ya vifungu vyote vya Agano Jipya vinavyozungumzia mitume katika Thomas Schirrmacher, Ethik, vol. 2, op. cit., pp. 542-546 na Thomas Schirrmacher, *Der Römerbrief,* vol. 2, op. cit., pp. 292-296.

Barnaba, neno [mtume] linaweza kuwa lilitumiwa kwa maana ya jumla, kama ilivyo katika 2 Kor. 8:23. Paulo, anapozungumza hapa kuhusu 'mitume' au 'wajumbe' wa makanisa, huwarejea watumishi–wenza ambao amewatuma kama wamishenari (neno, "mmishenari" likiwa ni tafsiri ya Kilatini ya neno la Kigiriki 'mtume' au 'mjumbe'), mwenye majukumu ya kiutawala juu ya makanisa kadhaa. Siyo *'mitume wa Yesu Kristo'* kwa maana finyu ya neno, bali hulingana na wamishenari wa sasa wanaojihusisha na uanzishaji wa makanisa mapya, au maaskofu wamishenari.

Kama ilivyo muhimu kwa wajibu wa jumla wa mmishenari ulivyo, jua kwamba ni mitume waanzilishi tu waliomaanishwa, wakati wowote Maandiko yanapozungumzia maneno au amri za mitume, msingi wa Kanisa la Agano Jipya au ya ufunuo wa neno la Mungu.

Kwa hiyo, inaonekana wazi, kuwa ofisi ya mitume waanzilishi ilikuwepo tu kwenye kizazi cha wakati [wa maisha ya Yesu] na muda mfupi baada ya maisha ya Yesu duniani. Hata hivyo, katika karne ya pili[91] bado kulikuwa na 'mitume' kwa maana iliyotumiwa katika 2 Kor. 8:23, kama ambavyo wapo sasa, ingawa, ili kukwepa mkanganyiko, mtu hana budi kuwaita wamishenari au maaskofu.

---

91 Tazama Adolf von Harnack, *Die Mission und Ausbreitung des Christentums in den ersten drei Jahrhunderten,* VMA-Verlag: Wiesbaden, o. J. (reprint from 1924[4]), pp. 361. Kwa mujibu wa Einar Molland, „Besaß die Alte Kirche ein Missionsprogramm?",.pp. 51-76 katika: Heinzgünther Frohnes, Uwe W. Knorr (ed.), Die Alte Kirche, Kirchengeschichte als Missionsgeschichte 1, Chr. Kaiser: München, 1974, p. 57 wamishenari waliitwa 'mitume' wakati wa Zama za Kati.

## Paulo na Watumishi Wenzake: Jinsi 'Wamishenari wa Agano Jipya' Hufanya Kazi Pamoja

*Mhadhara kwa ajili ya mkutano wa mwaka 1997 wa Arbeitskreis für evangelikale Missiologie e.V. ( Muungano wa Wanazuoni wa Umisheni wa Kiinjili wa Ujerumani – Ushirikiano wa Kiinjili wa Ujerumani)*

## Kujifunza kutoka kwa Paulo

Wolf-Henning Ollrog wakati mmoja alionesha kwa namna inayofaa kuwa tafiti mbalimbali zimekwishafanyika juu ya wapinzani wa Paulo, lakini ni utafiti chache sana zilizookwishafanywa juu ya marafiki zake na watumishi wenzake.[92] Jambo la kushangaza, kwa kuwa si [kitabu cha] Matendo ya Mitume tu, bali pia nyaraka za Paulo hutupatia taarifa nyingi za marafiki wa karibu na wafanyakazi wenza wa mtume; nyaraka za kichungaji hujikita katika mada hii!

Katika vikundi vyetu vya kujifunza Biblia vya sasa, hatuwezi kukusanya kwa mpangilio taarifa zote juu ya mahusiano ya Paulo kwa marafiki zake na kwa makanisa, hata kama jitihada hizo zingekuwa bora namna gani. Wala hatuwezi kuweka katalogi ya sheria isiyokuwa na makosa kwa bodi za misheni na kwa wamishenari [ili] kuzibeba mifukoni mwao. Badala yake, tunaweza kuchunguza tu mazingira machache yaliyochaguliwa ya Agano Jipya ambayo yanaonesha pembetatu ya:

[92] Wolf-Hennig Ollrog. *Paulus und seine Mitarbeiter: Untersuchungen zu Theorie und Praxis der paulinischen Mission.* Wissenschaftliche Monographien zum Alten Testament 50 (Neukirchen, Germany: Neukirchener Verlag, 1979) p. 3. Akianza na data za kihistoria katika Agano Jipya juu ya watendakazi wenzake Paulo, na utafiti wa neno juu ya istilahi 'synergos', Ollrog huwagawa watendakazi wenza wa Paulo katika makundi matatu: watendakazi wenza wa mtume wa karibu zaidi, ambao huambatana naye muda wote; watendakazi wenza walio huru, ambao humsaidia katika hali mahususi 'zisizotarajiwa'; na wawakilishi wa makanisa, waliotumwa na makanisa yao ili kushiriki katika kuongeza jitihada za kimishenari. Kundi hili la mwisho lilifanya urafiki wa karibu zaidi na kanisa, wamishenari na eneo la umishenari. Cha kusikitisha, kitabu cha Ollrog si kamili, kwa kuwa anadhani kuwa 2 Thes., Efe., Kol., na nyaraka za kichungaji si za Paulo (uk. 1) na hivyo anatupilia mbali kiwango kikubwa cha taarifa. Maswali mengi ambayo huyaacha bila kutatuliwa yangeweza kujibiwa, kama uhakiki–kinzani mkali namna hiyo ungeacha kukiwekea mipaka kiwango [hicho] cha taarifa zenye kuaminika. [Kitabu cha] Matendo nacho kinashugulikiwa kwa mtindo huu: Kitabu kinachukuliwa kuwa ni cha Luka, lakini hakitiliwi maanani – mwandishi anashawishika kwamba Luka alighushi data zake.

mtume – watendakazi wenza – kanisa, ili kujua kile yanachotuambia juu ya Paulo na uhusiano wake na watumishi wenzake. Swali letu litakuwa, "Ni hekima gani tunayoweza kuipata katika kushughulika kwetu kila mtu na mwenzake?"

Kwa sababu mahusiano ya wanadamu yanatofautiana sana, yanabadilika na ni tata kuweza kurahisishwa kuwa ya asili moja, Maandiko hayajaribu kuyabadilisha kwa sheria kamilifu, lakini hupendekeza mwitikio wa busara[93] upatikanao kwa kupitia uzoefu, mifano na uchanganuzi makini wa hali [halisi]. Mhubiri 10:8 ("Mwenye kuchimba shimo atatumbukia ndani yake. Na yeye abomoaye boma, nyoka atamwuma.") ni ushauri wenye busara juu ya uhusiano miongoni mwa watu, lakini si sheria wala si ya moja kwa moja. Kitabu cha Agano la Kale cha Mithali, ni kitabu cha kusoma kwa ajili ya uhusiano binafsi, ingawa kinatoa sheria na taratibu. Kwa hakika, baadhi ya mithali hata huonekana kupingana zenyewe.

Mfano bora wa jambo hili ni Mithali 26:4, "Usimjibu mpumbavu sawasawa na upumbavu wake; usije ukafanana naye. Umjibu mpumbavu sawasawa na upumbavu wake; asije akawa mwenye hekima machoni mwake." Je, tuwajibu wapumbavu au la? Kuna sehemu mbili kwa swali hili, na majibu yetu yanategemea hali [halisi] – Biblia haitupi sheria kamilifu katika jambo hili. Mtu mwenye busara hupaswa kuamua kupitia hali halisi na mtu halisi, ni aina gani ya jibu litaleta matokeo bora.

Tunapata mfano mwingine zaidi wa kanuni ya hekima ambayo hupaswa kutumika tu kwenye hali halisi fulani katika vifungu viwili ambavyo vinatumia ukweli kwamba watu huichoka hata asali (Chokoleti waweza kuwa mfano ufaao katika utamaduni wetu) katika kuelezea hoja. Mithali 25:16-17 hutuambia, "**Je, umepata asali? Kula kiasi kinachokutosha, usije ukavimbiwa, na kuitapika. Ondoa mguu wako kutoka katika nyumba ya jirani yako, asije akakuchoka, na hivyo kukuchukia.**" Hata hivyo, Mithali 25:27 hutukumbusha kwamba, "**Si jambo jema kula asali nyingi: vivyo hivyo *kwa watu* kutafuta utukufu wao wenyewe *si* utukufu.**" Rejea ya asali hutupatia kanuni ya jumla ambayo huweza kutusaidia kuepuka kero za pande zote mbili. Mwalimu wa Hekima kwa urahisi hana kanuni kamilifu kwa ajili ya kiwango cha

[93] Thomas Schirrmacher. *Ethik* (Neuhausen, Germany: Hänssler Verlag, 1994) Vol. 1, pp. 492-503. „Kando na sheria halali kabisa na zinazotumika moja kwa moja, tunaona 'hekima', ambayo maamuzi yake hutegemea mazingira na maarifa ya watu wanaohusika. Hekima yaweza tu kuelezwa katika methali, hadithi-fumbo, mifano na vielezo, na hujumuisha uzoefu, ambao ni wa kweli tu katika mazingira fulani." (tazama Mith. 15:2; 22:6)" pp 492-493.

kukutana au cha kusifu tunachotaka kutoka kwa marafiki zetu. Maamuzi hayo huhitaji uzoefu, pia ufahamu wa marafiki binafsi; kumtembelea au kumsifu rafiki mwema mara kwa mara siyo dhambi, bali si busara.

Kwa kuwa Kitabu cha Mithali ni muhtasari wa mafundisho ya hekima, ningependa kutumia mithali ifaayo kwenye mitazamo mbalimbali ya shughuli ya kimishenari ya Paulo.

## Tukio la 1: Paulo anampa Tito umuhimu wa kwanza

(Paulo, Tito, Kanisa la Korintho)

> "Pasipo mashauri makusudi hubatilika; bali kwa wingi wa washauri huthibitika" (Mithali 15:22[94]).

Mahusiano ya Paulo kwa kanisa alilokwisha kulianzisha huko Korintho yalikuwa yanaharibika,[95] kwa kuwa sehemu ya kanisa ilichukua mwelekeo mpya kabisa ambao ulikuwa unaongoza kwenye matokeo angamivu. Baadhi ya waumini katika kanisa walikuwa wanashiriki katika ibada ya sanamu, kutembelea makahaba, kutelekeza ndoa zao na kutowajali watu wenye njaa wakati wa Ushirika [Meza ya Bwana]: na haya yote [yalifanyika] katika jina la Mungu,[96] lakini bado uongozi wa kanisa ulikataa kuiadhibu tabia hii, [hii ni] kejeli ya wazo halisi la maisha ya Kikristo. Katika kujibu, Paulo aliandika maneno makali kuliko kwenye nyaraka zake nyingine zote, isipokuwa Wagalatia. Wakati si nyaraka zake za wazi (moja iliyopotea; 1 Wakorintho 5:9-11 na 1 Wakorintho) wala safari zake zilizoleta maendeleo yoyote, mtume alikuwa kwenye hali ya kukata tamaa, amejaa hofu na machozi (2 Kor. 2:4) na hakuona sababu ya kuwa na safari nyingine zaidi ( 2 Kor. 2:1). Je, Paulo alifanya nini, kama mtume na mwangalizi wa injili? Kulitenga kanisa? Kudhani kwamba Wakorintho walikuwa wametia muhuri hatima yao wenyewe kwa kumkataa Paulo? Kukata tamaa?

Hapana, katikati ya kukata tamaa kwake na maumivu, alionesha ukuu wake wa kweli: akiwa hawezi kabisa kuendelea bila msaada, badala ya kusisitiza katika kutatua tatizo mwenyewe, alimwita Tito, yawezekana

---

94 Tazama pia Mithali 11:4; 20:18; 24:6.

95 Heinz Warnecke, Thomas Schirrmacher. „Plädoyer für die historische Glaubwürdigkeit der Apstelgeschichte und der Pastoralbriefe", in *War Paulus wirklich auf Malta?* (Neuhausen, Germany: Hänssler Verlag, 1992). pp. 181-235.

96 Thomas Schirrmacher. *Paulus im Kampf gegen den Schleier: Eine alternative Sichte von 1. Kor 11:2-16*. Biblia et symbiotica 4 (Bonn, Germany: Verlag für Kultur und Wissenschaft, 1993) pp. 111-152.

kutoka Krete.[97] "Kwa maana hata tulipokuwa tumefika Makedonia miili yetu haikupata nafuu; bali tulidhikika kote kote; nje *palikuwa* na vita, ndani [***palikuwa na***] hofu. Lakini Mungu, mwenye kuwafariji wanyonge, alitufariji kwa kuja kwake Tito" (2 Kor. 7:5-6).

Mtumishi mwenza huyu, ambaye ujio wake ulimfariji sana Paulo, sasa alitumwa kwenda Korintho akiwa na barua mpya, ijulikanayo kama "Barua ya machozi" (baada ya 2 Kor. 2:4), iliyoandikwa katikati ya 1 Wakorintho na 2 Wakorintho. Paulo alifurahi sana pale Tito alipoweza kufaulu mahali Paulo aliposhindwa (2 Kor. 2:5-13; 7:5-16).

Mtume kwa dhahiri aliona juu ya uwezekano kuwa mtu mwingine mwenye haiba nyingine, mwenye karama tofauti na mwenye uhusiano mwingine na kanisa angeweza kufaa zaidi kufikia malengo yaliyo muhimu. Akiacha umuhimu wa kwanza na mafanikio kwa mwanafunzi wake, alitegemea kuwa uhusiano ulioingia dosari kati yake na Wakorintho ulikuwa unazuia upatanisho, na hivyo mpatanishi asiye na upande angeweza kuibadili hali. Uwezekano wa kupoteza taswira haukuwa muhimu kwake, kwa kuwa yeye mwenyewe alihusianisha kukata tamaa kwake, machozi yake na ukosefu wake wa uwezo. Kurekebisha hali kwake ni muhimu zaidi kuliko kuokoa heshima yake mwenyewe. Alikuwa akiwajali wengine, sio juu yake mwenyewe.

Paulo mwenyewe anajielezea jinsi alivyo dhaifu na mwenye msongo, asiyeweza kufanya kazi pamoja na milango [fursa] iliyo wazi, alibakia hadi Tito aliporudi kutoka Korintho, "**Zaidi sana, wakati tulipofika Troa *kuhubiri* injili ya Kristo, na Bwana aliponifungulia mlango, sikuwa na pumziko rohoni mwangu, kwa sababu sikumkuta Tito ndugu yangu: lakini nikiagana nao, kutoka huko nilikwenda Makedonia**" (2 Kor. 2:12-13).

Twaweza kujifunza nini kutokana na tukio hili?

*Paulo angeweza kufanya kazi katika timu*. Hakuweza kufanya kazi vizuri akiwa peke yake; uwepo wa wafanyakazi wenza ulimfariji na kumtia moyo. Luka hutuambia kwamba alifika huko Korintho akiwa peke yake, lakini aliwaomba washirika–wenza wake kuja upesi kadri inavyowezekana (Matendo 17:15). Ni mpaka walipofika ndipo alipoanza safari yake halisi ya kimishenari. "**Na wakati Sila na Timotheo walipokuja kutoka Makedonia, Paulo alisukumwa rohoni mwake, na kushuhudia kwa Wayahudi *kuwa* Yesu *alikuwa* Kristo**" (Matendo 18:5).

Na hata baada ya maono ya Paulo ya wito kwenda Makedonia (Matendo 16:9, "Na maono yakamtokea Paulo wakati wa usiku; Kulikuwa

---

97 Heinz Warnecke, Thomas Schirrmacher. *War Paulus wirklich auf Malta?* op. cit.

na mtu wa Makedonia kasimama, na kumwomba, akisema, Vuka uje Makedonia, na utusaidie.”), aliwasiliana na wengine kabla ya kufanya maamuzi. Ni mpaka kundi lilipothibitisha wazo [hilo], ndipo alipoondoka (Matendo 16:10). Na hilo ni baada ya maono!

*Paulo hakujiona mwenyewe kama mmishenari mkuu na asiyeingilika* ambaye alitatua matatizo yote bila upendeleo. Badala ya kujitengenezea ukumbusho wake mwenyewe, aliongea waziwazi hisia zake mwenyewe, kama vile hofu au huzuni, au vikwazo vyake mwenyewe kwenye kazi yake, na upungufu wake wa ujasiri katika kuihubiri Injili, jambo linalosababisha kuyaomba makanisa kumwombea, “**Mkiomba daima kwa maombi yote na dua katika Roho, na mkiwa macho kwa uvumilivu wote na dua kwa ajili ya watakatifu wote; Na kwa ajili yangu, kwamba niweze kupewa usemi, kwamba niweze kufungua kinywa changu kwa ujasiri, kufanya siri ya injili ijulikane, ambayo kwayo mimi ni mwakilishi katika vifungo: kwamba katika hilo niweze kunena kwa ujasiri, kama ambavyo nimekuwa nikinena**” (Waefeso 6:18; tazama pia Kol. 4:3; 2 Thes. 3:1; Matendo 28:31).

Badala ya kujisifia uwezo wake, uvumilivu wake au mafanikio yake, alikiri kwa Wakorintho, “**Ikiwa ni lazima nihitaji utukufu, nitajitukuza kwa mambo yanayohusu udhaifu wangu**” (2 Wakorintho 11:30; tazama pia 12:5-9).

*Kwa Paulo, matatizo hayakuwa tu masuala ya kina ya kiroho au kitheolojia, bali kwa usawa ule ule masuala muhimu ya mahusiano binafsi, ambayo yalimhusu mtu kwa ukamilifu wake, ikijumuisha hisia zake.* Ndio maana si ajabu mara nyingi huzungumzia machozi yake (2 Kor. 2:4, Flm. 3:18; Mdo. 20:19+31; 2 Tim. 1:4-5).

Hata hivyo, pia ni jambo la kushangaza, *kuwa maamuzi mengi muhimu yalikuwa yakifanywa moja kwa moja kwenye uwanja wa kazi ya umishenari, sio na bodi ya kimishenari iliyoko mbali.* Wamishenari walikuwa wamishenari waelekezi. Kanuni zote [hizi] zilitunzwa hadi kwenye karne ya kwanza, lakini baadaye zikasahaulika. Ni mpaka misheni za imani za awali kama vile China–Inland Mission (OMF) na WEC za karne ya mwisho, ndipo kanuni hizi zilipohuishwa tena. Paulo hakuyauliza makanisa–shirika mapya ya nyumbani juu ya kumbukumbu za mteuliwa (Matendo 16:1-3), na aliyatarajia kusaidia wamishenari wao kupitia maombi, fedha na uwekaji wakfu, lakini maamuzi ya kimsingi yalifanywa kule ambako matatizo yaliibuka. Kisha makanisa yalifahamishwa, lakini hayakuingilia.

## Tukio la 2: Usia kwa Mtume

(Paulo na Kanisa la Rumi)

> “**Yeye achukiaye maonyo ni mpumbavu**” (Mithali 12:1) ... “**lakini yeye asikiaye ushauri ni mwenye hekima**” (Mithali 12:15).

Baada ya kumaliza makusanyo ya matoleo kwa ajili ya kanisa huko Yerusalemu (Warumi 15:26-28), Paulo alikusudia kusafiri kutoka Korintho[98] kupitia njia ya Yerusalemu na Rumi hadi Uhispania (Warumi 15:27-31), akiutumia Rumi kama kituo chake kikuu – au kanisa la nyumbani, twaweza kusema – badala ya Antiokia. Ili kutoa taarifa kwa ajili ya shughuli yake ya kimishenari na kushirikishana malengo yake na Wakristo wa Rumi, mnamo mwaka 57 B.K.[99] hivi aliandika waraka wake mkubwa kwa Warumi, uchanganuzi pangilivu wa Biblia ulio bora, wa Injili na uhalalisho wake wa kina zaidi wa umisheni wa kiulimwengu.[100]

---

98 Paulo anaishi nyumbani kwa Gayo (Rum. 16:23), aliye Mkorintho (1 Kor. 1:14), na anamsifu Foibe [Fibi] wa Kenkrea, [ambayo ni] bandari ya Korintho (Rum. 16:1). Inawezekana mama huyu alikuwa amewasilisha barua Rumi, kwa kuwa ni mtu wa kwanza anayetajwa katika orodha ya salamu ya Paulo katika Warumi 16, na kwa kuwa Paulo anapendekeza kuwa kanisa limpokee vema. Hivyo ni vema kimantiki kufikiri kuwa Paulo aliusoma waraka kwa Tito, katibu wake (Rum. 16:22) huko Korintho au Kenkrea, na kisha alimpa Foibe kuuwasilisha. Adolf Schlatter anaonesha wazi usambamba mwingi kati ya Warumi na Nyaraka kwa Wakorintho, na anahitimisha kuwa Waraka kwa Warumi ni lazima uwe umeandika dhidi usuli wa migogoro na Kanisa la Korintho. tazama: Adolf Schlatter. *Gottes Gerechtigkeit: Ein Kommentar zum Römerbrief* (Stuttgart: Germany: Calwer Verlag, 1975[5]) pp. 9-16.

99 Paulo haamui kutembelea Makedonia na Akaya, au kwenda Rumi akitokea Yerusalemu hadi [kwenye] Matendo 19:21. Katika Matendo 20:2, anasafiri akipitia Makedonia na Akaya, yawezekana akikusanya matoleo kwa ajili ya waamini huko Yerusalemu, jambo linalokubaliana na Warumi 15:26. Inawezekana aliandika barua mapema kabla ya safari huko Yerusalemu [na] kwa miezi mitatu huko Ugiriki jambo analolitaja katika Matendo 20:3. Katika mazingira haya, barua yawezekana kuandikwa mnamo mwaka 57 B.K.

100 Tazama: Thomas Schirrmacher. „Romans as a Charter of World Missions: A Lesson in the Relation of Systematic Theology and Missiology” An International Journal of Frontier Missions 10 (1993) 4 (Oct): 159-162. au katika Reflection: An International Reformed Review of Missiology 4 (1993/94) 1/2 (Sept.-Nov): 34-39: in Chalcedon Report No. 342 (Jan 1994): 43-47. Kwa majadiliano ya kina, tazama: Thomas Schirrmacher. *Der Römerbrief*, „ 2 Vols. (Nehuhausen, Germany: Hänssler Verlag, 1994), komentari juu ya Warumi kutokea mtazamo wa elimu ya misheni na udogmatiki.

Ingawa yeye binafsi hakulijua kanisa la Rumi, aliwaombea daima (Rum. 1:9-10) na alitamani kukutana nao (Rum. 1:10+13; 15:22-23). Salamu zake binafsi kwa watendakazi pamoja naye na marafiki waishio huko Rumi (Rum. 16:3-15) huonesha kiwango cha mahusiano yake binafsi. Pia analisalimu kanisa la nyumbani la watendakazi pamoja naye, [akina] Akila na Priska (Rum. 16:4, yawezekana kundi dogo jingine katika 16:10-11).

Jambo la kushangaza ni maelezo ya Paulo juu ya baadhi ya marafiki hawa. Hebu tuchunguze mifano michache.

Foibe [Fibi], mhudumu wa kike wa kanisa lililoko Kenkrea,[101] hana budi kusaidiwa kwa namna yoyote ile. "... kwa sababu yeye naye amekuwa msaidizi wa watu wengi, akanisaidia mimi pia" (Rum. 16:1). Akiwarejea Priska na Akila, anaandika, "Nisalimieni Priska na Akila, watenda kazi pamoja nami katika Kristo Yesu; waliokuwa tayari kukatwa kichwa kwa ajili ya maisha yangu; ambao ninawashukuru, wala si mimi tu, ila na makanisa ya Mataifa yote pia" (Rum. 16:3-4). Anawasalimu wanaume watatu kama "mpenzi" (Rum. 16:5+8+9), Mariamu, "aliyejitaabisha sana kwa ajili yenu" (Rum. 16:6), Androniko na Yunia,[102] ambao walifungwa pamoja na Paulo na "ni maarufu miongoni mwa mitume," (Rum. 16:7), Urbano, "mtenda kazi pamoja nami" (Rum. 16:9) na "Persisi, mpenzi aliyejitahidi sana katika Bwana," (Rum. 16:12) na "Apele, mwenye kukubaliwa katika Kristo" (Rum. 16:10), n.k.

Ni jambo gani Paulo analotaka kulifikia kwa waraka huu? Anakusudia kufanya nini huko Rumi? Mwanzoni mwa waraka, anaandika, "**Kwa kuwa natamani sana kuwaoneni, ili niweze kuweka ndani yenu karama ya kiroho, hatimaye mweze kuimarishwa; Hii inamaanisha, kuwa niweze kufarijiwa pamoja nanyi kwa imani ya pamoja yenu na yangu**" (Rum. 1:11-12). Paulo anataka kuwa na ushirika na waumini wa Rumi, ili yeye na wao waweze kushirikishana karama za kiroho. Neno 'kufarijiwa' katika mstari wa 12 pia lingeweza kumaanisha 'kupewa mausia', na mara nyingine limetafsiriwa namna hii. Baadhi ya wafasili hawakuweza kudhani kuwa Paulo si tu alikuwa na jambo la kuwaambia Warumi bali pia alitarajia baadhi ya faraja na mausia kutoka kwao! Paulo alishawishika, kuwa Wakristo huko Rumi walikuwa "*wamejaa wema, wamejazwa maarifa yote, pia waliweza kuusiana wao kwa wao*" (Rum. 15:14). Kwa nini yeye mwenyewe ajitenge na mausia yao?

Kinyume na mamlaka yake ya kitume, daima Paulo hujionesha yeye mwenyewe kuwa mwenye kutegemea msaada na maombi ya Wakristo

[101] Thomas Schirrmacher. *Der Römerbrief*, op. cit., pp. 311-312.

[102] *Ibid.,* p 312, kuhusu suala la kama Yunia ni mwanamume au mwanamke.

wengine. Twaweza kujifunza kanuni zifuatazo – kanuni ambazo tayari zinafahamika kwetu kutoka kwenye hali ya huko Korintho – kutoka kwake:

*Mausia na faraja havikuwa vya upande mmoja tu katika huduma yake.* Alitengeneza na alitarajia mazingira ambayo kwayo angeweza kupokea huduma hizi za kiroho kutoka kwa wengine.

*Hakujichukulia yeye mwenyewe pekee kuwa mshauri, kiongozi, mnasihi na mtoa usia binafsi wa watendakazi pamoja naye. Daima alitaja kujitaabisha kwao kwa uwazi.* Kumsifu Mungu na kuwasifu wengine halikuwa jambo la kumkanganya; bali aliyachukulia hayo kama pande mbili za sarafu moja. Shukrani kwa msaada wa Mungu na shukrani kwa usaidizi wa wengine huenda pamoja, na vyote havina budi kuelezwa kwa uwazi, si katika 'chumba cha ndani.'

Hata wakati Paulo alipopaswa kuwausia wengine – kama jambo la kweli, hivyo kipekee – alisisitiza yote waliyoyafanya kwake, kwa kanisa na kwa Mungu. Mfano dhahiri uko katika Wafilipi 4:2-3, "Namsihi Euodia, namsihi na Sintike, wawe na nia moja katika Bwana. Naam, nataka na wewe pia, mjoli wa kweli, uwasaidie wanawake hao; kwa maana waliishindania Injili pamoja nami". Tena 'alijivuna' kwa ajili ya kanisa la Korintho (1 Kor. 15:31; 2 Kor. 1:14; 7:4; 9:2-3), hata kwa ajili ya Tito, kabla ya kumtuma kutatua mgogoro kanisani (2 Kor. 7:13, 16)! Paulo aliusia na kupinga kwa ukali usio na maridhiano, lakini kamwe si pasipo kuelezea sifa na shukrani, au pasipo kuyatambua mambo mazuri.

## Tukio la 3: Paulo Anakataa Kupanda Kilele cha Kiroho

(Paulo, Apolo na kanisa la Korintho)

> "Kiburi huleta mashindano tu; bali hekima hukaa nao wanaoshauriana." (Mithali 13:10)

Hebu turudi tena kwenye mahusiano yenye mgogoro kati ya Paulo na Wakorintho. Tatizo moja lilikuwa ni makundi kinzani ya kiroho, ambapo kila moja lilivutiwa na viongozi wa kiroho tofauti. Paulo anaielezea hali hii kama ifuatavyo: "Basi, maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu kusema, Mimi ni wa Paulo, na, Mimi ni wa Apolo, na, Mimi ni wa Kefa, na, Mimi ni wa Kristo" (1 Kor. 1:12).

C. S. Lewis anaandika kwa usahihi: "Ibilisi... daima hupeleka duniani makosa katika pea – pea zinazokinzana. Na mara zote hututia moyo

kutumia muda mwingi kufikiri ipi ni mbaya zaidi."[103] Wakorintho waligawanyika karibu katika kila kitu, lakini kwa ujumla wake Paulo hakuegemea upande wowote,[104] bali kwa ujumla alipinga maoni yote, kwa kuwa hayakukubaliana na mawazo ya Mungu. Suala la viongozi wa kiroho halikuwa la hiari. Baadhi walimheshimu sana Paulo kiasi kwamba akauliza, "Je! Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu?" (1 Kor. 1:13). Kwa wale waliomkana kutokuwa na mamlaka yoyote, alisisitiza wito wake wa utume. Ukweli kwamba Bwana alikuwa amemkabidhi kweli za injili, [yeye aliye] mtumishi wa kawaida wa Mungu, ulikuwa hatarini kwa njia ya wale waliomfanya yeye kuwa kiini cha mvuto, vilevile na wale ambao – yawezekana kwa kuwajibu wale wa kwanza – walimdharau mtume na ufunuo aliouhubiri.

Paulo alikuwa hana budi kuwafundisha Wakorintho, kwamba si yeye, bali ni utume wake wa ki–Mungu na ufunuo katika Maandiko ya Ki–Mungu, yaliyokuwa kipaumbele. "Basi ndugu, mambo hayo nimeyafanya kuwa mfano wa mimi na Apolo kwa ajili yenu, ili kwamba kwa mfano wetu mpate kujifunza kutokupita yale yaliyoandikwa; ili mmoja wenu asijivune kwa ajili ya huyu, kinyume cha mwenzake" (1 Wakorintho 4:6). Kukataa mtazamo usio wa kibiblia hakutoi dhamana kuwa mtu hakosei. Na mtu aweza kuwa mwenye kiburi sawa tu na wapinzani wake. Kwa maoni ya Paulo, tatizo la Korintho lilikuwa kuwa kila mmoja aliweka maoni yake juu ya mafunuo na mafundisho maalumu ambayo yalikwenda zaidi ya ufunuo wa kimaandiko, na kisha kuwanukuu baadhi ya mtume, mwalimu au hata Kristo, [ili] kuthibitisha maoni yao, wakiwachezea watumishi wa Mungu kuwapinganisha kila mtu dhidi ya mwenzake, ingawa wote walifundisha kweli zilezile, japo kwa karama na utume tofautitofauti.

Sehemu yenye kuumiza zaidi ya siasa hizi za makundi ni kwamba walimchonganisha Apolo, mtendakazi mwenza aliyetambulishwa kwenye kanisa la Korintho na Paulo mwenyewe, dhidi ya Paulo mwenyewe. Kama tulivyokwishaona, Paulo anabainisha tatizo kuwa sio tofauti za watu au karama, bali ni uzidishaji mambo na fasili potovu ya Maandiko.

Paulo alikataa kushiriki kwenye aina hii ya ushindani: alidunisha kila mjadala uliokuwa muhimu, wa maana au mafanikio. "Basi Apolo ni nani? Na Paulo ni nani? Ni wahudumu ambao kwao mliamini; na kila mtu kama

---

[103] C. S. Lewis, *Mere Christianity* (New York: The Macmillan Company) l952, p. 160.

[104] Thomas Schirrmacher. *Paulus im Kampf gegen den Schleier*. op. cit., pp. 114-122. Tazama pia Karl Wieseler. *Zur Gesichte der Neutestamentlichen Schriften und des Christentum.* (Leipzig, Germany: J. C.Hinrich'sche Buchhandlung, 1880) pp. 1-53 kuhusu makundi ya Wakorintho.

Bwana alivyompa. Mimi nilipanda, Apolo akatia maji; bali mwenye kukuza ni Mungu. Hivyo, apandaye si kitu, wala atiaye maji, bali Mungu akuzaye. Basi yeye apandaye, na yeye atiaye maji ni wamoja, lakini kila mtu atapata thawabu yake mwenyewe sawasawa na taabu yake mwenyewe. Maana sisi tu wafanyakazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu. Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa, mimi, kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake. Maana msingi mwingine hakuna awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo" (1 Kor. 3:5-11; tazama sura ya 3 na 4).

Katika mazingira ambayo waumini wa kanisa walijaribu kuwatenga Paulo na Apolo, [kwa] kufasili theolojia zinazotofautiana kwa msingi wa watu wanaotofautiana na karama tofauti (mbinu iliyonukuliwa mara nyingi), Paulo alitafuta upatanisho, sio kwa kujielekezea mwenyewe au kusisitiza juu ya umoja, bali kuelekezea kwa msingi mmoja, Yesu Kristo, kama msingi ambao juu yake aina mbalimbali za mitindo, watu, karama na shughuli za kutumwa zaweza kuimarishwa.

Na Apolo? Ingawa hatujui chochote kuhusu jibu lake, twaweza kudhani kuwa alifarijiwa na kutiwa moyo na kukataa kwa Paulo kuruhusu migawanyiko na [kwa] jitihada za Paulo kutafuta msingi wa pamoja. Badala ya kumharibu mtendakazi pamoja naye, Paulo anaupa nguvu msimamo wa rafiki yake katika mazingira tata huko Korintho.

## Tukio la 4: Kufundisha kwa Kielelezo

> "**Toa *maelekezo* kwa mwenye hekima, na bado atabaki kuwa mwenye hekima: mfundishe *mtu* wa haki, naye atazidi katika kujifunza**" (Mithali 9:9).

Acha turudi tena kwenye hali tata na ngumu huko Korintho. Katika 1 Wakorintho 4:4-16, Paulo analinganisha uhusiano wake kwa kanisa na uhusiano wa baba na watoto wake. Anawaita, "watoto niwapendao," na yeye mwenyewe [anajiita] baba yao. Kwa sababu yeye ni baba yao, ni lazima awakaripie kwa ukali. "Siyaandiki hayo ili kuwatahayarisha; bali kuwaonya kama watoto niwapendao" (mst. 14). Tambua kwamba Paulo anahifadhi neno, 'Baba' kwa ajili yake mwenyewe; waumini wengine ambao wanahudumia kanisa la Korintho ni 'walimu' tu. Kwa kweli, Paulo anaona tofauti kubwa kati yake na 'walimu' wengine. Mkufunzi au mwalimu (Kigriki: 'paidagogos'; asili ya neno letu [la Kiingereza] 'pedagogy' = Kiswahili: 'pedagoji' au 'ufundishaji') alikuwa ni mtumwa

tu aliyehusika na ufundishaji wa kitaaluma. Paulo anasema, "**Hata ikiwa mngekuwa na wakufunzi bora elfu kumi kuwafundisha mambo yote mema na yafaayo, jambo hilo lisingenidunisha chochote [mimi] baba yenu!**" Kwa kuwa baba humfundisha mwanawe si tu mawazo bali pia maisha, Paulo anawausia Wakorintho kumwiga yeye (mst. 6). Wazazi hawachunguzi tu mawazo ya watoto wao bali pia vitendo vyao; si kwamba wanapatikana tu kwenye masuala ya kila siku, bali pia kwenye hatari na majanga.

Lawrence Richards, akifafanua tofauti kati ya njia za elimu ya kisasa na elimu ya Biblia, alipendekeza kwamba njia za kisasa hulenga katika kumfundisha mwanafunzi kile mwalimu wake anachojua; elimu ya Kikristo hulenga katika kumfundisha mwanafunzi kuishi kama mwalimu wake anavyoishi.[105]

Watendakazi pamoja na Paulo kwa sehemu kubwa walikuwa ni watu walioamini kutokana na huduma yake au wanafunzi wake waliofunzwa tangu mwanzoni kabisa (mf. Timotheo Mdo. 16:1-3; Akila na Priska: Mdo. 18:1+18+26, Rum. 16:3; 1 Kor. 16:19; 2 Tim. 4:19). Wengine walikuwa 'mitume wa makanisa' (2 Kor. 8:23; Flp. 2:25), wamishenari wenye kuhusika na makanisa kadhaa, waliotumwa na makanisa kwenda kumsaidia Paulo. Mbali na hawa watendakazi, Paulo pia alijikita katika kuwafuasa wazee wa makanisa mapya, kwa ujumla waamini wa kwanza katika eneo [husika]. Cha kushangaza aliwaweka wakfu [aliwawekea mikono] mapema (Mdo. 14:6-7+22-23) na aliondoka mapema baada ya wao kuchukua jukumu lao. Kukaa kwake kurefu katika eneo moja kulikuwa miaka mitatu na nusu (daima kukiwa na mwingiliano) huko Efeso (Mdo. 18:23-19:40).

Paulo alikuwa akiiga tu njia za ufundishaji za Yesu. Marko hutuambia, "**Na aliwaweka wakfu kumi na wawili, ili waweze kuwa naye, na kwamba aweze kuwatuma kuhubiri, Na wawe na nguvu ya kuponya magonjwa, kutoa pepo wachafu**" (3:14-15). Mitazamo mitatu katika uchaguzi wa Yesu ni muhimu.

*A) Yesu alijikita kwa kundi dogo la wanafunzi, "***ili waweze kuwa naye...***"* *Kama ambavyo baba anaweza kuijali vema tu idadi ndogo ya watoto*, ndivyo Yesu alichagua kuyashiriki maisha na mafundisho yake na kundi dogo la wanafunzi. Hakuna mtu awezaye kuishi kihalisia kwa makini na

[105] Lawrence O. Richards, *A Theology of Christian Education*, (Grand Rapids: Zondervan, 1975), p. 30. See also: *Lawrence Richards, A Theology of Church Leadership*, (Grand Rapids: Zondervan, 1979); Lawrence Richards, *A Theology of Personal Ministry*, (Grand Rapids: Zondervan, 1981).

watu wengi kuliko wachache. Twaweza kuona mpaka wa makusudi wa Yesu katika makundi ya karibu ya marafiki zake; makundi madogo yalifurahia ushirika wa karibu naye. Hata alikuwa na mwanafunzi mmoja mpendwa, Yohana (Yohana 19:26; 20:2, 21:7+20; tazama pia 19:27).

Paulo alikuwa na makundi ya karibu ya marafiki, na Timotheo akiwa katikati. “Maana sina mtu mwingine mwenye nia moja nami, atakayeiangalia hali yenu kweli kweli. Maana wote wanatafuta vyao wenyewe, sivyo vya Kristo Yesu. Ila mwajua sifa yake, ya kuwa ametumika pamoja nami kwa ajili ya Injili, kama mwana na baba yake” (Flp. 2:20-22). Kama mtendakazi wa karibu wa mtume, Timotheo alishiriki kwenye nyaraka tano (Wafilipi, Wakolosai, 1 na 2 Wathesalonike na Filemoni),[106] na alikuwa aliyepokea [nyaraka] nyingine mbili. Paulo anamsema kama “Timotheo, mwanagu hasa katika imani” (1 Tim. 1:2; 1:18) na “Timotheo, mwanangu mpendwa” (2 Tim. 1:2).

*B) Yesu alichagua wanafunzi “**kwamba aweze kuwatuma kuhubiri**.”* Lengo la ushirika wa kina namna hiyo na Bwana na utegemezi kwake lilikuwa huduma ijayo. Kamwe Yesu hakukusudia kuwa [hawa] Kumi na Wawili wabaki ‘wamefungwa kwenye vishungi vya vazi lake’ –; walipaswa kwenda ulimwenguni na kuendeleza kazi yake baada ya yeye kurudi mbinguni. Lengo lake lilikuwa Agizo Kuu, “Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari” (Mat. 28;120).[107] Programu ndefu ya mafunzo katika misheni, ambayo kwayo wanafunzi waliishi na kielelezo halisi cha mmishenari – Yesu Mwenyewe – haikuwa holela, bali iliyopangwa kwa umakini, kwa mujibu wa mikakati ifuatayo: 1) Kwanza, Yesu alihubiri yeye mwenyewe, kisha 2) alihubiri wakati wanafunzi wake wakimtazama. Hatimaye, 3) aliwaacha wanafunzi wahubiri wakati akiwatazama, na kisha 4) aliwatumwa waende wao wenyewe (lakini alibaki pamoja nao katika roho kama Bwana Mfufuka.) (Tazama Mat. 28:20).

Paulo aliwafundisha watendakazi pamoja naye kwa namna ile ile. Kama baba na kielelezo, alifanya kazi kwa ajili ya huduma huru ijayo ya makanisa yake na washiriki–wenza wake.

---

[106] Tazama mstari [kifungu] wa kwanza wa vitabu.

[107] Robert E. Coleman. *Des Meisters Plan der Evangelisation* (Neuhasuen, Germany: Hänssler, 1983).

*C) Programu ya kina ya mafunzo ya Yesu ilijumuisha maisha na mafundisho, nadharia na vitendo, ushauri wa mtu mmoja mmoja na ule wa kundi, ukuaji wa ndani na wa nje, kazi na mapumziko, utaalamu na maisha binafsi. Mafundisho yalishabihiana na ushauri na vitendo.*

Paulo alimwiga Yesu katika mtazamo huu pia, kama tuonavyo katika 1 Wathesalonike, "Paulo, na Silwano, na Timotheo," (sio Paulo tu) sio kwamba walihubiri Injili "katika maneno tu," bali pia walikuwa tayari kuyashiriki maisha yao na waumini (1 The. 1:1+5; 2:8). Hata hivyo walihubiri kwa maneno na mafundisho; ama sivyo hakuna mtu ambaye angeweza kuelewa kielelezo chao kilimaanisha nini! Nyaraka kwa Wathesalonike hudhihirisha kuwa Paulo alikuwa amemfundisha Sila na Timotheo kwa kielelezo chake, na kwamba Wathesalonike wenyewe wakawa kielelezo kwa wengine.

Paulo alimjumuisha Sila na Timotheo katika 1 Wathesalonike 1:6, "Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana". Wengi hujikwaa kwa tamko hili. Yawezekanaje Paulo akajilinganisha yeye na watendakazi pamoja naye, na Yesu? Hata hivyo, Biblia mara nyingi hutumia vielelezo vya wanadamu kuonesha kielezo cha Mungu. Je, jambo hilo si halisia? Mtoto hujipatia taswira ya Mungu kutoka kwenye kielelezo cha wazazi wake, na watoto wa kiroho hujipatia taswira yao ya Mungu kutoka kwenye kielelezo cha wazazi wao wa kiroho. Kila baba ni kielelezo, atake kuwa hivyo au la; analo chaguo moja tu kati ya kuwa kielelezo chema au kibaya. Wote wabebao majukumu kanisani, kila mwanasiasa, ni kielelezo, ama kizuri au kibaya.

Lakini je, ni Yesu na Paulo tu waliowekea mpaka programu zao za mafunzo kwa makundi madogo namna hiyo? 2 Timotheo 2:1-2 hupinga wazo hili, "Basi wewe, mwanangu, uwe hodari katika neema iliyo katika Kristo Yesu. Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine". Paulo anatupa sheria ya ufuasi. Kanisa la Bwana hukua kwa usimamizi binafsi wa waumini waliokomaa kiroho kwa makundi madogo madogo, sio kwa jitihada za kiongozi mmoja kuangalia dazani, mamia, au siku hizi, maelfu.

Ukuaji wa kweli wa kiroho na mafunzo ya kweli yenye matunda hutokea wakati Wakristo waliokomaa wanapojikita kwenye makundi madogo ya watoto wa kiroho, wakiyashirikisha maisha na mafundisho hadi waumini wachanga wanapokuwa wamekomaa kiasi cha kujitegemea. Hii ni njia bora ya kutimiza Agizo Kuu [la] kuyafanya mataifa yote kuwa wanafunzi ... kuwafundisha kuyashika yote ambayo Kristo aliyaamuru (Mat. 28:18-20).

Ni kanuni zipi tunazoweza kujifunza kutoka kwa Paulo?

1) Paulo aliwapenda watendakazi pamoja naye na alikuwa akipatikana kwao, sana. Upendo wake haukumwongoza kuwatendea kama watoto milele, bali aliwaelekeza kwenye makuzi ya kiroho na kujitegemea.
2) Paulo aliwekeza zaidi kwenye mahusiano ya wamishenari kila mmoja na mwenzake na katika makuzi yao ya kiroho kuliko maelezo ya kina au masuala ya kimkakati (ingawa pia alikuwa akifahamu vema aina hii ya tatizo!).
3) Daima na kwa kina Paulo aliomba kwa ajili ya watendakazi wenzake na makanisa yake, na aliwatarajia nao wafanye hivyo hivyo.
4) Paulo alichochea ukuaji wa karama za watendakazi wenzake. Alijua kwamba Mungu aliumba watu wa namna mbalimbali na alimtarajia Yeye kuwatumia ipasavyo.

# Yesu kama Mwelimishaji Mkuu[108]

“Watu hawajali kile unachojua,
mpaka wajue kuwa unajali.”

## 1. Mafundisho na Maisha

Kwa jinsi Wakristo wanavyohusika, suala la elimu ni lazima lishughulikiwe kutoka kwenye ufunuo wa kiungu wa Neno la Mungu. Kifungu cha Agano Jipya ambacho kwa uwazi zaidi hufundisha uvuvio wa kiungu wa Maandiko pia kwa uwazi hufundisha jukumu la Biblia kuhusiana na elimu. “**Maandiko yote hutolewa kwa uvuvio wa Mungu, na ni yenye faida kwa mafundisho, kwa kuonya, kwa kurekebisha, kwa maelekezo katika haki, ili mtu wa Mungu aweze kukamilishwa, na kutayarishwa vema kwa ajili ya kila kazi njema**” (2 Timotheo 3:16-17). Si tu kwamba Paulo anahusika na kurithisha ufahamu juu ya Biblia au elimu ya kitaaluma au utengenezaji wa tabia au sifa za kiroho, bali pia na mafundisho jumuifu ambayo hukidhi nyanja zote za maisha ambazo humtayarisha vema Mkristo “kwa ajili ya kila kazi njema.” Ikiwa huduma ya muda wote katika kanisa au katika umisheni inapaswa kuheshimiwa, Biblia ni ya muhimu katika maandalizi ya kuifanya huduma hiyo. Si tu kuwa yaliyomo katika Biblia ni muhimu, bali pia maelekezo ya kibiblia ya *jinsi* ambavyo yaliyomo hayo yanavyopaswa kuwasilishwa.

Wakristo wengi wana imani iliyogawanyika! Kwa sababu wanatofautisha kati ya tabia, maadili, mafundisho na maisha, wanakosa umoja jumuifu katika maisha yao – walau kulingana na suala la elimu lilivyo. “Mwako” (neno linalofupisha maendeleo yenye sura mbalimbali) limefanya mgawanyiko kati ya fikra na matendo, [hili ni] jambo lisilokubaliana na mafundisho ya kibiblia. Tangu wakati huo, maisha na tabia ya profesa wa Chuo Kikuu vinachukuliwa siyo muhimu vikilinganishwa na mafanikio yake ya kisayansi, hata wakati ambapo

[108] Kwa asili kilichapwa na kuongezwa kutoka kwenye „Jesus as Master Educator and Trainer“. Training for Crosscultural Ministries (World Evangelical Fellowship) 2/2000: 1-4; „Paul and His Colleagues“. Training for Crosscultural Ministries (World Evangelical Fellowship) 3/2000: 6-8; „Having a Role Model, Being a Role Model“. Training for Crosscultural Ministries (World Evangelical Fellowship) 1/2001: 4-7.

uhalisia – hata wakati iwapo ni uhalisia wa wanafunzi wake au watendakazi wenzake tu … hupatana na sayansi.

‘Mtazamo’, ‘Kujifunza’, ‘kuelewa’, ‘kuelimisha’, ‘kufundisha’, n.k. yote ni maneno ambayo Biblia huyahusisha na nyanja za kiakili vilevile na uwezo wa kutumia kile ambacho mtu amejifunza.[109] Matumizi ya Agano la Kale ya neno “kujua” kuelezea ukamilifu wa uhusiano wa kindoa, hudhihirisha pia mtazamo huu (Mwanzo 1:4-1, 17, 25; 19:8; 24:16: 1 Fal. 1:4),[110] kwa kuwa ‘ufahamu’ huu huhusisha uzoefu wa uwezo wa kifikira, kihisia, kiroho, kiakili na wa kimwili wa mtu.

Maandiko yasiyohesabika huonesha kutogawanyika kwa mafundisho na maisha, lakini mfano mmoja unatofautisha. Paulo anamwambia Timotheo, aliye mtendakazi pamoja naye na mrithi wake aliyemfundisha, “**Uwe mwangalifu kwa nafsi yako na kwa mafundisho**” (1 Tim. 4:14); angalia pia 1 Tim. 4:12; 2 Tim. 3:10; 3:1-4:5; 1 Thes. 1:1-2:12). Kwa Paulo, ni dhahiri kuwa wajibu wa Timotheo kwake mwenyewe na kwa makanisa mengi hujumuisha kupinga makosa ya mafundisho.

Kitabu cha Mithali ni kitabu kikuu cha Biblia kwa ajili ya elimu. Maelezo yake ya mafunzo jumuifu hujumuisha uwezo wa kujitegemea katika maisha ya kila siku na kushirikiana na wengine kwa kufanya kazi pamoja nao, kuwajali, kutafuta amani nao na kusimamisha uadilifu na haki. Kiini cha yote ni “Kumcha BWANA ni mwanzo wa hekima” (Mith. 9:10; 1:7; 15:33; Ayubu 28:28, Zaburi 111:10). Lengo la mpango wa mafunzo ya Mithali kwa uwazi ni kumwongoza mwanafunzi kwenye ‘hekima’, hiki ni kigezo awali cha mtu kujitegemea, kwa kumwelekeza kutii sheria za walimu wake na Sheria ya Mungu. Hata hivyo, hekima si zoezi la kiakili tu, bali pia ni uwezo wa kutumia ufahamu katika maisha na katika mahusiano ya watu binafsi (angalia Mithali 4:1-9).

Katika Agano la Kale, neno “mfuasi” au “mwanafunzi” mara nyingi hutumika kumaanisha mwamini, “**Bwana Mungu amenipa sikio la wenye elimu… Huniamsha asubuhi kwa asubuhi, huliamsha sikio langu kusikia kama wenye elimu**” (Isaya 50:4-5). Neno ‘mfuasi’ limechotwa kutoka katika hali ya ulinganifu wa juu (‘discipulus’)[111] ya neno la Kilatini ‘junior’ (mwanagenzi, mwanafunzi au mtu wa ngazi ya chini[112]) na hii

---

109 Tazama: Laurence O. Richards. A Theology of Christian Education (Grand Rapids, Michigan: Zondervan, 1975) pp. 32-24.

110 Friso Melzer. Das Wort in den Wörtern: Die deutsche Sprache im Lichte der Christus-Nachfolge: Ein theo-philologisches Wörterbuch (Tübingen, Germany: J.C. B. Mohr, 1965) p. 113.

111 *Ibid.,* p. 237-238.

112 *Ibid.,* p. 237.

humaanisha ‘mwanafunzi’. Agano Jipya, kwanza hutumia neno “mathetes” kumaanisha mitume wawili (kwa kuanzia Yohana 2:2 na kwa ujumla katika injili hii), na baadaye kuwaelezea wafuasi wote wa Yesu (Luka 6:17; Matendo 9:25). Utume Mkuu, ambao pia hutumia neno hili, kwa uwazi huzungumzia kufundisha na kufanya yale yote yaliyofundishwa, “mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi… na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi …” (Mat. 28:18-20). Wakristo ni wanafunzi ambao kamwe hawaachi kujifunza. Sifa ya kielelezo cha hekima. Kadiri mtu anavyozidi kufahamu, ndivyo anavyotambua ni kwa uchache namna gani anavyoelewa na ni kwa wingi namna gani kuna mambo ya kujifunza “… Kumcha BWANA ni mwanzo wa hekima, na kumjua Mtakatifu ni ufahamu” (Mithali 9: 8-10).

## 2. Mafunzo ya Mitume Kumi na Wawili

Mfano mzuri wa umuhimu wa mafunzo na elimu ni mafunzo ya mitume kumi na wawili, ambayo yalijengwa juu ya mpango wa kielimu wa kina ambao tunaweza tu kuufanyia maelezo ya kimuhtasari hapa. Maelezo ya kina zaidi yangehitaji taarifa juu ya mtiririko wa mwanzo hadi wa mwisho wa mafundisho ambayo Yesu aliyafundisha kwa miaka mitatu na maelezo ya tabia yake kwenye ushauri wa mtu binafsi au wa kundi. Kwa kiwango chochote kile, mpango wake uliunganisha maelekezo na maisha, ufundishaji na ushauri wa mtu mmoja mmoja na kuishia kuwa elimu jumuifu.[113]

Mitume kumi na wawili tayari walikuwa wamemsikia Yesu akihubiri kabla ya kuokolewa kwao na wakawa wa kwanza kuwa wafuasi wa jumla wa Yesu. Mpaka pale walipochaguliwa miongoni mwa kundi la wengi kuwa mitume. (Mifano ya mwito wa jumla ni mwito wa Petro katika Yohana 1: 35-42 na Luka 5:1-11; kuitwa kwa Mlawi/Mathayo katika Mathayo 9:9-13; Marko 2:13-17 na Luka 5:27-32. Linganisha mwito wa wafuasi wengine katika Mathayo 4:18-22 na Marko 1:16-20.

Injili–fanani zote tatu zinaeleza mwito maalumu wa Thenashara, zikijumuisha orodha kamili ya majina yao (10:1-4, Marko 3:13-17, Luka 6:12-16). Hebu tuangalie matukio matatu. “Akawaita wanafunzi wake kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoe, na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina” (Mathayo 10:1. Orodha inafuata katika mistari ya 2-4). Katika Luka 6:12, Yesu anaomba usiku mzima, kisha anawaita wanafunzi wake na kuchagua kumi na wawili “ambao

113 Bado ni somo bora: A. B. Bruce, *The Training of the Twelve*, Grand Rapids: Kregel Publ., 1971 (originally publ. 1894).

aliwaita Mitume" (Luka 6:13. Orodha ya majina inafuata katika mistari ya 14-16). Ni lazima Yesu alikuwa na wafuasi wengi zaidi kuliko wale Thenashara; Luka 6:17 hutofautisha kati ya "makutano makubwa ya watu" na "kundi la wanafunzi", ambalo pia lilijumuisha wanawake walioambatana na Bwana (Luka 8:2-3). Wakati Yesu alipozungumza juu ya sifa za uanafunzi, wengi walimwacha, lakini pia wengi, ikijumuisha wale Thenashara, walibaki (Yohana 6:66-69[114]). Marko anatueleza "Akapanda mlimanai, akawaita aliowataka mwenyewe; wakamwendea. Akawaweka watu kumi na wawili, wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri, tena wawe na amri ya kutoa pepo" (Marko 3:13-16. Orodha ya majina inafuata katika mistari ya 16-19). Kwa hiyo, Yesu aliwachagua Thenashara kutoka miongoni mwa kundi kubwa la wanafunzi, lakini fungu hili la mwisho huelezea mchakato na lengo la uchaguzi wake.

Ningependa sasa kufanya muhtasari wa sifa za mpango wa mafunzo uliotolewa kwa wanafunzi kumi na wawili kama ilivyoelezwa katika Marko 3:14. Vigezo vitatu vilikuwa muhimu katika uchaguzi wa Mitume:

**1) Yesu aliliwekea mpaka kundi la wanafunzi wake kuwa lenye idadi ndogo, kwa kuwa, kama vile baba anavyoweza kuwatimizia vema mahitaji watoto wachache, angeweza kutoa mafunzo yanayohitajika kwa wafuasi wachache tu kwa wakati.**

Wale kumi na wawili walikuwa wamechaguliwa kuwa naye na kuyashiriki maisha yake, lakini hakuna yeyote ambaye anaweza kuyashiriki maisha yake na kundi kubwa la watu. Ndoa, uhusiano wa karibu zaidi wa kibinadamu, imewekewa mpaka wa watu wawili tu. Idadi ya watoto katika familia ni kubwa, lakini bado inawezekana kuwahudumia – hakuna mtu yeyote ambaye angeweza kutekeleza wajibu wake unaojitosheleza kama mzazi ikiwa angekuwa na watoto 40 – ni taasisi ya yatima au vijana inayoweza kujaribu. (Ingawa kamwe siwezi kukosoa kazi ya kujitoa mhanga ya wafanyakazi wa kazi za kijamii, zinazofanywa katika taasisi hizo, ninapaswa kudokeza kuwa haziwezi kutoa uangalizi mkamilifu sawa na ule unaotolewa na wazazi kwenye familia yenye idadi ndogo ya watoto). Utambuzi wa Yesu kujizuia unaweza pia kuonekana katika makundi madogo madogo ya marafiki zake, makundi madogo madogo yenye ukaribu wa mawasiliano naye. Na hata alikuwa na mpendwa, yaani Yohana, "mwanafunzi aliyempenda" (Yohana 19:26, 20:2, 21:7, 20; 19:27). Jozi mbili za ndugu Yakobo na Yohana, na Petro na Andrea, walishirikishwa kwenye matukio mengi ambayo wengine

[114] Tofauti na Injili zingine. Kitabu cha Yohana hutumia neon 'mwanafunzi' kuwataja [wale] Kumi na Wawili tu.

hawayakushiriki (Mathayo 4:21; 10:2, Marko 1:19; 3:17; 10:35, 41; Luka 5:10; 6:14; 9:54; Matendo 1:13, 12:2). Ndugu wote wanne walikuwepo katika Marko 1:29, 13:3, watatu wao (akikosekana Andrea) katika Marko 5:37, 14:33 na Luka 8:51 na hasa wakati wa Kubadilika Sura kwa Yesu, Mathayo 17:1-3, Marko 9:1-4, Luka 9:28-30 na baadaye, kama nguzo ya kanisa katika Wagalatia 2:9.

| **Makundi Muhimu Yaliyomzunguka Yesu** |
|---|
| **Idadi Kubwa (= wote), uhusiano legelege**<br>• makutano<br>• kundi la wanafunzi<br>• wanafunzi wote waliombatana naye, wakiwemo wanawake<br>• wale Sabini<br>• wale Thenashara<br>• wanafunzi wanne, Petro na Andrea, Yakobo na Yohana. (Jozi mbili za ndugu, au wakati mwingine Petro, Yakobo na Yohana tu)<br>• mwanafunzi wake mpendwa aitwaye Yohana<br>**Idadi ndogo (= mmoja), uhusiano wa karibu zaidi** |

**2. Yesu aliwachagua Thenashara “wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri”. Lengo la ushirika wa karibu na Yesu na kumtegemea Yeye lilikuwa ni maandalizi ya huduma yao.**

Uhusiano wa karibu na Yesu halikuwa lengo la mwisho la mafunzo ya wanafunzi. Bali, walipaswa kwenda peke yao na kuendeleza kazi yake. Kama alivyotumwa na baba yake (Yohana 3:16-18; 8:16, 26, 29; 12:45-49, 16:5, 28; 17:3, 8) naye amtuma Roho Mtakatifu kuchukua nafasi yake (Yohana 14:15-31, 16:5-11, 12-17). Anahamishia agizo hilo kwa mitume. Katika Yohana 17:18, anamwambia Baba yake, “Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni”. Katika Yohana 20:21, anawaambia wale Thenashara, “kama Baba alivyonituma mimi, mimi nami **nawatuma** ninyi”.

Tangu mwanzo Yesu alikusudia kuwaandaa kwa ajili ya Utume Mkuu, “mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi ... na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi...” (Mathayo 28:18-20). Walipaswa kufanya kitu kile kile alichokifanya hapa duniani ambacho alikifanya wakiwa pamoja naye – kuhubiri injili kwa watu wengi, kuchagua wanafunzi kutoka miongoni mwa kundi kubwa la walioamini, na kushirikishana maisha yao kwa

kufundisha, kuwandaa kwa mafunzo [wale] waliochaguliwa ili wawe viongozi wa kiroho.[115]

Maombi yake katika Yohana 17 kwa uwazi yanadhihirisha kuwa, mbali na kupata wokovu wetu pale Msalabani, alikuwa na kazi nyingine maalumu ya kufanywa na wale Thenashara. Katika mstari wa 4 anasema, "Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye" na anaongeza sababu, "Sasa wamejua ya kuwa yote uliyonipa yatoka kwako. Kwa kuwa maneno uliyonipa nimewapa wao; nao wakayapokea, wakajua hakika ya kuwa nalitoka kwako, wakasadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma" (Mistari ya 7-8). Yesu aliwataka wanafunzi si tu kujua alichokijua, bali pia kuishi kama alivyoishi. Lengo la mpango wake wa mafunzo lilikuwa kwa wao kufuata hatua zake (isipokuwa kwenye Uungu wake na kwa kifo chake cha kidhabihu pale Msalabani) kama alivyorudia mara kwa mara kuwafundisha.

Muktadha wa Luka 6:40 kipekee ni wenye kuvutia ("**Mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake, lakini kila mtu ambaye amefunzwa vema atakuwa sawa na mwalimu wake**"). Katika mstari wa 39,[116] anauliza, "Je, aliye kipofu aweza kuongoza kipofu? Hawatatumbukia shimoni wote wawili?" Viongozi vipofu ni watu ambao wanaweza kuongea vema, lakini ni vielelezo vibovu, kwa kuwa hawana chochote cha kuiga.

Jambo muhimu ni ukweli kuwa mitazamo hiyo yote iko pamoja, *"wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri..."* Mahusiano ya karibu kiasi hicho kati ya mwalimu na mwanafunzi yanahalalishwa tu pale yanapokusudia kuwasaidia wanafunzi kujitegemea. Kukuza watoto vema siku zote hujumuisha aina fulani ya mgogoro katika makuzi tangu kwa mtoto mchanga asiyeweza kujisaidia kabisa na anyewategemea kabisa wazazi wake kuelekea kwa mtu mzima anayejitegemea. Kila uhusiano, ikijumuisha msisitizo juu ya utii, unaelekezwa kwenye kujitegemea, si tu katika kumkuza mtoto, bali pia mafunzo ya watumishi katika Ufalme wa Mungu. Tangu mwanzo, mpango wake wa mafunzo, hata alipokuwa akiwaita wanafunzi wake, Yesu alikuwa na mtazamo wa Utume Mkuu. Alijua kile ambacho bado walikuwa hawajakiona, ya kuwa aliwachagua ili awafunze kama viongozi wajao katika Kanisa na katika nyanja ya umisheni, siku ile ambapo angewaacha.

**3. Mpango wa mafunzo wa Yesu haukuwa wa shaghalabaghala, bali ulifuata mpangilio dhahiri. Wanafunzi walipaswa kufunzwa kwa ajili**

[115] Tazama Robert E. Coleman, *The Master Plan of Evangelisation,* Old Tappan: Revell, 1963.

[116] Lawrence O. Richards. *A Theology of Christian Education,* op.cit., pp. 54-56.

**ya nyanja ya umisheni kwa kuishi na kufanya kazi kwa miaka kadhaa wakiwa na kielelezo halisi cha mmishenari, yaani Yesu mwenyewe.**

Mpangilio wa kufuatana wa mpango wake wa mafunzo unaliweka hili dhahiri. Kwanza, alihubiri peke yake, kisha alihubiri wakati wanafunzi wakimtazama. Baadaye, aliwaacha wahubiri wakati yeye akiwatazama. Baada ya hapo aliwatuma katika makundi ya wawili wawili na kujadili matokeo pamoja nao. Kazi ya kwanza, ya muhula mfupi inaelezwa katika Mathayo 10:1-11, Marko 6:7-13 na Luka 9:1-6. Mwishoni, aliwatuma peke yao,[117] (akibakia pamoja nao kama Bwana Mfufuka – Mathayo 28:18-20). Wale Thenashara waliendelea kufanya vile vile kwa Wakristo wengine.

| **Njia ya Kuelekea Kujitegemea** |
|---|
| 1) Yesu anahubiri yeye mwenyewe<br>2) Yesu anahubiri wakati wanafunzi wakimtazama<br>3) Wanafunzi wanahubiri wakati Yesu akiwatazama<br>4) Wanafunzi wanatumwa kwa kazi ya kipindi kifupi<br>5) Wanafunzi wanatumwa kwa kazi ya kudumu<br>6) Wanafunzi wanahubiri wakati wengine wakiwatazama<br>7) na kadhalika<br><br>1) Mimi<br>2) Mimi na Wewe<br>3) Wewe na Mimi<br>4) Wewe jaribu peke yako, Mimi ninatoa maoni<br>5) Uko peke yake kabisa<br>6) Wewe na Mwingine<br>7) Mwingine na Wewe<br>8) na kadhalika. |

[117] Zoezi la kwanza la muhula mfupi linaelezwa katika Mathayo 10:1-11, Marko 6:7-13, Luka 9:1-6. Tazama pia utumwaji wa wale Sabini katika Luka 10:1-16 na majadiliano Yake pamoja nao juu ya uzoefu wao katika Luka 10:17-21.

Mpango huu hufanya kazi vizuri, si tu katika mafunzo ya watumishi wa kanisa bali katika kila aina ya elimu inayojiwekea yenyewe lengo sahihi, kujitegemea chini ya Mungu.

**4. Mpango wa mafunzo ya Yesu kwa wanafunzi ilijumuisha mawanda yote ya maagizo na maisha, nadharia na vitendo, ushauri wa mtu mmoja mmoja na wa kikundi, shughuli binafsi na za jamii, kazi na mapumziko, weledi na maisha binafsi. Kufundisha na kushauri huunda kitu kimoja.**

Mikanganyiko hii ya wazi haikuwa imetenganishwa katika maeneo mbalimbali ya maisha, bali yote ilifanywa kwa wakati mmoja, kutegemea matakwa na uwezekano wa hali iliyopo.

## 3. Paulo na Watendakazi Wenzake

Mbali na Yesu na wale Thenashara, mfano mzuri unaojulikana wa kufunza wanafunzi ambao hujumuisha maisha na maelekezo, kufundisha na kushauri; muundo na uigaji, ni kazi ya Paulo na watendakazi wenzake, ambao tunawafahamu tu kutoka kwenye "Minyororo ya vielelezo vya kuigwa" michache.

| Mifano ya Minyororo ya Vielelezo vya Kuigwa |
|---|
| Kumbukumbu la Torati, Yoshua, Waamuzi, Musa – Yoshua – Wazee |
| 1 Petro 5:1-3, Yesu – Petro – wazee – wanafunzi |
| 2 Timotheo 2:2, Paulo – Timotheo – "watu waaminifu" – "wengine pia" |
| 1 Wathesalonika 1:6-7, Paulo – Timotheo na Silvano – Wathesalonike – jimbo la Akaya – ulimwengu wote |

Paulo hakufanya kazi peke yake, bali aliambatana na wasaidizi au watumishi wenzake (kwa mfano, Matendo 17:15), ambao walipokea mafunzo ya kiroho wakiwa naye. Kabla ya kuanza kazi yake ya injili huko Efeso, alisubiri mpaka wafanyakazi wenzake walipowasili: "Hata Sila na Timotheo walipotelemka kutoka Makedonia, Paulo akasongwa sana na lile neno, akiwashuhudia Wayahudi ya kwamba Yesu ni Kristo" (Matendo 18:5). Hata baada ya mtume kuota juu ya mtu aliyekuwa akimwita kwenda Makedonia, aliwasiliana na wengine kabla ya kuanza safari: "Basi alipokwisha kuyaona yale maono, mara tukataka kutoka kwenda Makedonia, kwa kuwa tuliona hakika ya kwamba Mungu ametuita tuwahubiri Habari Njema" (Matendo 16:10). Wasaidizi hawa kwa ujumla walikuwa ni watu ambao

aliwaongoza kwa Kristo na alikuwa amewafundisha tangu mwanzo, nao ni: Timotheo (Matendo 16:1-3), Akila na Prisila (Matendo 18:2, 18, 26; Warumi 16:3; 1 Wakorintho 16:19; 2 Timotheo 4:19). Vilevile kulikuwa na ‘mitume’ wa makanisa (2 Wakoritho 8:23; Wafilipi 2:25), yaani wamishenari waliotumwa kuchukua wajibu kwenye makanisa ambayo Paulo aliyaanzisha.[118] Mbali na wasaidizi wake, Paulo alijikita katika kuwafunza wafuasi wengine, hasa wazee wa makanisa mapya. Aliwaweka wakfu wazee katika hali ya kushangaza mwanzoni tu mwa kazi (Matendo 14:22-23), kwa kawaida ni waamini wa kwanza, na akabaki kwa muda mfupi katika eneo moja, kwa kuwa alitegemea wazee waendeleze kazi yake. Kukaa kwake kurefu kwa miaka mitatu na nusu, katika eneo moja kulikuwa ni Efeso, na huku pengine kulisababishwa na mambo mengi ya muda mrefu yaliyoingilia kati.[119]

Nyaraka kwa Wathesalonike ni ushuhuda bora zaidi kwamba si Paulo pekee, bali pia na watumishi wenzake (Silvano na Timotheo), [na] si kwamba walihubiri tu Injili, bali pia walikuwa wameandaliwa kuyashirikisha maisha yao (1 Wathesalonike 2:8) kama vielelezo. Kwa kawaida wote watatu walihubiri kwa maneno na kwa mafundisho. Ama sivyo, ni kwa namna gani hadhira yao ingeelewa maana ya mifano yao? Nyaraka hizi zinadhihirisha jinsi Timotheo na Silvano, waliofundishwa na Paulo kama vielelezo vyao, walivyokuwa vielelezo wao wenyewe kwa Wakristo wa Thesalonike ambao pia walipaswa kuwa vielelezo.

Silvano na Timotheo wanajumuishwa, kwa kuwa 1 Wathessalonike 1:6 hutuambia “Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana”. Wengi wameiona kauli hii kuwa yenye kukwaza. Inawezekanaje Paulo ajilinganishe na Yesu? Lakini Maandiko yenyewe husifia vielelezo kufuatisha mfano wa Mungu. Je, hilo haliko hivyo siku zote? Uelewa wa mtoto juu ya Mungu hutegemea wazazi wake, kama ni mzuri au ni mbaya. Watoto wa kiroho huvutwa na mfano mzuri au mbaya wa uhusiano wa wazazi wao wa kiroho na Mungu.

---

[118] Thomas Schirrmacher. *Der Römerbrief.* 2 Vols, (Neuhausen, Germany: Hänssler, 1993) Vol. 1, p. 291-299.

[119] Heinz Warnecke. Thomas Schirrmacher. „Plädoyer für die historische Glaubwürdigkeit der Apostelgeschichte und der Pastoralbriefe.“ in War Paulus wirklich auf Malta (Neuhausen, Germany: Hänssler, 1992) pp. 223-227.

| **Mafundisho na Maisha, Kielelezo na Uigaji katika Nyaraka za Wathesalonike** |
|---|
| 1 Thes. 1:5-9, "… ya kwamba injili yetu haikuwafikia katika maneno tu, bali na katika nguvu, na katika Roho Mtakatifu, na uthibitifu mwingi; kama vile mnavyojua jinsi zilivyokuwa tabia zetu kwenu, kwa ajili yenu. Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana, mkiisha kulipokea neno katika dhiki nyingi, pamoja na furaha ya Roho Mtakatifu. Hata mkawa kielelezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia na katika Akaya. Maana kutoka kwenu neno la Mungu limevuma, si katika Makedonia na Akaya tu, ila na kila mahali imani yenu mliyonayo kwa Mungu imeenea; hata hatuna haja sisi kunena lolote. Kwa kuwa wao wenyewe wanatangaza habari zetu, jinsi kulivyokuwa kuingia kwetu kwenu; na jinsi mlivyomgeukia Mungu mkaziacha sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai, wa kweli;" |
| 1 Thes. 2:7-12, "…bali tulikuwa wapole katikati yenu, kama vile mlezi awatunzavyo watoto wake mwenyewe. Vivyo hivyo nasi tukiwatumaini kwa upendo mwingi, tuliona furaha kuwapa, si Injili ya Mungu tu, bali na roho zetu pia, kwa sababu mmekuwa wapendwa wetu. Maana, ndugu, mnakumbuka taabu yetu na masumbufu yetu; kwa kuwa mchana na usiku tulifanya kazi tusije tukamlemea mtu wa kwenu awaye yote, tukawahubiri hivi Injili ya Mungu. Ninyi ni mashahidi, na Mungu pia, jinsi tulivyokaa kwenu ninyi mnaoamini, kwa utakatifu, na kwa haki, bila kulaumiwa; vilevile, kama mjuavyo, jinsi tulivyomwonya kila mmoja wenu kama baba awaonyavyo watoto wake mwenyewe, tukiwatia moyo na kushuhudia; ili mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Mungu, mwenye kuwaita ninyi ili mwingie katika ufalme wake na utukufu wake." |
| 1 Thes. 2:14, (kwa kanisa lililoko Thesalonike) "Maana ninyi, ndugu, mlikuwa wafuasi wa makanisa ya Mungu yaliyo katika Uyahudi, katika Kristo Yesu; kwa kuwa mlipata mateso yale yale kwa watu wa taifa lenu wenyewe, waliyoyapata na hao kwa Wayahudi;" |
| 2 Thes. 3:7, "Mwajua wenyewe jinsi iwapasavyo kutufuata; kwa sababu hatukuenda bila utaratibu kwenu;" |
| 2 Thes. 3:9, "Si kwamba hatuna amri, bali ni kuzifanya nafsi zetu kuwa kielelezo cha jinsi mnavyopaswa kutufuata." |

Kila mmoja ni mfano wa kuigwa: hatuwezi kuchagua kama tunataka kuwa kielelezo au la, bali ni kuwa kati ya mfano mbaya au mfano mzuri. Kila

kiongozi wa Kanisa na kila mwanasiasa ni kielelezo na anaweza kuchagua tu ni aina gani ya kielelezo anachotaka kuwa. Jambo hili ni mahususi kabisa katika mafunzo ya theolojia.

Kuna masomo mengi kuhusu wapinzani wa Paulo, lakini rafiki zake na watendakazi wenzake wametelekezwa kwa kiasi kikubwa.[120] Kuna machapisho mawili juu ya watendakazi pamoja na Paulo, yote yakiwa yameandikwa kutoka kwenye mtazamo tofauti.[121] Wolff–Henning Ollrog anadhani kuwa matumizi ya Paulo ya wasaidizi wengi hayakuwa ya maamuzi holela, bali ilikuwa ni mbinu ya kimakusudi ya kimishenari. Ikianza kwa taarifa za kihistoria zilizotolewa katika Agano Jipya na masomo juu ya istilahi 'synergos' ('colleague'), tasnifu hii iliyohakikiwa tena inafikia kwenye makundi matatu ya wasaidizi: 'watendakazi pamoja naye walikuwa karibu zaidi', walioambatana na Paulo daima, 'watendakazi pamoja naye waliokuwa huru', waliomsaidia katika mazingira na nafasi maalumu, na wajumbe wa makanisa ya mitaa', waolichaguliwa na makanisa yao kuambatana na mtume ili kushiriki katika jitihada zake za kimishenari. Kundi la mwisho lililotajwa lilifanya ushirikiano uwezekane kati ya makanisa, wasaidizi na misheni. Ollrog anahitimisha kwa masomo ya theolojia ya mtu binafsi na mjadala wa tathmini ya Paulo juu yao. Kitabu kinafungua nyanja mpya ya utafiti na kuweka wazi mahusiano yaliyoachwa na mafundisho ya kimapokeo, lakini cha kushangaza ni kuwa [kitabu hiki] ni kipande tu, kwa kuwa mwandishi anazikataa 2 Wathessalonike, Wakolosai; Waefeso na nyaraka za kichungaji (1 na 2 Timotheo, Tito) kuwa siyo za Paulo,[122] hivyo anatupilia mbali kiwango kibubwa cha taarifa. Maswali mengi anayoshidwa kuyatatua yangeweza kujibiwa, ikiwa njia kinzani na kali aliyotumia isingeondoa taarifa hizo za uhakika. Kitabu cha Matendo ya Mitume kinakumbana na tatizo lile lile, kwa Ollrog anashindwa kukichukulia kwa umakini, ingawa anakichukulia kuwa ni kazi ya Luka. Ollrog daima anaonekana kujua ni kwa nini Luka kwa makusudi aliharibu ukweli wa habari zake.

Tatizo hili la mwisho halionekani katika kitabu cha Bönig.[123] Akijikita katika uhusiano wao na mitume, mwandishi anaelezea wasaidizi kumi na

---

120 Wolf-Henning Ollrog. Paulus und seine Mitarbeiter Untersuchungen zu Theorie und Praxis der paulinischen Mission. Wissenschaftliche Monographien zum Alten und Neuen Testament 50 (Neukirchen, Germany: Neukirchener Verlag, 1979) p. 3.

121 Ibid., and Manfred Bönig. *Wir haben die Welt erobert: Die Mitarbeiter des Apostel Paulus* (Witten, Germany: Bundes Verlag, 1980).

122 Ollrog, *op. cit*., p. 1.

123 Manfred Bönig, *op. cit.*

sita wa Paulo. Ingawa Bönig anatupa somo zuri lililotolewa kwenye somo kamilifu la vyanzo vyote vya Agano Jipya, anashindwa kujali mbinu za Paulo katika kuchagua njia zake. Tena, tunakutana na tatizo la zamani: Mhakiki wa kiliberali anatupa somo bora ambalo linafungua mwelekeo mpya wa Agano Jipya, lakini anaacha taarifa nyingi ili kuvivunja vizingiti vya kimapokeo, wakati mwandishi wa kikonsevativu anatupa kazi ambayo ni ya kujenga lakini isiyojitosheleza. Hadi pale itakapowezekana kuunganisha ukamilifu wa kitaaluma na ufasili wa kikonsevativu, msomaji anayevutiwa ni lazima asome vitabu vyote na kuvuna yaliyo bora kutoka kwenye vitabu hivyo.

Mtu anaweza kupinga kuwa ushirikishaji wa kina wa maisha na kazi na kundi dogo la watoto wa kiroho umefungwa kwa Yesu na Paulo. 2 Timotheo 2:2 inapinga fikra hii, hata hivyo, kwa kuamuru ufuasaji kama mpango endelevu kwa kanisa na misheni: “Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.” Kielelezo cha Yesu kinawekwa katika mpango wa mafunzo wa lazima. Kanisa la Kristo hupanuka kupitia kazi ya Wakristo waliokomaa, wenye nia ya kiroho wenye makundi madogo ya waamini, siyo kwa majaribio ya kiongozi mwajibikaji mmoja anayejaribu kutenda haki kwa dazani, mamia au hata maelfu kwa mara moja. Kukua kiroho kwa kweli na mafunzo yenye matunda hutokea pale ambapo Wakristo waliokomaa, wenye nia ya kiroho hujikita kwenye kikundi kidogo cha watoto wa kiroho, ambamo hushiriki maisha na maelekezo mpaka pale watoto wanapokuwa watu wazima wanaojitegemea, wao wenyewe wakiwa na uwezo kuchukua wajibu kwa ajili ya wengine. Hii ndiyo njia nzuri ya kutimiza Utume Mkuu, “... mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi... na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi;” (Mathayo 28:18-20). Tunapata vielelezo vingi vya minyororo ya aina hii katika Biblia.

| **Fasili ya Kufuasa**[124] |
|---|
| *Kila mstari huelezea hoja kuu*<br>– Kuwafuasa wengine<br>– ni mchakato<br>– ambao Mkristo mwenye<br>– maisha yafaayo kuiga<br>– hujitoa mwenyewe |

[124] Fasili hii ni toleo lililochukuliwa la fasili ya Allen Hadidian, Successful Discipling, Moody Press: Chicago, 1979. p. 29. Kitabu hiki ni utangulizi mzuri kwa ufuasi katika kanisa la mtaa.

| |
|---|
| – kwa kipindi cha muda mrefu<br>– kwa ajili ya watu wachache<br>– ambao wameletwa kwa Kristo,<br>– lengo likiwa<br>– ni kusaidia<br>– na kuongoza<br>– ukuaji wao kuelekea ukomavu wa kiroho<br>– ili waweze kujiongeza wao wenyewe<br>– katika kizazi cha tatu cha kiroho,<br>– ambacho wanakijenga kupitia ufuasaji. |

## 4. Kuwa na Kielelezo cha Kuigwa, Kuwa Kielelezo cha Kuigwa

Maandiko huvichukulia vielelezo vya kuigwa kama kipengele muhimu cha kumwandaa mtu ili ajitegemee. Dietrich Bonheoffer, akielezea maono yake kwa Kanisa lililofanywa upya, anaandika:

> "Kanisa haliwezi kushusha thamani ya "vielelezo vya kuigwa" vya kibinadamu (vikianzishwa na Yesu na kuthaminiwa sana na Paulo!): siyo msamiati [wenyewe], bali "kielelezo cha kuigwa" hulipa neno lenyewe msisitizo na nguvu. (Kipekee, nitaandika juu ya vielelezo vya kuigwa katika Agano Jipya! Kwa kiasi takribani chote tumepoteza wazo hili!)"[125]

Petro anakubaliana na Yesu na Paulo anapotoa amri kwa wazee wa Kanisa, siyo kutawala, bali kujipatia mamlaka yao kwa vielelezo vyao. "Nawasihi wazee walio kwenu, mimi niliye mzee, mwenzi wao, na shahidi wa mateso ya Kristo, na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye; lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi" (1 Petro 5:1-3).

Mapitio bora ya mafundisho ya Agano Jipya juu ya vielelezo na uigaji yanaweza kuimarishwa kwa kukusanya marejeo yote kulingana na neno husika (angalia jedwali mwisho wa makala haya).

Kuwa kielelezo haihitaji ukamilifu, kama Lawrence O. Richards, mwanatheolojia na mwalimu wa Kimarekani anavyoelezea. Anamwelezea

[125] Dietrich Bonhoeffer. *Widerstand und Ergebung:* Breife und Aufzeichnungen aus der Haft (Munich, Germany: Chr. Kaiser, 19588) p. 262. Kwa kadri nijuavyo, Bonhoeffer hakuweza kuandika juu ya somo hili.

mtu aliye kielelezo cha kuigwa kama mfano si ulio kamilifu, bali wa makuzi (au mabadiliko).[126] Wakati Maandiko yenyewe huchukulia kuwa Wakristo waliokomaa wanapaswa kuwatumikia wengine kwa kuwa vielelezo vya kuigwa, hoja au hofu zozote kinzani huthibitika kuwa ni udhuru ambao huonekana kuwa wa kitawa zaidi kuliko Biblia yenyewe.

Katika 1 Wakoritho 4:14-16, Paulo anaeleza uhusiano wake na kanisa huko Korintho. "Siyaandiki hayo ili kuwatayaharisha; bali kuwaonya kama watoto niwapendao. Kwa kuwa ijapokuwa mna waalimu kumi elfu katika Kristo, walakini hamna baba wengi. Maana mimi ndimi niliyewazaa katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili. Basi, nawasihi mnifuate mimi." Paulo analiita kanisa 'watoto wake wapendwa', yeye mwenyewe ni baba yao. Kwa sababu yeye ni baba yao wa kiroho, anapaswa kuwaonya (mst. 14). Cha kushangaza, Paulo si tu anajitambulisha mwenyewe kwa Wakristo wengine wanaowatumikia Wakristo wa Korintho, bali pia anadai nafasi ya juu. Anajitofautisha kati yake na hawa 'wafundishaji' (Kiyunani 'paidagogos'). Msamiati huu uliwarejea watumwa waliowafundisha watoto na ni asili ya neno letu 'pedagogy' (=pedagoji). Wafundishaji hawa walihusika kwa elimu ya ufahamu ya wanafunzi wao. Paulo anasema, "hata kama mngekuwa na walimu wazuri 10,000 waliowafundisha vitu sahihi na vizuri, hilo lisingebadili ukweli, kwamba mimi ni baba yenu, kutoka kwa baba yenu mnajifunza si tu mafundisho lakini pia maisha. Na baba huhoji si tu fikra za watoto wao, bali pia matendo yao . Si tu kwamba yupo pale mambo yote yaendapo shwari, bali pia katika nyakati za dharura na hatari.

Lawrence O. Richards wakati fulani alieleza tofauti kati ya njia za kisasa za kipedagoji [ufundishaji] na zile za Biblia katika hali ambayo inaakisi mawazo ya Paulo. "Sehemu kubwa ya elimu inahusika na kuwasaidia watu kujua kile ambacho walimu wao wanajua; elimu ya Kikristo inahusika na kuwasaidia watu kuwa sawa na walimu wao walivyo."[127]

**Hapa duniani, mara zote mwanafunzi hutarajiwa kujua kile mwalimu wake anachojua, lakini kanisani mwanafunzi ni lazima aishi kama mwalimu wake anavyoishi.** Kama Lawrence O. Richards[128] anavyotukumbusha, Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Mwanafunzi hayuko juu ya mwalimu wake, lakini kila mtu ambaye amefunzwa kikamilifu atakuwa kama mwalimu wake" (Luka 6:40). "Mwanafunzi hayuko juu ya mwalimu

---

126 Lawrence O. Richards. *A Theology of Christian Education,* op.cit., p 142.

127 *Ibid.,* p. 30

128 Tazama Lawrence O. Richards. *Ibid.* Tazama pia Lawrence O. Richards*, A Theology of Church Leadership* (Grand Rapids: Zondervan, 1979), and Lawrence O. Richards, *A Theology of Personal Ministry* (Grand Rapids: Zondervan, 1981).

wake, wala mtumwa hayuko juu ya bwana wake. Yatosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake, na mtumwa kama bwana wake." (Mathayo 10:24-25). Baada ya kuwaosha miguu wanafunzi wake, anawaambia, "Kwa kuwa nimewapa kielelezo, ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende hivyo. Amin, amin nawaambia ninyi, Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake; wala yeye atumwaye si mkuu kuliko yeye aliyempeleka"(Yohana 13:15-16).

Kwa kweli tunahitaji maarifa! Basipo hayo, watu au kanisa vitashindwa kujidhibiti (Mithali 29:18), lakini ikiwa Kanisa limekufa, maarifa hayana matumizi. Je, kanisa la sasa limetelekeza kielelezo cha kuigwa? Je, si rahisi kurejea vitabu au mahubiri mazuri, kuliko mtu kuyashiriki maisha yake na wenzake kama kielelezo? Hata hivyo, ikiwa tunataka waumini wapya wakue katika Kristo na kubaki katika imani, ni lazima tuwe na mvuto katika maisha yao. Ili kufanya hilo, ni lazima sisi wenyewe tuwe na uhusiano binafsi na Kristo na tunapaswa kuishi kufuatana na sheria yake. Je, bado tunaweza kuwatia changamoto wengine kuiga mfano wetu (1 Kor. 4:16)? Je, maisha yetu ya Kikristo yanastahili kuigwa? Je, wengine wanayafahamu vya kutosha maisha yetu kiasi kwamba wanaweza kutuiga kwa kufuata mtindo wa kimaandiko?

Walimu wa theolojia wanapaswa kuwa mababa na wamama imara ambao hawaendelei kuwashirikisha wanafunzi wao maarifa, bali wapatikanao muda wote katika nyanja zote za maisha.

Si kwa bahati kitabu cha Mithali kinampa mwalimu wa hekima cheo cha "Baba" (4:1), na kumwaita mwanafunzi wake mtoto wake (13:1; 1:10, 15). Eliya na Elisha pia wanaitwa 'baba yangu' na 'watoto' wao, yaani watoto wa kiume wa manabii (2 Wafalme 20:35; 2:3, 57; 4:1, 38; 5:22; 6:1; 9:1)."[129]

Kufuasa ni muhimu kwa mafunzo ya viongozi wa kiroho na kwa wafanyakazi kanisani na katika umisheni wa kiulimwengu. Ingawa vielelezo vya Yesu na Paulo, au vya viongozi wa Agano la Kale, vinaweza visichukuliwe kikamilifu katika maisha ya sasa, hata hivyo hii bado ni njia bora ya kufundisha na kuwatengeneza viongozi wa siku zijazo.

---

[129] Hans Walter Wolff. *Anthropologie des Alten Testamentes.* Chr. Kaiser: München, 1977[3]. p. 263.

**Nani Aliye Kielelezo cha Kuigwa?**

Sehemu zote zifuatazo za Biblia hutumia neno ‘kielelezo’ (Kigriki: ‘typos’, ‘hypotyposo’) na maneno ‘mwigaji’ au ‘kuiga’ (Kigriki: ‘mimetes’, ‘mimeistai’ au ‘symmimetai’).

*1. Mungu*

Waefeso 5:1 “Hivyo mwigeni Mungu kama watoto wapendwa.”

*2. Yesu Kristo*

1 Wathesalonike 1:6, “Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana,”

1 Wakorintho 11:1, “Niigeni mimi, kama nami pia nimwigavyo Kristo.”

*3. Mitume n.k.*

Wafilipi 3:17, “**Ndugu, mwungane nami kwa kufuata kielelezo changu, na mkawatazame wale waendao kwa namna ile, kama mlivyo na sisi kama kielelezo.**”

1 Wathesalonike 1:6-7, “Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana, mkiisha kulipokea neno katika dhiki nyingi, pamoja na furaha ya Roho Mtakatifu. Hata mkawa kielelezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia, na katika Akaya.”

2 Wathesalonike 3:7, “**Kwa kuwa ninyi wenyewe mwajua jinsi iwapasavyo kutufuata sisi; kwa kuwa hatukuwa tusio na utaratibu miongoni mwenu.**”

2 Wathesalonike 3:9, **“Si kwa sababu hatuna amri, bali sisi wenyewe kujifanya kielelezo cha namna mnavyopaswa kutufuata.”**

1 Wakorintho 11:1, “**Niigeni mimi, kama nami pia nimwigavyo Kristo.**”

1 Wakorintho 4:16, “**Kwa hiyo, nawasihi ninyi, niige mimi.**”

*4. Wanaume na Wanawake katika Historia*

Waebrania 6:12, **“… ili msiwe wazito, bali waigeni wale ambao kwa njia ya imani na uvumilivu huzirithi ahadi.**”

Waebrania 13:7-(8), “**Wakumbukeni wale wanaowaongoza, ambao wamelinena neno la Mungu kwenu, fuateni imani yao, mkifikiria sana matokeo ya mwenendo wao**.”

*5. Baba zetu wa kiroho, waliotujulisha ukweli wa Biblia*

1 Wakorintho 4: (14)-16, "Kwa kuwa ijapokuwa mna walimu kumi elfu katika Kristo, walakini hamna baba wengi. Maana mimi ndimi niliyewazaa katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili. **Kwa hiyo, nawasihi ninyi, niige mimi.**"

*6. Wazee wa Kanisa*

1 Petro 5: (1)-3, "**Nawasihi wazee walio miongoni mwenu… lichungeni kundi la Mungu… si kama kuwa mabwana juu ya wale waliokabidhiwa kwenu, bali kuwa vielelezo kwa kundi.**"

*7. Vijana wa kiume walio wa kweli*

1 Timotheo 4:12, "**Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi, katika mwenendo, katika upendo, katika roho, katika imani na katika usafi.**"

*8. Makanisa mengine*

1 Wathesalonike 2:14, "**Kwa kuwa ninyi, ndugu, mkawa waigaji wa makanisa ya Mungu yaliyo katika Uyahudi, katika Kristo Yesu;**"

1 Wathesalonike 1:7, "**hivyo basi mkawa kielelezo kwa wote waaminio katika Makedonia na katika Akaya.**"

*9. Agano la Kale na watu wake*

1 Wakorintho 10:6, "**Basi, mambo haya yakawa mifano kwetu,**"

1 Wakorintho 10:11, "**Sasa, mambo haya yote yaliwatokea wao kama vielelezo, na yakaandikwa kwa kutuonya sisi,**" (Linganisha na vielelezo vya Agano la Kale katika mistari ya 1-13).

*10. Mafundisho Yafaayo*

Warumi 6:17, "**… lakini mliitii kutoka mioyo mwenu aina ile ya mafundisho ambayo mliwekwa chini yake**;"

2 Timotheo 1:13 "**Shika sana kielelezo cha maneno yafaayo yaliyo katika Kristo Yesu ambayo umeyasikia kutoka kwangu, katika imani na upendo.**"

*11. Yote yaliyo mema*

3 Yohana1:11, "**Mpenzi, usiige kile kilicho kiovu, bali kile kilicho chema.**"

Tito 2:7, "… katika mambo yote ukijionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema,"

# Wito wa Mitindo Mbadala ya Elimu kwa ajili ya Kanisa na Misheni: Hoja 21

*Zimewasilishwa katika mkutano wa Mwungano wa Wamishenari wa Kiinjili wa Ujerumani wa mwaka 1999, kama utangulizi wa majadiliano kati ya viongozi wa umisheni na wakuu wa seminari.*[130]

Kielelezo bora kabisa kilichopo kwa ajili ya maandalizi ya watumishi wa kudumu wa kanisa kinaweza kupatikana katika njia ambayo Yesu aliwafundisha wanafunzi kumi na wawili na katika maandalizi ya Paulo kwa wafanyakazi wenzake, na vilevile katika shughuli za kielimu za viongozi wa Agano la Kale. Kanuni hizi hutumika kwa aina zote za mafunzo, lakini hasa ni muhimu katika ufundishaji wa viongozi wetu wa kesho.

| Ni rahisi kuwa mchungaji; lakini siyo rahisi kuwa [mchungaji] halisi.[131] |
|---|

Tatizo la milele katika elimu ya uongozi wa kiroho ni kuwa wachungaji na wamishenari wanahitaji aina mbili ya masomo ambazo zinaonekana kutengana mbali: 1) Elimu nzuri ya taaluma ya kitheolojia na 2) vitendo katika ufundishaji wa kazi unaombatanishwa na ufuasi kwa mtu binafsi na mafunzo ya kujitegemea. Lengo la mipango hiyo linapaswa kuwa kuzalisha viongozi wa kiroho waliokomaa, wenye uzoefu wa kivitendo katika maisha halisi ya kanisa. Siku hizi, baadhi hujifunza theolojia katika kiwango cha kitaaluma pasipo kujipatia makuzi ya tabia yanayopatikana kupitia ushauri na uzoefu binafsi na pasipo mwongozo halisi wa wachungaji au wamishenari wazoefu. Wengine hupata uzoefu wa

---

130 Kwa asili ilichapwa katika Kijerumani kama „Ausbilden wie Jesus und Paulus“. pp. 7-43 in: Klaus W. Müller, Thomas Schirrmacher (Ed.). Ausbildung als missionarischer Auftrag. Referate der Jahrestagung 1999 des afem. edition afem - mission reports 7. Verlag für Kultur und Wissenschaft: Bonn, 1999; see also „Jesus as Master Educator and Trainer“. Training for Crosscultural Ministries (World Evangelical Fellowship) 2/2000: 1-4; „Paul and His Colleagues“. Training for Crosscultural Ministries (World Evangelical Fellowship) 3/2000: 6-8; „Having a Role Model, Being a Role Model“. Training for Crosscultural Ministries (World Evangelical Fellowship) 1/2001: 4-7; and Dios Quiere que Tú Aprendas Trabajes y Ames. Funad: Managua (Nikaragua), 1999[1]; 2000[2] (Spanish).

131 Imechukuliwa kutoka katika methali ya Kijerumani ‘Ni rahisi kuwa baba, lakini si rahisi kuwa [baba] halisi’.

kivitendo ndani ya maisha ya kila siku ya kanisa, lakini kamwe hawajipatii maarifa muhimu ya historia ya kanisa, vikundi vya kisasa vya kidini na dini au lugha za Biblia.

**Yesu na Paulo waliwafunza wafuasi kwa kuunganisha 1. taarifa 2. ushauri wa mtu binafsi 3. ushauri wa kundi 4. kuwafunza kuelekea kujitegemea 5. mafunzo kazini.** Je, hatuwezi kupata njia yoyote ya kuunganisha mafundisho ya juu ya kitaaluma katika theolojia na mafunzo binafsi ya mtu mmoja mmoja ndani ya mazingira ya kila siku ya misheni na ya kanisa? Hatupati mfumo uliowekwa wa mafunzo ya watumishi wa muda wote katika Biblia, ila kama ilivyo kwa kazi ya kanisa na katika misheni, tunaweza kuchunguza na kutumia kanuni zilizowekwa katika Maandiko, tukizichukua kwa hekima na kuziweka katika mazingira yetu pasipo kuacha mambo muhimu ya kiroho.

Kama ninavyoshawishika kuwa mtindo wa kisasa wa kuwazoesha watu viwango vya kibiblia na ukubali wa mahitaji ya kisasa vyote vitatuongoza kwenye matokeo yale yale, naamini kuwa hoja zifuatazo za mabadiliko hukubaliana na Maandiko na vilevile na uchambuzi wa siku hizi na zama zetu wenyewe, jamii yetu na mahitaji yake ya kielimu. Elimu iko kileleni mwa jamii ya kizazi kipya kama ilivyo kwa njia za mawasiliano ya habari. Kwa hakika, mabadiliko moja kwa moja si jambo zuri, lakini twaweza kutumia mengi ya maendeleo haya mapya kwa faida yetu. Hatuwezi kuruhusu kukosa fursa hizi kama ulimwengu wa elimu ya kisekyula katika Ujerumani ufanyavyo.

| **Sababu Tatu za Ulazima wa Mabadiliko katika Programu Zetu za Elimu ya Theolojia** |
|---|
| *1. Utambuzi wa kibiblia:*<br>Mifano itolewayo na Yesu Kristo na Paulo,<br>umuhimu wa vielelezo vya kuigwa,<br>amri ya misheni,<br>mahitaji ya kiroho ya uongozi. |
| *2. Mabadiliko katika elimu ya sasa*[132]*:*<br>mabadiliko ya daima na ongezeko katika mambo yanayopaswa kujifunza,<br>utandawazi,<br>hitaji la daima la elimu ya juu,[133]<br>umuhimu wa kufuasa,<br>kozi kwa njia ya elimu masafa,<br>tovuti,<br>Umuhimu wa VH=Viwango Hisi),<br>Andragoji badala ya Pedagoji.[134] |
| *3. Uzoefu wa kimataifa kwenye nyanja ya misheni, hususani katika Ulimwengu wa Tatu*[135]*:*<br>(ETE) Elimu ya Theolojia kwa njia Enezi[136] |

---

132 Kwa mfano tazama; Wolf Lodermann. „Management-Gurus aus USA in Europa auf Studenten Jagd: MBA-Titel als Sprosse auf Karriereleiter“. Bonner Rundschau 7. Sept.1996; Bärbel Schwertfeger. „International, praxisnah und teamorientiert: Der MBA setzt sich auch in Deutschland durch“. Welt am Sonntag vom 7.Oct. 1997.

133 Tazama; Detlef Joszok. „Lernen als Beruf: Arbeit und Bildung in der Informations- und Wissensgesellschaft“. Aus Politik und Zeitgeschichte (Beilage zu Das Parlament) B 9/99 (26. Feb.1999): 31-38.

134 Tazama; hapo chini.

135 Kwa mfano tazama; F. Ross. Kinsler (Ed.). Ministry by the People. WCC Publ.: Genf & Orbis Books: Myrknoll (NY), 1983; Harvie M. Conn, Samuel F. Rowen (Ed.). Missions and Theological Education. Associates of Urbans: Farmington (MI), 1984; Tom Chandler. „A Caring Model of Training“. Training for Crosscultural Ministries (Occasional Bulletin of the International Missionary Training Fellowship) 1/1996: 4-5 (on India); David & Rosemary Harley. „Missionary Training in Africa is Gaining Momentum“. Training for Crosscultural Ministries (Occasional Bulletin of the International Missionary Training Fellowship) 2/1994: 3-4; Heinz Suter. „Training Tentmakers from the Latin Context“. Training for Crosscultural Ministries (Occasional Bulletin of the International Missionary Training Fellowship) 1/1996: 5-6 (on Latin America).

na mitindo mingine mbadala ya mafunzo,[137]
mitindo ya mafunzo katika tamaduni nyingine,[138]
ongezeko la idadi ya waombaji wenye umri mkubwa kwa ajili ya huduma ya muda wote,
Huduma ya Mwanachama,
mafunzo ya watumishi katika makanisa makubwa.

Siegfried Buchholz, kwenye mkutano kwa ajili ya viongozi wa Kikristo alisema:

> "Fursa ya pili ambayo tusingethubutu kuikosa ni namna tunavyochukulia elimu na mafunzo. Tunapaswa kuchukulia kuwa elimu itakuwa malighafi muhimu zaidi katika karne ijayo. Mfumo wetu wa elimu wa sasa hauwaandai vijana kwa ajili ya siku zijazo, kwa sababu unashindwa kufahamu mahitaji ya biashara na viwanda. Shule zinatumika tu kusambaza aina za maarifa ambayo yanaweza kufundishwa na mtu kujifunza katika muundo wa kimapokeo, na kuchukulia kuwa wanafunzi watadumu kwa maisha yao yote katika utaalamu wa kimapokeo, ambao tayari haupo. Zaidi ya stadi na maarifa yanayohitajika na ajira maalumu, wanafunzi wanapaswa kujifunza stadi za kujiajiri, yaani utayari na uwezo wa kukabiliana na ulimwengu wenye mabadiliko ya daima ya wasifu wa kazi na taaluma, ili kuweza

---

136 Tazama 'seminari mama' ya TEE [Kisw: ETE], seminari ya Kimatengenezo huko Guatemala: Kenneth B. Mulholland. „Presbyterian Seminary of Guatemala: A Modest Experiment Becomes a Model for Change". pp. 33-41 in: F. Ross. Kinsler (Ed.). Ministry by the People. op. cit. On TEE, tazama ufupisho katika: Fred Holland. Teaching Through T. E. E.: Help for Leaders in Theological Education by Extension in Africa. Evangel Publishing House: Nairobi (Kenia), 1975 and Richard Hart. „New Paths in Theological Education". PTEE info (Program for Theological Education by Extension, Amman, Jordanien) 1/1998. p. 1; „Experiencing the Aspect of 'Extension'„. PTEE info (Program for Theological Education by Extension, Amman, Jordanien) 1/1995. p. 1.

137 Tazama maelezo ya mitindo mbadala kwa ajili ya elimu ya kitheolojia katika; David Kornfield. „Seminary Education Toward Education Alternatives". pp. 191-210 in: Harvie M. Conn, Samuel F. Rowen (Ed.). Missions and Theological Education. op. cit.

138 Tazama: Harvie M. Conn. „Teaching Missions in the Third World: The Cultural Problems". pp. 249-279 in: Harvie M. Conn, Samuel F. Rowen (Ed.). Missions and Theological Education. Associates of Urbans: Farmington (MI), 1984. pp. 268ff „ethnoandragogy".

kurukia ndani ya boti ambazo zinaondoka bandarini. Na hatujifunzi hili katika mfumo wetu wa sasa wa elimu."[139]

Uunganishaji wa taarifa, ushauri wa mtu binafsi na wa kundi na juu ya mafunzo kazini – kielelezo kilichotolewa na Yesu na Paulo – kwa maoni yangu ni njia pekee ya kuwasaidia Wakristo wa sasa kukuza majukumu ya sifa za uongozi wa kibiblia (1 Tim. 3: 1-13; Tito 1: 5-9) ili waweze kuwa na sifa ya kuchukua majukumu ya maisha ya kanisa na [yale ya] nyanja ya umisheni. Moja ya sifa iliyosisitizwa kwenye Biblia, ambayo ni uwezo wa kuhubiri, hujumuisha maarifa na uwezo wa kushirikisha uwezo huo. Elimu ya Theolojia hujifanya kutojali sifa nyingine (mfano, kuwa na kiasi, kukomaa kupitia majaribu, maisha ya familia yaliyo mfano), kwa kuwa seminari hushindwa kutoa ama ushauri au mafunzo ya kivitendo ya ushirikiano kwa kutumia walimu katika maisha ya kila siku ya Kanisa.

Detlef Lehmann hutarajia yafuatayo kutoka kwenye mafunzo mazuri ya kitheolojia: Mchungaji au mmishenari wa siku zijazo anapaswa:

1) afundishwe kufundisha (si tu kujua mafundisho, bali kujua namna ya kuyashirikisha),
2) aoneshe mtindo wa maisha ulio wa mfano,
3) aweke kipaumbele kikuu katika ibada na maombi.[140]

Hivyo, mafunzo ya kitheolojia yanapaswa kuundwa [ili] kuchochea kujitegemea, na hayana budi kuhusisha ushauri na vitendo vya kushirikiana katika kazi za kanisa pamoja na vitendea kazi bora vya kitheolojia, ili Wakristo waandaliwe kuusambaza Ufalme wa Mungu kwa ushirikiano na wengine.[141]

---

139 Siegfried Buchholz. „Fit für die Zukunft - Aufspringen auf einen fahrenden Zug". pp. 7-20 in: Jörg Knoblauch, Horst Marquart (ed.). Fit für die Zukunft: Konzepte christlicher Führungskräfte. Brunnen: Gießen, 1999. pp. 13-14.

140 Detlef Lehmann. „Gedanken und Überlegungen zur Frage der Ausbildung von Pastoren in den lutherischen Kirchen". Evangelium - Gospel 10 [= 21] (1983) 3 (June-Aug): 382-399.

141 Tazama: Wolfgang Simson. Gottes Megatrends: Sechs Wege aus dem christlichen Ghetto. C & P: Emmelsbüll & Koinonia: Rothrist (CH), 1995. pp. 49-51.

**Isiwe Hivi:**

Mwanafalsafa alijipatia mkate [riziki] wake
kwa kutumia tasnifu yake,

[basi] maisha humaanisha kifo.

Mpinzani wake, aliyefundisha

mawazo kinzani

pia aliheshimiwa na kulishwa vema.[142]

Changamoto tunayokabiliana nayo kutokana na mabadiliko katika elimu yako wazi. Huko nyuma miaka ya 70, Milton Baker wa Ushirika wa Kiinjili wa Misheni (Evangelical Fellowship of Missions – EFMA) aliandika:

> "Hatufundishi viongozi wa kutosha. 2. Hatufundishi viongozi halisi. 3. Gharama za mafunzo ziko juu sana. 4. Ufundishaji wa kimapokeo katika shule za bweni huwatenga viongozi wategemewa, hivyo wanakuwa wataalamu. 5. Tunawafundisha watu katika dhana zisizo halisia."[143]

Tunawezaje kuyashinda mapungufu haya? Ngoja nilete hoja chache. [Hoja] hizi zaweza kuwa si kamilifu,[144] lakini natumaini kuwa angalau zitachochea majadiliano tunayoyahitaji juu ya maendeleo zaidi ya programu zetu za mafunzo kwa ajili ya wamishenari na wachungaji.

Sitaki kuibua mkanganyiko usio wa lazima, kwa vile hatujaja kwenye mkutano huu kutukuzana sisi wenyewe, bali kupambana kwa nia njema

---

142 Tafsiri na Cambron Teupe katika mtindo wa kishairi wa Kijerumani.

143 Imenukuliwa katika Fred Holland. Teaching Through T. E. E.: Help for Leaders in Theological Education by Extension in Africa. Evangel Publishing House: Nairobi (Kenia), 1975. p. 9.

144 Kwa mapendekezo zaidi sawa na hayo, tazama: Paul A. Beals. A People for His Name: A Church-Based Missions Strategy. William Carey Library: Pasadena (CA), 1995². pp. 199-206 (für instructors) und pp. 207-214 (for students). Nimeshajipatia mapendekezo mengi kutoka the World Evangelical Fellowship's (WEF) International Missionary Training Fellowship (Journal: Training for Crosscultural Ministries: Occasional Bulletin of the International Missionary Training Fellowship): Robert Ferris (Ed.). Establishing Missionary Training. World Evangelical Fellowship Series 4. William Carey Library: Pasadena (CA), 1995; David Harley. Preparing to Serve: Training for Cross-Cultural Mission. World Evangelical Fellowship Series 3. William Carey Library: Pasadena (CA), 1995; William D. Taylor (Ed.). Internationalizing Missionary Training. Paternoster Press: Carlisle (GB), n.d.(ca. 1994).

kwa ajili ya kuueneza Ufalme wa Mungu, na kujali mawazo mapya kutoka kwa watu wengine na misheni nyingine.

**1. Lengo la Elimu ni kumsaidia mtu aweze kujitegemea, siyo kumfanya tegemezi wa mtu aliye kielelezo kwa maisha yake yote.**

Jambo hili humaanisha kuwa mwanafunzi huhitaji kujua *jinsi* mwalimu wake alivyofika kwenye mahitimisho, kwa kiwango kile kile sawa na kujua mahitimisho yenyewe. Mtumishi huwasiliana na walimu wake wakati anapokabiliana na matatizo katika maisha ya kila siku. Anapaswa kuwa na uwezo wa kutafuta majibu yake mwenyewe. Kwa hiyo elimu inapaswa kumfundisha mwanafunzi kujifunza, hata pasipo mwalimu, kama Warumi wa zamani walivyosema: “non scholae, sed vitae discimus” – “Hatujifunzi kwa ajili ya shule bali kwa ajili ya maisha.” Kwa mfano, seminari hufundisha madarasa kwa kuzingatia vikundi vya kidini vya zamani lakini kwa sababu ya mabadiliko ya haraka katika vikundi vingi, na kuibuka kwa daima kwa vikundi vipya, kwa makusudi wanafunzi wanahitaji kujua jinsi ya kuchanganua mafundisho na vitendo vya makundi mapya, ili waweze kuwaonya vema washiriki wa makanisa na kuwasaidia katika ushuhudiaji kwa makundi ya aina hiyo.

**2. Elimu ya Theolojia ni lazima itunze mtazamo wa malengo yake, kama Yesu alivyowafundisha wanafunzi wake akiwa na Agizo Kuu akilini mwake.**

Jonathan Lewis[145] anaainisha malengo ya elimu ya theolojia katika maeneo matatu; “matokeo ya uelewa,” (maarifa) “matokeo ya stadi” na “matokeo ya kimhemko” (kihisia).[146] Kwa sababu seminari huruhusu jamii kuweka malengo yao badala ya Maandiko, programu nyingi za mafunzo hushindwa kutoa zaidi kuliko mojawapo ya maeneo haya.[147] “Ili kuwa na ufanisi, programu za mafunzo ya huduma zahitaji kulenga kwenye dhumuni la kweli la mafunzo – [yaani] watenda kazi wa ufalme watauwa na wafaao”.[148]

---

145 Jonathan Lewis. „Matching Outcomes with Methods and Contexts“. Training for Crosscultural Ministries (Occasional Bulletin of the International Missionary Training Fellowship) 2/1998: 1-3.

146 Ibid., p. 1.

147 Ibid., p. 1.

148 Ibid., p. 3.

**3. Maarifa, uzoefu na ukomavu wa mwalimu na wanafunzi vyote vina umuhimu unaolingana.[149] KA cha kitheolojia hakitoshi pasipo KH[150] cha kitheolojia.[151]**

Nadharia na vitendo, KA na KH vyote vinapaswa kusisitizwa. Seminari hazitawatia moyo wanafunzi wao kujifunza vema na kwa utashi kwa kuwapa fursa za kushirikiana katika mikutano mbalimbali ya kiinjili kama gharama ya ubora wa kitaaluma, wala kwa kuwategemea kuwa mahiri wa mambo maalumu pasipo kuwapa fursa [za] kupata uzoefu wa kivitendo.

Kwa sababu wanafunzi huhitaji mwongozo mkubwa katika maisha yao binafsi kama ilivyo katika makuzi ya kiakili, vipengele vitano muhimu kwa Yesu na kwa Paulo vinapaswa kusokotwa pamoja katika programu nzima ya mafunzo: 1. taarifa, 2. ushauri wa mtu binafsi, 3. ushauri wa kundi, 4. kupandishwa hadhi ya kujitegemea, 5. mafunzo kazini.

**4. Elimu inapaswa kuwekwa katika maisha, siyo maisha kuwekwa kwenye elimu. Kwa kuwa hali ya mwanafunzi ina athari kubwa juu ya uwezo wake wa kujifunza, mafunzo ya kitheolojia hayawezi kuwa yenye kubadilikabadilika sana.**

Tunapaswa kuachana na matakwa kuwa mwanafunzi anapaswa kujiasilisha kikamilifu na kwa namna ya kipekee kwa seminari yake. Vituo vya mafunzo havina budi pia kuikubali hali ya mwanafunzi. Njia ya kuelekea sehemu moja mahali pake hapana budi kuchukuliwa na toa na pokea.

**5. Elimu ya Theolojia ya sasa ni lazima itoe na ijumuishe njia mbalimbali mbadala na za kimapokeo.**

Mafunzo ya theolojia huhitaji mabadiliko kuliko nyanja nyingine, kwa sababu ni lazima yajali uanuai ambao Mungu ameubuni kwa ajili ya

---

149 Hususani katika: Paul A. Beals. A People for His Name. op. cit., pp. 210-212.

150 Kiwango Akili.

151 Kiwango Hisi, au ‘akili za hisia’. Tazama; Daniel Goleman. Emotionale Intelligenz. Hanser: München, 1996 = dtv: München, 1997 [I do not shard Goleman’s Buddistic tendencies! Tazama; Daniel Goleman (Ed.). Die heilende Kraft der Gefühle: Gespräche mit dem Dalai Lama ... dtv: München, 1998[2]]; Robert K. Cooper, Ayman Sawaf. Emotionale Intelligenz für Manager. Heyne: München, 1997; Branko Bokun. Wer lacht lebt. Ariston: München, 1996; Andreas Huber. Sichwort Emotionale Intelligenz. Heyne: München, 1996[4]. Mnamo mwaka 1962, Ciba-Symposium [Mkutano wa Ciba] juu ya siku za usoni za mwanadamu, ulijadili msisitizo upitao kiwango wa KA na umuhimu wa uwezo wa mtu binafsi kushughulika na wengine. Tazama: Gordon Wolstenhom (Ed.). Man and His Future. J. & A. Churchill: London, 1963.

Ufalme wake. Inasikitisha kiasi gani kuwa mafunzo ya theolojia ya Kiinjili katika Ujerumani ni yale yasiyopokea mabadiliko zaidi kuliko programu za kidunia zilizochunguzwa katika tafiti za elimu.

Ulimwengu wetu wa leo umetupatia lundo la njia. Mbali na mihadhara, vitabu vya kiada na ufundishaji wa darasani, twaweza kutumia kozi za elimu ya masafa, kujifunza binafsi, mafunzo ya vitendo, kufuasa, kozi za moduli, kozi za mtandao, kozi zinazosimamiwa na mkufunzi, utafiti, vikundi vya majadiliano – si kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili ya wanafunzi wetu.

Mkanganyiko uliopo juu ya programu bora ya elimu unachukuliwa katika mazingira yasiyo na siha kabisa ambamo njia mbadala na za kimapokeo zimekuwa zikigonganishwa kila moja na nyenzake. Sisi Wakristo tunapaswa kwa kina, kwa furaha na katika hali ya mabadiliko kujinufaisha na njia zote zilizopo, ili kuwaendeleza wanafunzi wetu na jukumu lao katika Ufalme wa Mungu.

**6. Wanafunzi wa theolojia ni watu wazima na hawapaswi kufundishwa kwa kufuata kanuni zilezile kama watoto wa shule katika miaka ishirini ya mwanzo ya maisha [yao]. Walimu ni lazima waheshimu ukomavu wao. Watu wazima hujifunza kwa namna tofauti kuliko watoto wanavyofanya.**[152]

Walimu wamezoea kuhamishia dhana nyingi sana za ufundishaji (‘pedagoji’, ‘kumwongoza mtoto’ hutokana na neno la Kigriki ‘pais’) kwenye nyanja ya androji (kutoka neno ‘andros’, ‘mtu mzima’). Maandiko mapya hutoa nuru ya kutosha katika mahitaji ya wanafunzi walio watu wazima.

Mafunzo hayawezi tena kutawaliwa na mihadhara na maelekezo ya darasani, ambayo hata hivyo hutoa 20% tu ya maarifa![153] Ni vitabu vingapi vya Biblia vinavyoweza kufundishwa darasani katika miaka minne?

**7. Aina ya kujifunza kwa mwanafunzi ni lazima izingatiwe kadri iwezekanavyo. Tunamtaka *ajifunze* vilevile kwa kina kadiri inavyowezekana, siyo tu kutimiza matakwa yetu ya kitaasisi.**

---

152 Tazama: Duane H. Elmer. „Education and Service“. pp. 226-244 in: Harvie M. Conn, Samuel F. Rowen (Ed). Missions and Theological Education. Associates of Urbans: Farmington (MI), 1984. pp. 227-229 („Paedagogy and Andragogy“) und Harvie M. Conn. „Teaching Missions in the Third World“. op. cit., pp. 268ff „eth-noandragogy“.

153 Aniul D. Dolanky. „A Critical Evaluation of Theological Education in Residential Training“. pp. 156-168 in: Harvie M. Conn, Samuel F. Rowen (Ed.). Missions and Theological Education. op. cit., p. 157.

Mungu ameumba aina nyingi mbalimbali za watu na aina nyingi mbalimbali za Wakristo. Iwapo Mungu huumba watoto wake na huduma maalumu akilini mwao, ni kwa namna gani taasisi za kitheolojia zaweza kuwalazimisha katika sheria kali za kielimu? Waalimu wengi wa theolojia wanaonekana kutojua kabisa mambo mapya yenye mashiko kwenye nyanja za elimu ya watu wazima na saikolojia ya kujifunza.

**8. Aina ya kujifunza kwa mwanafunzi na vipawa vyake binafsi ni lazima vizingatiwe.**

Je, [kifungu cha] 1 Petro 4:10 (**Kama kila mtu alivyopokea karama, *hivyo basi* hudumianeni ninyi kwa ninyi, kama mawakili wema wa neema ya Mungu iliyofunuliwa.**) hakina uhalali katika mafunzo ya kitheolojia? Ikiwa tunataka kuwaandaa watu kutumia vipawa vyao kwa maisha yao yote kwa ajili ya kuuendeleza Ufalme wa Mungu, basi vipawa hivyo ni lazima vishiriki jukumu la kimsingi katika mafunzo ya mwanafunzi.

Kwa kuwa vipawa tofauti vya kiroho moja kwa moja huathiri aina ya kujifunza kwa mwanafunzi na mapendeleo yake, programu ya mafunzo haina budi kujumuisha mambo muhimu ya msingi na fursa za kubobea katia utaalamu maalumu. Ni vipawa vichache tu vya kiroho vinavyoweza kuendelezwa katika nyanja za theolojia ya kimapokeo, ambazo hutoa fursa chache kwa mwanafunzi kukuza vipawa vyake binafsi.

**9. Walimu ni lazima wawe watendaji hai kama wachungaji, wamishenari au wajihusishe katika huduma nyingine na vilevile wawe walimu na wasomi.**

Walimu wengi katika seminari za Ujerumani wana uzoefu mdogo katika huduma hai, kama sio wote, lakini bado wanaandaa wanafunzi kwa ajili ya utaalamu ambao wao wenyewe wana uzoefu mdogo au hawana kabisa. Ingawa twapenda kukosoa mafunzo ya theolojia katika makanisa ya Serikali, tumekuwa tukiyaiga katika mtazamo huu. Walimu wanapaswa kuwa wamefuzu kitaaluma na wametoa mchango katika taaluma, lakini pia bado wanapaswa kuwa hai moja kwa moja au kwa muda katika maisha ya kanisa na umisheni. Profesa wa upasuaji hawezi kufundisha kwa ufanisi iwapo alifanya upasuaji wake wa mwisho miaka kumi na saba iliyopita! Wanafunzi wake humtarajia awe mwenye kwenda na wakati na maendeleo mapya na aweze kurejea uzoefu wa hivi karibuni katika chumba cha upasuaji. Mafunzo ya kitaaluma na uzoefu wa kivitendo unaondelea vyote pia ni muhimu kwa elimu ya theolojia.

**10. Kwa kuwa maisha binafsi ya mwalimu ni muhimu sawa na uwezo wake wa kiakili, seminari zinapaswa kuzingatia zaidi ya mitazamo ya kitaaluma, kiakili au 'wa macho' katika kuchagua vitivo vyao.**

Sifa muhimu zaidi ya mwalimu inapaswa kuwa uwezo wake wa kuwa kielelezo chema kwa wanafunzi wake, na kufanya kazi pamoja nao kwa vitendo. Vipawa vyake vinapaswa kuwa na mchango muhimu sawa na nafasi yake katika familia, kanisa, misheni au jamii.

Hapana budi pia kuwe na uwezekano wa kuwashirikisha walimu wasio na sifa rasmi za kitaaluma kufundisha madarasa kwenye masomo ambayo wana ufahamu au uzoefu maalumu. Kwa mfano, Rabi Maharaj, kama kuhani wa zamani wa Kihindu, anastahili zaidi kufundisha juu ya Uhindu kuliko mwalimu ambaye amejifunza tu kitaaluma. Je, tungemwajiri Paulo tu na kutupilia mbali mchango binafsi wa Yohana?

**11. Seminari ni lazima ziwapatie wanafunzi mahusiano ya karibu na walimu nje ya darasa na fursa zilizopangwa za ushauri wa mara kwa mara juu ya matatizo ya kitheolojia, kikanisa na yale binafsi kama sehemu ya kozi.**

Walimu ambao ni lazima watumie muda mwingi nje ya chuo au ambao hawawezi kupatikana siku za mwisho wa wiki walau ni lazima wachukue wanafunzi wachache, ili waweze kutazama na kujifunza kutoka kwenye maisha halisi.

**12. Zaidi ya yote wanafunzi ni lazima wajifunze kukabili msongo wa mawazo na majukumu ya kanisa na mahali pa misheni. Uwezo wa kushughulikia mtihani wa msongo kimsingi siyo muhimu sana!**

Mtihani mmoja mwishomi mwa wakati wa mafunzo hueleza zaidi juu ya uwezo wa kukabili mitihani kuliko juu ya maarifa. Tungeweza kugundua zaidi juu ya maarifa ya mwanafunzi na uwezo wake wa kuyatumia kwa kuchukua mtazamo mpana katika mafanikio yake ya kitheolojia na kivitendo kwa wakati wote.

Yawezekana kila mwanafunzi aweza kusimamiwa na mkufunzi binafsi kwa wakati wote wa mafunzo. Mwalimu huyu kisha aweza kutathmini maendeleo na mafanikio yote ya mwanafunzi, ikijumuisha ukuaji wake binafsi, ushiriki wake kwenye kanisa la mtaa na maswali. Kisha upimwaji wake waweza kujadiliwa na kutathminiwa na wengine ambao wameshiriki katika mafunzo ya mwanafunzi.

**13. Mbali na wingi wa waalimu maalumu katika fani zao, kila mwanafunzi ni lazima awe na mkufunzi wake binafsi. "Uangalizi wa**

**roho" ulio endelevu na ushauri wa mara kwa mara unapaswa kuwa matendo ya kawaida katika elimu ya theolojia.**

Kwa kweli, jambo hili humaanisha wanafunzi wachache, si kwa seminari kama taasisi, bali kwa mwalimu binafsi. Kupunguza idadi ya wanafunzi pekee moja kwa moja haitafikia lengo hili, ambalo hutegemea uwezo wa mwalimu kuwajumuisha wanafuzi katika kazi na maisha yake mwenyewe.

**14. Mwingiliano na ufanyaji kazi kama timu wa walimu na wanafunzi kanisani unapaswa kuwa utaratibu rasmi, hasa kwa kuwa wanafunzi wetu baadaye watachukua majukumu ya uongozi. Uvumilivu na kujitoa dhabihu hakuwezi kufunzwa katika mipango ya muda mfupi bali katika majukumu endelevu tu.**

Uzoefu wa kivitendo unaopatikana katika shughuli za muda mfupi kama vile kazi za nje ya masomo, safari za kimisheni za majira ya joto ndani au nje ya nchi zina thamani yake, lakini kinyume na utaalamu wa siku zijazo, mwisho wa miradi ya muda mfupi unaonekana. Matatizo ambayo hayakutatuliwa yanaweza kuachwa. Baadaye, wakati mwanafunzi awapo amechukua kazi ya muda wote, ni lazima akabiliane na matatizo na kisha kubeba wajibu wa mambo ambayo angependa kuyarekebisha. Kamwe hawezi kukwepa wapinzani wa daima, wala mkanganyiko wa kitheolojia, wala mchakato wa muda mrefu wa kufikia makubaliano kwenye bodi ya wazee washindani.

**15. Mafunzo hayapaswi kupatikana kwa vijana tu. Twahitaji programu ambazo zitawawezesha waumini wazee na wafanyakazi wa kanisa wenye uzoefu kupata elimu nzuri ya theolojia pasipo kuhitajika kuondoka kwenye kazi na familia zao.**[154]

Katika ongezeko la jamii yetu isiyo ya kikanisa, kuna vijana wachache sana watokao kwenye misingi ya Kikristo waanzao seminari mapema baada ya kumaliza shule, lakini Biblia haiweki mpaka wa umri katika kuanza huduma ya muda wote. Kwa nini mtu ambaye amekuwa Mkristo kwa miaka mitano asianze mafunzo ya theolojia katika umri wa miaka 50, kwa kuchukulia kuwa ni mtu aliyekomaa binafsi na kiroho?

Hofu kwamba vijana wadogo waliopata nafasi zao katika maisha ya kitaaluma hawatavutwa na huduma ya muda wote imesababisha "mafundisho" kuwa mchungaji au mmishenari wa 'kawaida' hana budi kupatwa mwanzoni mwa kazi zao. Wakati mtu wa umri wa kati – kama

---

[154] Tazama: Thomas Schirrmacher. „Aus meiner Sicht: Mission und Bewährung". *Evangelikale Missiologie* 1/1989: 2.

mtume Paulo – aingiapo kwenye huduma, sote tunashangaa. Lakini je, Paulo halionyi kanisa dhidi ya kutoa majukumu mengi kwa "… mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi" (1 Tim. 3:6)? Je, haya si malalamiko ya mara kwa mara mahali pa misheni, ambapo wachungaji au wamishenari vijana hudharau uzoefu wa Wakristo wenyeji waliokomaa? Siku hizi twahitaji sana watumishi waliothibitishwa wenye ukomavu binafsi na uzoefu wa kutosha kanisani na katika misheni [ili] kukabili migogoro mbalimbali kwa hekima na umakini.

**16. Elimu ya theolojia katika yote yaliyomo na katika njia zake, haina budi kutoa mtazamo mpana wa Kikristo kuhusu ulimwengu.**[155]

Imani katika Yesu Kristo yapaswa kujumuisha nyanja zote za maisha yetu. Ikiwa Yesu, ambaye katika yeye na kupitia yeye ulimwengu uliumbwa, ni Bwana wake, basi hakuna kinachoweza kukwepa athari yake. Mtazamo mpana hauna maana kwamba tunajiondoa kwenye mnara wa dhahabu wa somo finyu la utawa, bali kwamba upanuzi wote wa mawazo na maisha yetu unapata kuhusishwa katika mafunzo ya kitheolojia na kuwekwa chini ya imani yetu katika Kristo.

Hatuwezi kutupilia mbali wala hata kukataa taaluma zisizo za kitheolojia, kama vile ufundishaji, saikolojia au historia, wala kumeza bila kuhakiki chochote wengine wasemacho. Wanafunzi wetu hawana budi kujifunza kutathmini! Kadri athari ya mwalimu iamuavyo kwa kiasi kikubwa jinsi wanafunzi wake washughulikavyo na kiwango kingi cha taarifa zinazowakabili, ni lazima awe macho na jukumu lake kama kielelezo.

**17. Wakristo wa Magharibi wana mambo mengi ya kujifunza kutoka kwa Wakristo katika nchi nyingine.**

Kadri utandawazi wetu unavyoifunika dunia yetu, walimu na wanafunzi wanapaswa kujifunza zaidi kutoka kwa Wakristo wa tamaduni nyingine. Kuishi na kufanya kazi katika utamaduni mwingine, hata kwa muda mfupi, kumewachochea vijana wengi – hata kama ni kutambua tu athari za utamaduni wao kwenye mtindo wa maisha ya Kikristo. Wakati uleule, wengi wamevutiwa na misheni – hata kama hawawi wamishenari hapo baadaye, wanaweza kuhakikisha kuwa misheni itakuwa sehemu muhimu ya ufahamu wao wa Kanisa.

Wanatheolojia wa Ujerumani – si tu waliberali, hata hivyo – wanaweza kujichukulia wenyewe kama kitovu cha ulimwengu, lakini katika utawala

155 Hususani, Paul A. Beals. *A People for His Name*. op. cit, pp. 199-200.

wa elimu, tuna mambo mengi ya kujifunza kutoka tamaduni nyingine.[156] Ninavutiwa sana na namna waumini wa Asia walivyounganisha kiwango cha juu cha kitaaluma na hamasa kubwa ya kiroho. Kwa mfano, Lesslie Newbigin anapendekeza kuwa programu za mafunzo za Kimagharibi zinapaswa kurekebishwa upya kimuundo, katika njia na katika yaliyomo, kulingana na uzoefu uliofanywa katika tamaduni zingine.[157]

**18. Utenganishwaji usiokubali mabadiliko katika taaluma husababisha unadharia uvukao mpaka na uchaguaji fani maalumu upitao mpaka.[158] Ni moja ya majukumu makubwa ya elimu kuimarisha na kupendekeza uhusiano baina ya mambo ya maarifa; lakini katika theolojia, jambo hili kwa ujumla limeachwa kwa mwanafunzi.**

Ni kwa haraka namna gani walimu hufanya madarasa yao kitovu cha ulimwengu, kuwapima wanafunzi kwa mujibu wa mafanikio yao katika fani zao wenyewe na kutupilia mbali kabisa maendeleo yake mengine. Paulo A. Beals, anayeuita upofu huu “ushamba wa kielimu”,[159] hauwezi hata kuepusha fasili–chimbuzi na majukumu yake ya kutumikia kanisa na umisheni,[160] ingawa seminari za Kiinjili mara nyingi huheshimu fani hii kama aina ya ng’ombe mtakatifu asiyehitaji kuhesabiwa haki. Fasili–chimbuzi haihitaji tu kuwa chini ya Uhakiki wa Kibiblia, lakini pia ni lazima ijiweke chini ya tamko la Kibiblia kuwa Maandiko yote “**ni yenye faida kwa mafundisho**”, (2 Tim. 3:16). Kama fasili–chimbuzi ilivyo muhimu, ni lazima ichangie kwenye mahitaji ya kanisa.

Mnamo mwaka 1787, Johann Philipp Gabler alidai kuwa “Theolojia ya Kibiblia” inapaswa kutengwa kutoka kwenye “Theolojia ya Kidogmatiki”.[161] Tangu hapo, Kanisa limepata shida kutokana na

---

156 Kwa uchaguzi mzuri wa mitindo mbadala, ikijumuisha nchi nyingine, tazama: For an Robert W. Ferris. *Renewal in Theological Education*. Billy Graham Center: Wheaton (IL), 1990.

157 Lesslie Newbigin. „Theological Education in World Perspective“. pp. 3-18 in: Harvie M. Conn, Samuel F. Rowen (Ed.). Missions and Theological Education. Associates of Urbans: Farmington (MI), 1984.

158 Hususani John M. Frame. *The Doctrine of the Knowledge of God*. op. cit., pp. 206-214.

159 „Educational Provincialism“, Paul A. Beals. *A People for His Name*. op. cit., p.. 200.

160 *Ibid*. p. 201-202.

161 Johann Philipp Gabler. De iusto discrimine theologiae biblicae et dogmaticae regundisque recte utriusque finibus. Inauguralrede an der Universität Altdorf. Altdorf, 1787; on Gabler, tazama: Otto Merk. „Anfänge neutestamentlicher Wissen-

ukengeuko unaongezeka kati ya uwasilishi wa ukweli wa 'Kikristo' na fasili–chimbuzi ya Maandiko. Uhakiki–kinzani wa Kihistoria wa sasa usingeimarishwa pasipo hili! Vyuo vya Biblia vya Kiinjili mara nyingi vilianzishwa ili kupambana na seminari kinzani, lakini bila kutarajia mara nyingi vimechukua taaluma zao, miundo yao na mipaka yao, bila kujua vikihifadhi matokeo kinzani asilia badala ya kuyapindua.

Mara nyingi matokeo ya kushangaza zaidi ya Uhakiki–kinzani wa Kihistoria hutunzwa badala ya kuanzisha mapinduzi yanayosisitiza fasili ya Neno la Mungu na kudhihirisha ushiriki wake katika Theolojia Pangilivu, udogmatiki, maadili na utetezi wa imani na vilevile katika ushauri na umisheni wote kwa wakati mmoja.

John M. Frame anapinga kwa nguvu mtazamo wa kifalsafa unaotawala kuwa uainishaji wa taaluma za maarifa na za kisayansi ni muhimu kwa usomi.[162] Huchukulia mpangilio huu kama suala la dharura, na huwapinga wasomi wa Matengenezo ya Kiholanzi, ambao kwa namna nyingine anawahusudu sana: Abraham Kuyper na Herman Dooyeweerd, ambao walifundisha kwamba mgawanyo wa taaluma na uainishaji sahihi ni muhimu kwa uelewa halisi wa ulimwengu.

## 19. Misheni zinapaswa kuwa kitovu kwa ajili ya mtaala. Nyanja zote za elimu ya kitheolojia hazina budi kuelekezwa kwenye upandaji wa makanisa na umisheni wa kiulimwengu.[163]

---

schaft im 18. Jahrhundert". pp. 37-59 katika: Georg Schwaiger (Ed.). Historische Kritik in der Theologie. Studien zur Theologie - und Geistesgeschichte des Neunzehnten Jahrhunderts 32. Vandenhoeck & Ruprecht, 1980, hapa ni uk. 57. Theolojia ya Kilutheri ilifungua njia kwa maendeleo haya. Kwa mujibu wa Robert Scharlemann. "Theology in Church and University: The Post-Reformation Development". Church History 33 (1964) 23ff, Melanchthon alitofautisha kati ya theolojia ya kitaaluma, ambayo hujipatia msimamo wake katika maendeleo ya kihistoria, na theolojia ya kipawa, ambayo inahubiri katika kanisa la sasa; tofauti ambayo wanatheolojia wa Kilutherani wa kiothodoksi kama Johann Gerhard (1582-1637) waliiendeleza baadaye. Tazama; Ibid. Theolojia ya Matengenezo hujifungamanisha na mfano wa John Calvin. Calvin alishughulikia kisomi fasili-chimbuzi na mahubiri kama elementi mbili za taaluma moja. (Tazama: K. Karl Müller. Symbolik. A. Deichert: Erlangen, 1896. pp. 340-343+389+454-463).

162 John M. Frame. *The Doctrine of the Knowledge of God*. op. cit., pp. 91-92.

163 Tazama: Lois McKinney. "Why Renewal Is Needed in Theological Education". Evangelical Missions Quarterly 18 (April 1982) 93-94 and the collection; Harvie M. Conn, Samuel F. Rowen (Ed.). Missions and Theological Education. op. cit., especially David Bosch. "Missions in Theological Education". pp. xiv-xlii and Horst Engelmann. Mobilmachung für die Mission: Wie können Mitarbeiter für

Kila taaluma ni lazima ifundishwe akilini, kukilengwa ukuaji wa kanisa na misheni. Wanafunzi hawana budi kuvuviwa na fursa ya kushirikiana katika kazi kubwa ya Mungu ya kufanya uinjilisti na misheni. "Bila kujali fani yake mahususi ya kitaaluma, kila mwana kitivo katika shule ya theolojia ni lazima afundishe masomo yake akiwa na mtazamo wa misheni ya Kanisa."[164] Marehemu, [aliyekuwa] mtaalamu wa elimu ya misheni, wa Afrika Kusini, ndugu David Bosch; wakati mmoja alielezea jukumu muhimu la elimu ya misheni, ambalo linapaswa kupenyeza kwenye nyanja nyingine zote kama chachu.[165] Anabainisha,

> "Tatizo kuu ni kwamba mgawanyo uliopo wa masomo ya kitheolojia uliwekewa kanuni katika kipindi ambapo Kanisa huko Ulaya lilikuwa likijitazama kwa ndani [tu] kabisa."[166]

---

den Missionsdienst gewonnen werden? Missionshaus Bibelschule Wiedenest: Wiedenest, n.d. (ca. 1983) 60 pp.


164 Paul A. Beals. *A People for His Name*. op. cit., p. 199.

165 David Bosch. *„Missions in Theological Education"*. op. cit., pp. xxxi-xxxii.

166 *Ibid*., pp. xxx-xxxi.

Tutaangalia kwa undani kuhusu mtaala hapo baadaye.

Grafu ifuatayo[167] huonesha ukuu wa Agizo Kuu kwenye uhamasishaji na uelekezaji wa fani nyingine zote.




*Dhana ya misheni inapaswa kuhamasisha na kuongoza kazi ya kitheolojia katika nyanja zote.*

Ngoja nirudie hoja nilizoziunda katika kitabu changu cha Warumi[168] kama msingi wa fikra za Paulo:

---

[167] Imechukuliwa kutoka Paul A. Beals. *A People for His Name*. op. cit.,. p. 201.

[168] *Der Römerbrief.* 2 vol. Hänssler: Neuhausen, 1994[1]; RVB: Hamburg, 2001[2]; see also „Romans as a Charter of World Mission: A Lesson in the Relation of Systematic Theology and Missiology“. Reflection: An International Reformed Review of Missiology 4 (1993/94) 1/2 (Sept-Nov): 34-39 = International Journal of Frontier Missions 10 (1993) 4 (Oct): 159-162 = Chalcedon Report No. 342 (Jan

1) Yeyote anayesoma elimu ya misheni kivitendo na kutupilia mbali mafundisho anahudumia kwa kujituma mwenyewe; anapuuza kile Mungu alichokisema juu ya ufanyaji injili.
2) Yeyote afundishaye ‘mafundisho’ yasiyokitwa katika umisheni na yasiyolenga kwenye ufanyaji uinjilisti anafundisha mafundisho yake mwenyewe na anapuuza sababu za Mungu kwa ajili ya mafundisho.
3) Umisheni wa Kibiblia daima huanza na mafundisho sahihi. Mafundisho sahihi daima huongoza kwenye umisheni.

**20. Kushidwa kwa shule za Biblia na seminari za kiinjili kutambuana zenyewe kwa zenyewe ni janga.**

Shule za kiinjili ni lazima zianze kuzikubali kozi na programu za kila moja. Programu zinapaswa ziwe zenye kupatana vema, ili wanafunzi waweze kubadilisha shule, pale ambapo taasisi nyingine itakuwa inafaa zaidi kwa tabia ya mtu husika, hali au mipango yake ya baadaye – na hivyo seminari zinapaswa kuwatia moyo kufanya hivyo! Programu zinapaswa kuratibiwa vema ili ziweze kutoa aina na mabadiliko mbalimbali.

**21. Viwango vya usajili na matakwa yake magumu mara nyingi huakisi njia za kizamani za ufanyaji wa mambo na mara nyingi hufanya liwe jambo lisilowezekana kwa wageni wapya, shule mpya na zilizoanzishwa, kuweza kukubaliwa.[169] Katika siku za usoni, [viwango hivi] havina budi pia kuingiza mitazamo ya elimu ya kivitendo, kiroho na kibinafsi.**

Usajili unapaswa kutumika kutambua kama shule inaandaa vema wanafunzi wake kwa ajili ya taaluma itolewayo, na ni utendaji muhimu kwa ajili ya kuthamini ufaaji wa taasisi kwa malengo ya mwanafunzi. Kwa sababu taaluma ya mchungaji, mmishenari au kiongozi wa Kikristo hutegemea tu kwa juu juu uwezo wa kitaaluma; usajili ni lazima pia uangalia kiwango ambacho wahitimu wa taasisi husika wameandaliwa kuongoza, kufanya kazi, kuitikia ulimwengu wao unaobadilika, na kuelezea ukweli wa kiroho.

Kwa sasa, usajili unajifanya kusisitiza kupita kiasi mitazamo rasmi ya elimu kama vile urasimu. Vigezo hivi vya kizamani (mfano, idadi ya

1994): 43-47; reprinted in Thomas Schirrmacher. *World Mission – Heart of Christianity.* RVB: Hamburg, 2000.

169 Kuhusu michango bora juu ya suala la usajili, tazama: Samuel F. Rowen. „Accreditation, Contextualization and the Teaching of Mission“. pp. 137-155 in: Harvie M. Conn, Samuel F. Rowen (Ed.). *Missions and Theological Education.* Associates of Urbans: Farmington (MI), 1984.

vitabu, fedha, idadi ya walimu wenye shahada ya uzamivu) ni rahisi kupima, lakini mara nyingi ni vyenye thamani halisi ndogo katika mafunzo ya theolojia.[170] Kitu muhimu kuliko idadi ya vitabu katika maktaba ni upatikanaji wa vitabu, ama katika maktaba ya shule au katika maktaba za walimu. Na vitabu ni kwa matumizi gani, iwapo wanafunzi hawafundishwi kuvitumia wakiwa peke yao kufuatana na haiba zao wenyewe, vipawa vyao na huduma yao ijayo? Mabadiliko ya kirasimu kukidhi kanuni za usajili husaidia kuongeza ubora kwa uchache sana.[171]

---

170 Hususani *Ibid*., p. 139.

171 Ibid., p. 141 and Aniul D. Dolanky. *„A Critical Evaluation of Theological Education in Residential Training“*. pp. 156-168 in: Harvie M. Conn, Samuel F. Rowen (Ed.). *Missions and Theological Education.* Associates of Urbans: Farmington (MI), 1984. pp. 158-159.

# Je, Ukatoliki wa Kirumi Umebadilika?

## Mapitio ya Sheria ya Kanoni ya Hivi Karibuni

## Au: Uondoaji Mamlaka ya Baraza kwa njia ya Upapa (1990)[172]

*Baadhi ya waaangalizi huzungumza juu ya matengenezo muhimu yanayoendelea ndani ya Ukatoliki wa Kirumi, lakini tathmini ya matamko rasmi ya karibuni yanapendekeza vinginevyo.*

## I. Mahali pa Kuanzia: Matumizi ya Neno "Mapokeo" katika Maandiko

Kabla ya kujadili Sheria mpya ya Kanisa Katoliki, basi tuanze kwa kufafanua baadhi ya madhanio. Twchunguza mafundisho na muundo wa kitaasisi wa Kanisa lolote kwa mujibu wa ufunuo wa kiungu unaopatikana katika Maandiko Matakatifu. Mtazamo huu unaweza ukatukiwa kwa kiasi kidogo kwenye dhana ya "mapokeo".

Neno "mapokeo" (Kigriki: *paradosis*; Kilatini: *traditio*) katika Agano Jipya linaweza kurejea kwenye kitendo cha "kurithisha" (uwasilishaji); au linaweza kurejea kwenye mambo yaliyorithishwa (yaliyowasilishwa). Kawaida linahusiana na uwasilishaji wa mafundisho au maelekezo. Matumizi ya kibiblia ya neno hili lenyewe hayamaanishi uthaminishaji: mapokeo yanaweza kuwa ya kiungu au ya kibinadamu, ya kweli au ya uongo.

### A. Mapokeo katika Agano la Kale

Agano la Kale halina neno maalumu kwa ajili ya "mapokeo". Hata hivyo, kitendo chenyewe, kinaelezwa kwa dhana mbalimbali. Mapokeo halisi yenye msingi katika matendo ya ufunuo wa *Yahwe* [Yehova] yanapaswa kurithishwa kwa kizazi kinachofuata. Mapokeo potovu, yaliyokitwa kwenye hekima ya mwanadamu, hushambuliwa: **"… Msiende katika**

172 Ilirudiwa kuchapwa „Has Roman Catholicism Changed? An Examination of Recent Canon Law". Antithesis: A Review of Reformed/Presbyterian Thought and Practice 1 (1990) 2 (März/Apr): 23-30.

**amri za baba zenu, wala msizishike hukumu zao… [bali] endeni katika amri zangu, mkazishike hukumu zangu, na kuzitenda…**" (Eze. 20:18-19). Kuyashika sana mapokeo halisi huleta uzima (Mithali 4:13);[na tena] hakuwezi kuzuiliwa (Mithali 4:12).

## B. Mapokeo katika Agano Jipya

Kwa nyongeza, kutumia neno "mapokeo" kwa maana ya kitu kilichowasilishwa, Agano Jipya pia hutumia muundo wa kitenzi "wasilisha", wakati mwingine kikiwa na maana ya "kukubali kushindwa". Vifungu vinaweza kugawanywa kati ya vile vinavyohusika na urithishaji chanya, ambao unapaswa kutiliwa maanani, na vile vile vinavyohusika na ule [urithishaji] hasi ambao unapaswa kuepukwa. Luka anabainisha urithishaji kwa njia ya mdomo wa mashahidi wa kuona kama chanzo cha habari ya Injili yake (Luka 1:2).

### *1. Mapokeo ya Ki–Mungu au Yafaayo*

Pia Paulo kwa uwazi anawaita mashahidi wa kuona [ili] kutetea habari iliyorithishwa ya kifo na kufufuka kwa Yesu kuwa ni yenye kulingana na Maandiko (1 Kor. 15:3k). Meza ya Bwana hurejea nyuma kwenye urithishaji wa Ki–Mungu (=mapokeo) ambao ulirithishwa na wanadamu (1 Kor. 11:23k, imerejewa tayari kwenye mst. 2).

Sambamba na urithishaji wa matokeo ya kihistoria, vilevile ni urithishaji wa maelekezo maalumu ya Mitume ya Injili au ya imani. Maazimio ya baraza la Yerusalemu yalirithishwa kwenye makanisa kama mafundisho yaliyoimarishwa sana yapaswayo "kushikwa" (Matendo 16:4). Katika 2 Wathesalonike 1:15 na 3:6 mapokeo yanapaswa kushikwa sana, ambayo yalirithishwa "ama kwa maneno, ama kwa waraka wetu" (2:15). 2 Petro 2:21 huzungumzia amri takatifu "**zilizotolewa kwao**". Upungufu katika amri hizi unalinganishwa na upungufu katika imani yenyewe. Sambamba na hili, Yuda 3 hutuonya, "**… mnapaswa kushindana kwa dhati kwa ajili ya imani ambayo ilitolewa mara moja kwa watakatifu**". Hivyo, katika Agano Jipya, maana chanya ya mapokeo kama urithi safi wa kitauwa (= mapokeo) hujumuisha Maandiko (rejea, 2 Timotheo 3:15k), Injili, na imani kwa ujumla, vilevile matukio maalumu ya kihistoria na maelekezo ya Mitume, hili la mwisho linapatikana kwetu kwa njia ya Maandiko pekee.

## *2. Mapokeo Potovu au ya Kibinadamu katika Agano Jipya*

Kwa kiwango kile kile kuwa, Agano Jipya huidhihirisha Injili yenyewe kama mapokeo; hupinga mapokeo mengine ambayo hudai mamlaka ya ki–Mungu. Kwa mujibu wa 1 Petro 1:18, ukombozi unahitajika kwa hakika kutoka katika mwenendo wa kuishi ulio batili "**uliopokelewa kwa njia ya mapokeo[173] kutoka kwa baba zetu**"! Hukumu hii hutumika kwa mapokeo yote ya kibinadamu: "**Iweni macho mtu yeyote asije kuwaharibu kupitia falsafa na uongo batili, kwa mapokeo ya wanadamu …**" (Kol. 2:8).

Katikati ya aina zote za wainjilisti na walimu, Paulo hataki mtu yeyote atoke nje ya kile kilichoandikwa (1 Kor. 4:6), kwa kuwa hilo lingemwongoza mtu kujiinua mwenyewe dhidi ya mwingine, wakati kile kilichorithishwa huunganisha (1 Kor. 4:6-7)!

Ushindani wa Paulo hasa ni kwa mapokeo ya Kiyahudi ambayo yalikuwa yameongezwa kwenye Agano la Kale. Kwa uwazi Paulo anayakataa haya "mapokeo ya mababa" ambayo kwayo yeye mwenyewe alikuwa mwenye juhudi nyingi kabla ya uongofu wake kwa Kristo (Gal. 1:14). Utetezi unapatikana hasa katika majadiliano kati ya Yesu na Waandishi na Mafarisayo. (Masadukayo kwa sehemu kubwa, walikataa mapokeo ya mdomo sambamba na sehemu kubwa za Agano la Kale). Katika Mathayo 15:1k na Marko 7:1k mapokeo yanawekwa katika upinzani mkali na amri na Neno la Mungu. Kwa kadri ambavyo mapokeo haya hushikwa, Neno la Mungu hufanywa kuwa tupu (Marko 7:13). Katika uhusiano huu Yesu ananukuu Isaya 29:13, "**Isaya alitabiri vema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, 'Watu hawa huniheshimu kwa midomo yao, ila mioyo yao iko mbali nami. Hata hivyo, huniabudu katika ubatili, wakifundisha mafundisho yaliyo amri za wanadamu.' Kwa kuiweka kando amri ya Mungu, mnashika mapokeo ya wanadamu …**" (Marko 7:6-8).

Katika Hotuba Mlimani, Yesu anatumia mifano halisi kutofautisha Sheria kutoka kwenye mapokeo ya wazee (Mathayo 5:17 - 6:18). Haongezi masharti ya Sheria, bali tu anayarejea: kulaani, kumtamani mwanamke (amri ya kumi!), talaka isipokuwa katika uzinifu, chuki kwa adui za mtu, n.k. ambayo tayari yameshatamkwa kuwa machukizo katika Agano la Kale. Mapokeo ya kifarisayo hayaifafanui Biblia, bali husimama katika upinzani wa moja kwa moja dhidi ya Neno la Mungu popote yadaipo mamlaka ya Ki–Mungu (rejea Marko 7). Kwa hakika, mara nyingi

[173] Huu ni utokeaji pekee wa neon la Kigiriki *patroparadotos* kumaanisha mapokeo.

kutakuwa na mambo fulani yanayohusiana na tamaduni mbalimbali ambapo uvumbuzi unafaa – kwa mfano, saa ya huduma ya ibada, mpangilio wa kukaa, n.k. Lakini haya kamwe hayafungi nafsi za watu wote isipokuwa kama yana msingi wa Biblia. Kujikwaa kwenye mavumbuzi haya haimaanishi kuwa mtu hujikwaa dhidi ya mafundisho ya Mungu ya milele na ya kiulimwengu. Maoni yote yanayohusiana na jinsi Mkristo anavyopaswa kuishi, ikiwa yanadai uhalali wa ki–Mungu, yanaweza kupimwa na kuhojiwa kwa misingi ya Biblia. Hili pia linahusika na Sheria Mpya ya Kanisa Katoliki la Rumi, ambalo ndilo somo letu katika mjadala unaofuata.

## II. Kiini cha Sheria ya Kanisa Katoliki

### A. Sheria za Kanisa Katoliki kwa ujumla

#### *1. Hudai kuwa ni "ya ki–Mungu"*

Sheria ya Kikatoliki haitoi tu muundo wa kisheria wa Kanisa kwa maana ile ambayo kila taasisi kwa wakati fulani hujitiisha yenyewe. Sheria ya Kanisa Katoliki ina tabia tofauti kabisa mbali na ile ya makanisa ya Kiprotestanti, hata kama hii ya mwisho [ya Kiprotestanti] inaweza kupingwa katika haki yake yenyewe. Kamusi moja ya Kikatoliki huelezea Sheria ya Kanisa kama "sheria iliyoumbwa na Mungu na kanisa, kwa ajili ya kanisa".[174]

#### *2. Huakisi Kiini cha Kanisa*

Kwa sababu ya sifa yake dhanifu ya ki–Mungu, Sheria ya Kanisa katika Kanisa la Kirumi siyo ya zao lisilo na msingi maalumu, bali huakisi kiini cha Kanisa: kwa kweli, ndiyo inayoamua kiini cha Kanisa. Mkutano wa Ujerumani wa Maaskofu uliielezea kama ifuatavyo:

> "Yesu Kristo mwenyewe alianzisha muundo asilia wa utaratibu huu. Kanisa ni lenye asili ya ki–Mungu. Uhai wake hutiririka kutoka katika Neno la Mungu, [na] Sakramenti. Mdhamini wa umoja wake ni kiti cha Petro. Maaskofu huongoza dayosisi zao kama wafuasi wa Mitume katika umoja

[174] K. Mörsdorf, article „Kirchenrecht" in *Lexikon für Theologie und Kirche*, 2. edition, ed J. Höfer et al., (Freiburg 1986), vol. 6 pp. 245-250, hapa ni uk. 245.

> pamoja na Papa. Hivyo, Sheria ya Kanisa ni njia ya maisha ya Kanisa, uelezi wa umoja wake na kanuni inayoelezea jinsi ya kuzitunza roho."[175]

Mtazamo huu unabaki kuwa halali hata katika nyakati za hivi karibuni kama nukuu inavyoonesha, na haujadhoofishwa na matengenezo yote yanayodaiwa ya Kanisa Katoliki la Kirumi kwa miongo iliyopita. Katika utangulizi wake wa Sheria mpya ya Kanisa, mwenyekiti wa Tume ya Tafsiri ya Sheria ya Kanoni ya Kijerumani, Winfried Aymans anaandika:

> "Sheria ya Kanisa hukua, kwa mujibu wa uelewa wa Kikatoliki, kutoka katika kiini cha kanisa lenyewe. Kwa mujibu wa mafundisho ya Baraza la Vatikani la pili, [Sheria ya Kanisa] ni upande wa nje wa ukweli changamani; kwa wakati uleule ni maelezo ya kibinadamu ya ukweli wa kiroho wa namna nyingi ambao mzizi wake ni Mungu."[176]

### *3. Huhusika na Wokovu*

Sheria ya Kanisa Katoliki, kwa mujibu wa Kanisa Katoliki la Kirumi, hurejea kwa Mungu na kwa mamlaka ya kiroho ya Kanisa. Hivyo, ina tabia ya kuhusika na upatanishi wa wokovu. Kitabu kilichonukuliwa hapo juu chasema,

> "Kazi ya upatanishi wa wokovu wa Sheria ya Kanisa, ina maelezo machache ya wazi katika kanuni ya zamani iitwayo "*Extra ecclesiam nulla salus*" (nje ya Kanisa hakuna wokovu), ambayo katika uelewa wake wa asili ilirejea Kanisa linaonekana, lililoundwa kwa ngazi za kiutawala [za kimsonge]. Nguvu yake ya kawaida ya kisheria hushiriki jukumu la kiuamuzi katika kazi ya ukombozi ya Yesu Kristo."[177]

Zaidi ya hayo,

> "Sheria ya Kanisa ni Sheria Takatifu kuhusiana na asili yake wa ki–Mungu na kazi yake kuhusika na upatanishi wa wokovu; hili lilielezwa katika maneno ya Kikristo ya hapo mwanzo kwa ajili ya Sheria ya Kanisa, kwa mfano, *jus divinum, sacrum, poli, coeli* (ya ki–Mungu, takatifu, ya kweli, ya mbinguni)."[178]

---

[175] Deutsche Bischofskonferenz 1983 as quoted in W. Aymans, *Einführung in das neue Gesetzbuch der lateinischen Kirche,* Arbeitshilfen 31 (Bonn 1983), p. 5.

[176] W. Aymans, *op. cit.* p. 8.

[177] K. Mörsdorf, *op.cit.* p. 246.

[178] *ibid.*.

Kwa hiyo, mamlaka ya Sheria ya Kikanisa ya Kikatoliki hujitanua zaidi kupita mipaka ya Kanisa Katoliki. Baadhi ya sehemu huhusika kwa watu wote, nyingine kwa watu wote waliobatizwa kwa ukiri wowote ule.

> "Sheria ya Kanisa Katoliki ni sheria ya Kanisa linalounganishwa chini ya Papa kama kiongozi [kichwa] wake anayeonekana, ambalo lenyewe hujitambua kama Kanisa la Yesu Kristo: kwa hiyo, utaratibu wake wa kisheria kimsingi huhusika na watu wote waliobatizwa… Ingawa madai kuhusiana na Wakristo wasio Wakatoliki kwa ujumla hayawezi kulazimishwa, lakini bado yana umuhimu wa kivitendo wakati wowote uhusiano wa kisheria kwa Wakristo wasio Wakatoliki (mfano, uhalali wa ndoa) unapoletwa mbele ya kongamano la Kikatoliki."[179]

## B. Tofauti kati ya Haki ya Mungu na ya Kibinadamu katika Sheria ya Kanisa

Kwa kuwa sasa kuna toleo jipya la Sheria ya Kanoni, ni wazi kuwa siyo maeneo yote ya sheria hiyo hayabadiliki. Kipekee, tofauti inapaswa kufanywa kati ya sheria za ki–Mungu na zile za kibinadamu chini ya mfumo wa sheria ya kikanisa.

> "Sheria halisi ya kikanisa, sawa na sheria zote za kibinadamu, yaweza kubadilika ili kukabiliana na mazingira yanayobadilika. Sheria ya ki–Mungu haibadiliki, ingawa haipaswi kufikiriwa kama ya kudumu. Sawa na kwamba kuna (maendeleo ya mafundisho) endelevu katika hali ya uelewa na uunganishaji wa mambo ya ufunuo, vivyo hivyo Kanisa pia hukua katika uelewa wake chanya wa sheria ya ki–Mungu – kwa mfano, mafundisho yanayohusu ukuu wa papa. Zaidi ya yote, hili hufanya kazi kwa kanuni ya ki–Mungu ya asili."[180]

Herman Avenarius anaelezea tofauti vema zaidi:

> "Sheria ya Kanoni ya Kikatoliki huanzia kwenye ukuu wa sheria ya ki–Mungu (*ius divinum*). Hii imegawanyika katika makundi mawili: Sheria chanya ya ki–Mungu *(ius divinum positivum)* kama ilivyofunuliwa katika historia ya ukombozi, zaidi ya yote katika Maandiko; na sheria ya asili *(ius naturale)* zitokanazo na ufunuo wa asili wa Mungu katika mpango wa uumbaji. Sheria ya *ius divinum* ni ya kiulimwengu na halali kwa nyakati zote; haiwezi kuwekwa pembeni kwa nguvu, wala kwa kubadilishwa. Chini ya kundi hili kuna Amri Kumi, ibada za Sakramenti… na ukuu wa upapa.

---

179 *ibid.* p. 245.
180 *ibid.* p. 246.

> Sheria ya kibinadamu husimama kinyume na *ius divinum* na zinaweza kugawanywa katika makundi ya sheria ya kiraia *(ius civile)* na sheria ya Kanisa *(ius humanum ecclesiaticum)*; kwa uasili wake yaweza kubadilishwa. Mamlaka ya kiutendaji ya *uis humanum ecclesiasticum,* ambayo yanawabana wale waliobatizwa tu, yako kwa Papa kwa ajili ya Kanisa zima, na kwa Askofu kwa ngazi ya dayosisi."[181]

Katika toleo lolote jipya la Sheria ya Kanoni, sheria ya ki-Mungu inaweza tu kupangwa [kupitiwa] tena, wakati sheria ya kibinadamu yaweza kubadilishwa kabisa. Hata hivyo, bado matamko ya awali yanaendelea kuwa na maana:

> "sheria ya zamani iliyofutwa, huendelea kuishi kama ya msingi katika CIC,[182] na huendelea kuwa na umuhimu kwa ajili ya fasili yake endelevu."[183]

Mtu anapaswa kutia akilini historia ya tofauti hii. Kwa maneno ya mkanoni wa Kikatoliki, "tofauti kati ya ius divinum na ius humanum haikutambuliwa kwa uwazi hadi kipindi cha Matengenezo".[184]

Kwa mtu wa nje, inaweza kuwa vigumu kutofautisha kati ya sheria ya ki-Mungu na sheria ya kinadamu ndani ya Sheria ya Kanoni. Hata maprofesa wa Kikatoliki wa Sheria ya Kanoni wana mabishano yao juu ya hili.[185] Hata hivyo, vilevile jambo hili ni kweli kwa mafundisho ya Kanisa Katoliki. Mafundisho yote ya kidogma yasiyokosea huchotwa kutoka katika mafundisho maalumu kupitia mchakato tata wa kimsonge. Katika toleo la Kijerumani la mafundisho muhimu zaidi na maandiko ya Kanisa Katoliki, jaribio lilifanywa [la] kugawanya mafundisho katika yale ambayo "hayakosei" au yasiyobadilika, na yale yanayoweza kupitiwa tena.[186] Kazi hii inajisifu yenyewe kama kijalizo kizuri cha mafunzo ya Sheria ya Kanoni.

Tunafanya muhtasari wa sifa za Sheria ya Katoliki ya Kanoni kwa maneno ya Erwin Fahlenbusch, profesa wa alama za kanisa:

---

181 H. Avenarius, *Kleines Rechtswörterbuch,* (Bonn 1985), p. 217.

182 CIC ni kifupi cha Codex Iuris Canonici (Mkusanyiko wa Sheria ya Kanoni) na hudokeza mkusanyiko ulioandikwa wa Sheria ya Kamisa Katoliki.

183 K. Mörsdorf, article „Codex Iuris Canonici“ in *Lexikon für Theologie und Kirche,* 2. edition, ed J. Höfer et al., (Freiburg 1986), vol. 2 pp. 1244-1250, here p. 1246.

184 E. Corecco in *Handbuch des Katholischen Kirchenrechts*, ed J. Listl et al., (Regensburg 1983), p. 14.

185 e. g. Listl et al., op.cit.

186 J. Neuner, H. Roos, Der Glaube der Kirche in den Urkunden der Lehrverkündigung, 10. edition, (Regensburg 1979).

> "Kanisa Katoliki la Kirumi huendesha ibada yake na maisha yake katika ulimwengu huu katika mtindo wenye nidhamu: Mpangilio wake umeundwa kisheria. Sheria ya Kanoni (au Sheria ya Kanisa Katoliki) hujumuisha kwa ujumla sheria zote (matamko ya kisheria; "kanoni", kipimo, kiwango) zinazotawala utendaji na taasisi za Kanisa… Umuhimu wa sheria hiyo, kwa Kanisa Katoliki la Kirumi, haukurahisishwa tu kutokana na ukweli kuwa ni ushirika wa kijamii, na kama ilivyo kwa ushirika wowote ule, hitaji la sheria fungamanishi. Badala yake huona umiliki wake wa nidhamu kama unaotolewa sambamba na katiba na huduma yake. Kwa maneno mengine, nidhamu ya Kanisa ni ya ukombozi – iliyofungwa na sheria za kihistoria; na kimantiki na kiuhalisi hutangulia viwango muhimu kwa ajili ya taasisi yoyote ya kijamii. Hujumuisha sheria zinazohitajika kwa ajili ya uratibu na ulinzi, lakini huenda mbali zaidi ya hili kwa kuwa kihalisia huhusishwa na kufanya kazi ya upatanisho wa wokovu. Sheria ya Kikanoni hujitofautisha yenyewe kutoka kwenye mfumo wowote wa sheria kama vile Kanisa linavyojitofautisha kutoka kwenye jamii nyingine yoyote. Ni uakisi wa uelewa wa Kanisa Katoliki la Kirumi wa asili yake lenyewe."[187]

# III. Sheria Mpya ya Kanoni ya Kikatoliki ya 1883

## A. Sheria ya Kanisa kama Uelezi wa Upapa

Sheria ya Kanisa Katoliki huchota kikamilifu mamlaka yake kutoka kwenye ofisi ya kipapa ya Petro, kama ilivyo wazi kutoka katika nukuu hapo juu. Aymans anaandika katika mazingira ya kuwasilisha uibukaji wa polepole wa sheria mpya:

> "kazi ya mageuzi, iliyoanzishwa na kusaidiwa na Baraza, na matokeo yake katika muundo wa Kodeksi inayotangazwa kisheria[188] sasa, ulitolewa rasmi kwa njia ya mamlaka ya Papa."[189]

Hali hii ya mambo hujidhihirisha wazi katika jina la Sheria mpya ya Kanoni:

> "Mkusanyiko wa Sheria ya Kanoni, iliyotangazwa kisheria kwa mamlaka ya Papa Yohana Paulo II" (imetafsiriwa kutoka CIC, toleo la 1984).

---

187 E. Fahlenbusch, *Kirchenkunde der Gegenwart,* Theologische Wissenschaft 9, (Göttingen 1979), p. 73.

188 „Kutangaza rasmi au kisheria [promulgate]" ni kishazi rasmi kwa ajili ya utaratibu wa ufafanuzi wa papa, jambo linaloipa nguvu nyaraka husika.

189 W. Aymens op.cit. p. 9.

## B. Uhalisia wa Sheria ya Kanoni

Sheria mpya ya Kanonia ya 1983 ni chombo kizuri sana kwa ajili ya kuhakikisha hali ya sasa ya maendeleo ya Kanisa Katoliki. Yeyote atakayejihusisha na mijadala na Sheria ya Kanisa Katoliki hatahitaji kujibu kipingamizi kuwa anashambulia misimamo ya Kikatoliki iliyopitwa na wakati au anajaribu kuvuta mambo ya pembeni kuyaleta katikati ya jukwaa. Sheria ya Kanisa ya 1983 ni:

– iliyovuviwa na Vatikani II, na hudai kuchukua mageuzi yake yenyewe na kuyaweka katika muundo thabiti;
– kazi ndefu ya karne katika wakati wetu wenyewe, na imeleta mafuriko ya maandiko mapya yakitoa hoja juu ya mabadiliko na kupendekeza matumizi ya kivitendo;
– ilichapwa kwa mamlaka ya Papa aliyepo;
– kama zilivyo Sheria zote za Kanoni, imefungwa pamoja na kiini cha Kanisa Katoliki vilevile na dhana yake ya wokovu.

Uhalisia wa Sheria mpya ya Kanisa Katoliki utaeleweka vema zaidi kama tutatazama maendeleo yake ya kihistoria.

## C. Usuli wa Kihistoria wa Sheria Mpya ya Kanoni

Sheria ya kanisa daima imeshiriki jukumu kubwa katika historia ya Kanisa Katoliki la Kirumi. Hata hivyo, kwa karne nyingi, ilikuwa imetawanywa katika nyaraka nyingi, na sehemu zake nyingine zilipachikwa katika maandiko mengine na mara zote huchukuliwa kutoka utendaji wa sasa. Baada ya juhudi ya miaka mingi, katika mwaka 1917, sheria na maazimio yaliyosambaa yasiyo na idadi yalikusanywa pamoja katika kazi [kitabu] kubwa iitwayo “Codex Iuris Canonici” (CIC), ambayo imebaki ikitumika kwa kiasi kikubwa bila mabadiliko wala masahihisho mpaka 1983.

Tarehe 25 Januari 1959, akilitarajia kwa hamu Baraza la Vatikani la Pili (1962-1965), Papa Yohana XXIII alitangaza mapitio yenye masahihisho ya Sheria ya Kanisa, ambayo yalikuwa yajumuishe hususani mabadiliko [ambayo yangefanywa] na Baraza la Vatikani la Pili. Wanatume mbalimbali waliifanyia kazi baada ya Baraza.

Papa Yohana Paulo II, aliyechukua ofisi mnamo mwaka 1978, aliupa mradi [huu] msukumo mahususi. Baada ya maandalizi ya muda mrefu, mnamo tarehe 25 Januari 1983 alitoa rasmi Sheria mpya ya Kikatoliki – kwa istilahi ya Kikatoliki “aliitangaza rasmi” (“promulgated” it) – akitenga tarehe 27 Novemba 1983 kama tarehe ambayo utekelezaji wake ungeanza. Je, ilikuwa ni bahati tu kuwa sherehe ya siku ya kuzaliwa kwa Martin

Luther iliangukia mwezi ule ule, ambayo kwa dhati ilisherehekewa na makanisa ya Kiprotestanti?

Sheria mpya ya Kikatoliki hutumika kwa Wakristo Wakatoliki wote walio katika tawi la Kilatini la Kanisa Katoliki. Mengi ya maazimio hudai uhalali kwa watu wote waliobatizwa; [maazimio] mengine mengi kwa Wakatoliki wote. Hata hivyo, mengi ya maazimio, huhusika na Wakatoliki wa Kilatini na wa Kirumi, hii inamaanisha, siyo kwa (ni kwa kiasi kidogo sana) Makanisa ya Othodoksi ambayo yanaunganishwa kwenye Kanisa la Kikatoliki la Kirumi. Kusudio la msingi la kuanzishwa kwa Sheria ya Kanisa Katoliki itakayotumika sawia kwa Makanisa yote yasiyo ya Kilatini ndani ya wigo wa Kanisa Katoliki lilishindwa. Kwa kiasi fulani, maagizo mengine huhusika na Makanisa haya, hasa kwa yale yenye urithi wa kiothodoksi. Hata hivyo, kwa kigezo cha idadi, makanisa haya hayana umuhimu.

## D. Tofauti kati ya Sheria za Kanisa za 1917 na 1983

Katika muundo na yaliyomo kuna tofauti nyingi kati ya sheria kama zilizochapwa mnamo mwaka 1917 na 1983.

Wakati ambapo Sheria ya Kanisa ya mwaka 1917 ilifinyangwa kwa uthabiti baada ya muundo wa kisheria wa Sheria ya Kirumi (persona/res/actiones, yaani watu/vitu/matendo), sheria mpya inajikita zaidi kwa masuala ya mtu binafsi kwa mujibu wa Vatikani II. Baada ya utangulizi mrefu, Kitabu cha I huanza na “Kanuni [desturi] za jumla”. Kitabu cha II kinafuata na “Watu wa Mungu”. Hiki hueleza kwa kina zaidi kuliko kile cha kwanza na kimeingiza haki na wajibu wa walei na sehemu muhimu juu ya Wakleri. Ni mahali hapa kuwa mafundisho–kanisa ya Kanisa la Kirumi (=nadharia ya kanisa) yamefunuliwa. Kinyume chake, Kitabu cha III kinachozungumza juu ya “Ofisi ya Ufundishaji ya Kanisa “ni kifupi sana! Inashangaza kuwa sehemu hii pia inajumuisha kanuni za shule na vyuo vikuu vya Kikatoliki. Kitabu cha IV chenye maelezo ya kina, kinachohusu “Ofisi ya Kutakasa katika Kanisa”, kwa umuhimu hujumuisha, maagizo yote ya kisakramenti. Sehemu nyingine ni Kitabu cha V kinachohusu “Mema ya Muda ya Kanisa”, Kitabu cha VI kinachohusu “Adhabu katika Kanisa”, Kitabu cha VII kinachohusu “Michakato”; hivi vitatu huelezea muundo mzima wa kisheria wa Kanisa pamoja na mfumo wake wa kimahakama.

## E. Maoni ya Jumla juu ya Sheria Mpya ya Kanisa

Kwa Sheria mpya ya Kanisa, Kanisa Katoliki kwa mara nyingine tena linajifunua lenyewe kama dini halisi ya sheria ya (mwanadamu). Luther alizungumza kwa usahihi juu ya “sheria ya Papa”. Ni Sheria ya Kibiblia tu inayojumuisha Sheria ya Musa ya Agano la Kale ina asili ya ki–Mungu ambayo Sheria mpya ya Kanoni bila haki inadai [asili ya ki–Mungu] (mfano, Apost. Const. 14, 17). Sheria ya Kibiblia hujitofautisha yenyewe kutoka kwenye Sheria ya Kikanoni ya Kikatoliki kwa maana ya kuwa ni fupi, jumuishi, na rahisi; kwa sehemu kubwa inaelezwa kwa kanuni na mifano ambayo inaweza kutumiwa katika hali halisi. Sheria ya Kanisa Katoliki ni tofauti sana. Kanoni 1,752 sambamba na vipengele vyake hushughulikia kila kitu kutoka kwenye haki ya uwepo wa Kanisa hadi kwenye gharama za mchakato, kutoka kwenye Chuo Kikuu cha Kikatoliki mpaka kwenye vyeti vya Kipaimara, utengwaji wa moja kwa moja mpaka kwenye uuzaji wa masalia ya vitu vya watakatifu. Katika yote haya, hakuna kinachoachwa kama bahati; istilahi zote zinaelezwa barabara kabisa.

Mifano miwili itaonesha kwa kina kiwango cha kujali.

Askofu anaagizwa kama ifuatavyo:

> “Isipokuwa kwa sababu nzito na ya dharura hapaswi kutokuwepo katika dayosisi yake wakati wa Krismasi, wakati wa Wiki Takatifu, wakati wa Pasaka, wakati wa Pentekoste, au Corpus Christi [Ekaristi Takatifu].” (Kan. 395 §3)

Maana ya mtoto haramu inaendelea:

> “Watoto huchukuliwa kuwa halali iwapo wanazaliwa angalau siku 180 baada ya sherehe ya ndoa au ndani ya siku 300 kutoka tarehe ambapo maisha ya unyumba yalipokatizwa.” (Kan. 1138 §2)

## F. Mwendo Kuielekea Biblia?

Mtu husikia ahadi za kuondoka katika mwelekeo wa Biblia katika Sheria mpya ya Kanoni. Vifungu vingi kwa hakika vina ishara mpya ya Kiinjili ndani yake. Fungu moja husomeka “kuhesabiwa haki kwa njia ya imani” (Apost. Const. 15), “kuzaliwa upya katika Kristo” (Kan. 208) na zaidi sana. Lakini mwonekano huo ni wa udanganyifu. Maneno yako pale, lakini yanamaanisha kitu kingine kabisa. Mifano michache itadhihirisha hili.

Maaskofu hufanya kazi pamoja katika “roho ya ushirikiano [ki–baraza]” (Apost. Const 7, 13, 20), lakini maneno yao hayana umuhimu

zaidi kando na uthibitisho wa Papa (rud., hasa 13, 20). Uekumenika unatetewa (Apost. Const. 22; Kan. 256 §2:383 §3:755 §1), lakini wanaambatanisha sharti, "kama unavyoeleweka na Kanisa". Wanazungumza juu ya "utakaso unaoendelea" (Kan. 210), lakini wanamaanisha hapa kuwa utakaso wa waamini hufanyika kupitia kushiriki Sakramenti (rejea Kitabu IV "Ofisi ya Kutakasa katika Kanisa" kuhusu Sakramenti; Kan. 834, 1253; na hasa 835 §1). Kutoka katika umisheni wa kisasa, wanachota wazo kuwa walei ni lazima washiriki "katika ofisi ya Utume" (Kan. 225 §1), lakini kwa wakati ule ule wanaimarisha ukuu wa kisakramenti wa wakreli [viongozi wa kanisa]. Wanasema "injili" inapaswa kuhubiriwa kwa watu wote (Kan. 9, 11; 747§1; 757; 781k.), lakini wanalielewa hili kwa ujumla wake kisakramenti na wanaongeza "kuhusiana na Kanisa zima, kazi ya kutangaza Injili kimsingi imeaminiwa kwa Papa na kwa Baraza la Maaskofu" (Kan. 756 §1). Hivyo basi, kazi hii inaweza kukasimiwa kwa mapadre (Kan. 757).

## G. Makuzi katika Sheria Mpya ya Kanisa?

Sheria mpya ya Kanisa kwa hakika hujumuisha mlolongo wa "makuzi". Hata hivyo, haziendi katika mwelekeo wa kurahisisha mafundisho ya Kikatoliki kwa kupendelea kurudi kwenye msingi wa Kibiblia, lakini badala yake bado huongeza zaidi kwenye mfumo ule ule ambao umekuwa ukikua kwa karne nyingi.

### *1. Kukua kwa Upapa*

Mfano mzuri wa kukua huku ni nafasi ya upapa. Katika kipindi cha karne nyingi, upapa umetanuliwa zaidi sana. Uhusiano wa Papa na kusanyiko la Maaskofu, yaani Baraza, mara zote umekuwa hoja muhimu ya ushindani. Hatimaye, mabadiliko yalifikia kiwango ambacho ni Papa tu awezaye kuitisha Baraza – lakini bado Baraza katika mkutano linaweza kuamua mambo yahusuyo mafundisho yasiyo na makosa na husimama likiwa na haki sawa kama ile ya Papa. Baada ya hili, hatua iliyofuata ilichukuliwa katika karne ya 19: katika mwaka 1870, matamko ya ki "ex cathedra" [eksi kathedra] ya papa yalitangazwa kuwa yasiyo na makosa. Papa alililazimisha fundisho hili la kidogma kupitia Baraza, kwa kutumia njia ambazo daima hazikuwa za wazi na zenye ushawishi, kama ambavyo mwanahistoria wa Kikatoliki August Bernhard Haster ameonesha.[190]

---

[190] A. B. Hasler, *Wie der Papst unfehlbar wurde* (Frankfurt 1981); cf. H.Küng, Unfehlbar? Eine Anfrage (Frankfurt 1980).

Hata hivyo, kwa kiwango kikubwa mafundisho haya yamebaki kuwa ya kinadharia baada ya jaribio la mwanzo la uwezo wake, ama kwa sababu Papa na Baraza waliunganishwa kwenye maswali ya sasa, au kama inavyoweza kuwa, hakuna maamuzi ya ex cethedra [eksi kathedra] ambayo yalihitajika. Ni baada ya miaka 80 tu ndipo upapa ulipoweza kuchukua hatua nyingine: Matumizi ya fundisho la udogma la kutokukosea kwa upapa. Papa, pasipo mkutano wa Baraza linalokutana na pasipo kuweza kurejea hata kidogo kwa kilichotangulia katika tamaduni za kanisa zinazojulikana, alitamka fundisho la kidogma la kupaa kwa Mariamu.

Baada ya "hatua hii ya maendeleo" katika kumpa mamlaka zaidi Papa, hatua inayofuata iliweza kuandaliwa: Kuondoa kisheria mamlaka ya baraza. Kwa kuwa mpaka sasa, Baraza lilikuwa na haki sawa na Papa na lenyewe lingeweza kufanya maamuzi yasiyo na makosa.

## *2. Uondoaji wa Mamlaka ya Baraza kwa Njia ya Upapa*

Uondoaji wa mamlaka ya Mabaraza ulifanywa kimya kimya na ulikamilishwa kwa usiri kwa kutumia Sheria mpya ya Kanisa Katoliki (hususani Kan. 749 §2).

Katika suala hili neno zuri "ushirikishanaji majukumu" halipaswi kudanganya, kama lilivyodokezwa tayari hapo juu. Hofu iko wazi katika Kan. 333 §2, ambayo huendeleza mamlaka yasiyo na mpaka ya Papa juu ya Kanisa kama inavyoelezwa katika Kan. 333 §1.

> "Pontifa wa Rumi, katika kutimiza ofisi ya mchungaji mkuu wa Kanisa, daima huungana na Maaskofu wengine na Kanisa la Ulimwengu; hata hivyo, kwa mujibu wa mahitaji ya kanisa, anayo haki kuamua namna ya utendaji wa jukumu hili, ama kibinafsi au kwa ushirikiano."

Papa, kwa mujibu wa aya hii, hufanya kazi "kwa ushirikiano" tu pale anapopenda kufanya hivyo. Ukataji rufaa kwa Baraza dhidi ya Papa unakatazwa (Kan. 1372). Baraza "pamoja na mkuu wake, na kamwe si pasipo mkuu wake, pia ni mtekelezaji wa mamlaka kuu na kamili juu ya Kanisa la Ulimwengu" (Kan. 336). Hivyo, amri za Baraza ni halali tu pale ambapo kuna makubaliano na Papa (Kan. 341 §1)!

| **Kupanuka kwa Mamlaka ya Papa katika Nyakati za Sasa** | |
|---|---|
| | Papa ni … |
| Sheria ya Kanisa ya 1983 | … bwana juu ya Baraza |
| Fundisho juu ya Mariamu la 1950 | … asiyekosea hata bila Baraza |
| Fundisho juu ya Upapa la 1870 | … asiyekosea sawa na Baraza |

### *3. Sheria ya Kanisa kama Sheria Mpya ya Upapa?*

Sheria ya Kanisa yote hukatiwa rufaa kwenye mamlaka ya Papa (Apost. Const. 13, 30). Mara kwa mara mamlaka yake kuu huimarishwa. Yeye ni hakimu mkuu, ambaye yeye mwenyewe hawezi kufikishwa mbele ya mahakama (Kan. 14041105); pasipo yeye, hakuna Baraza liwezalo kufikia maamuzi au hata kukutana (Kan. 336-341); Yeye hakosei katika maamuzi yake ya mafundisho (Kan. 749 §1; rej. 2). Kan. 331 husema,

> "Askofu wa Kanisa la Rumi [yaani Papa], ambaye kwake inakaa ofisi iliyotolewa kwa njia maalumu na Bwana kwa Petro, wa kwanza miongoni mwa mitume, na kurithishwa kwa warithi wake, ni mkuu wa Baraza la Maaskofu, Mwakilishi wa Kristo na Mchungaji wa Kanisa la Ulimwengu hapa duniani; kwa hiyo, kwa stahili ya ofisi yake, anafurahia mamlaka ya kawaida makuu, kamili, yaliyo karibu, na ya kiulimwengu katika kanisa, ambayo daima anaweza kuyatekeleza kwa uhuru."

Ili kuwa na hakika, cheo "Mwakilishi wa Kristo" kilitumika hapo kabla, lakini sasa kwa mara ya kwanza kimefungamanishwa katika Sheria ya Kanisa. Kanoni za 330-336 zinaimarisha sana ofisi ya upapa, iwe ni juu yake "kuamua namna ya utendaji wa jukumu hili, ama kibinafsi au kwa ushirikiano". Mazungumzo ya Baraza la Maaskofu ni utaratibu tu, kwani Baraza na Sinodi vyote vimenyimwa haki [ya kuamua].

Mamlaka ya Papa, ambayo kwa kiasi kidogo yangeweza kuongezeka zaidi tena, yameandikwa katika nukuu nyingine:

> "Hakuna rufaa wala kimbilio dhidi ya maamuzi au amri ya Pontifa wa Rumi." (Kan. 333 §3)
>
> "Pontifa wa Rumi ni hakimu mkuu wa ulimwengu wote wa Kikatoliki; huendesha kesi ama yeye mwenyewe au kupitia mahakama za kawaida…" (Kan. 1442)

> "Wanafunzi hawana budi kufinyangwa sana kiasi kwamba, wakiwa wamejazwa na upendo kwa Kanisa la Kristo, wajitoe kwa unyenyekevu na upendo wa kindugu kwa Pontifa wa Rumi, mrithi wa Petro, na wawe wameshikamanishwa kwa Askofu wao wenyewe kama watumishi wenzake waaminifu…" (Kan. 245 §2)
>
> Watumishi wa kanisa wamefungwa kwa njia ya wajibu maalumu kuonesha heshima na utii kwa Pontifa Mkuu na kwa wenzao wa kawaida." (Kan. 273)
>
> "Kwa mujibu wa Kanisa la Ulimwengu kazi ya kutangaza Injili kipekee imeaminishwa kwa Pontifa wa Rumi na kwa Baraza la Maaskofu." (Kan. 756 §1)

Kwa ujumla, mtu anapata taswira kuwa Sheria mpya ya Kanisa katika hali halisi ni Sheria ya Upapa. Katika sura zote muhimu, ukuu kamilifu wa papa umesisitizwa kuliko kitu chochote, hata kama suala liwe ni kutunza roho za watu, kufanya uinjilisti, mali ya kanisa, hukumu, au utungaji sheria wa kanisa. Kazi zote za Kanisa kwa uhalisia hutekelezwa tu kama zinavyoagizwa na Papa na katika uwakilishi wa Papa, na kutoka katika hili hujipatia mamlaka yao [ya] (Kan. 204 §2: uongozi wa watu wa Mungu; Kan. 377 §1-3: uchaguzi wa Maaskofu; Kan. 782 §1: mwelekeo wa misheni; Kan. 1256: mamlaka juu ya mali zote; 1273: utawala wa mali za kanisa; n.k.).

### *4. Uhakiki–kinzani wa Kikatoliki kuhusu Haki Mpya za Kipapa*

Uhakiki–kinzani kutoka katika kalamu za Wakatoliki wasomi pia huonesha ni kwa kiasi gani Sheria mpya ya Kanisa Katoliki ni upanuzi zaidi wa ukuu wa upapa. Jarida la Kikatoliki "Diakonia" liliweka rasmi kwenye toleo la (Mei 1986) kichwa cha habari kiitwacho "Askofu". Ndani yake mkanonia Knut Walf alihitimisha kuwa maendeleo ya baada ya baraza hayakutoa kile ambacho Baraza lilikuwa limeahidi kwa neno "ushirikishanaji majukumu". Anaandika:

> "'Codex Iuris Canonici' mpya ya mwaka 1983 inaweza kuleta kikwazo kikubwa kisichoshindwa katika hali ya kuondoa mvutano kati ya Uaskofu Mkuu [Upapa] na uepiskopo [uaskofu] katika kipindi cha karibuni chenye matokeo yanayotabirika. Mara kwa mara jambo hili haliwezi kurudiwa: Kodeksi mpya haipulizii roho ya ushirikiano katika sehemu zake za katiba za

kisheria. Bali, inaifanya nafasi ya ukuu ya upapa kuwa ngumu katika namna ngeni hata kwenye Kodeksi ya 1917."[191]

Kwa kutoa mifano, Walf ananukuu yafuatayo:

> "Badiliko la msisitizo kuelekea kwenye nafasi kuu ya mamlaka ya Papa" katika Kan. 331, "ambamo ndani yake mamlaka haya ya Papa katika Kanisa, lakini pia kipekee kwenye Baraza la Maaskofu, linafasiliwa kwa upya katika namna ambayo haliwezi kuvukwa", kinyume na kile Walf hurejea "Uundaji wa wastani wa kodeksi ya awali".
>
> Madai ya cheo cha "Mwakilishi wa Kristo" katika Kan. 333.
>
> Kuchukua cheo kilichotumiwa katika Dola ya Rumi kwa ajili ya Mfalme, "principatus" katika Kan. 333 §1 na upanuzi uliomaanishwa kutoka kwenye mamlaka ya kisheria juu ya Kanisa zima kwenda kwenye mamlaka ya "kawaida", ambayo yanajitanua juu ya "makanisa yote mahususi na makundi yote ya makanisa mahususi" (Kan. 333 §1).
>
> Katika kuyahusisha kindugu mabaraza ya Kikanisa. Kwa mujibu wa Walf, "Kwa mpangilio na kwa Sheria, Baraza limebanwa kwenye kona mbaya". Wakati Sheria ya zamani ya Kanisa iliwaweka Papa na Baraza, kila mojawapo kwenye haki sawa, [kila moja] katika sehemu yake yenyewe, katika Sheria mpya ya Kanisa tofauti zimeondolewa. Baraza limefanywa kuwa sehemu ya ibara inayomhusu Papa, na Baraza la Maaskofu linaweza kuombwa kuitishwa kwa barua na kwa njia nyingine ambazo hazikufahamika hapo kabla, siku zote chini uongozi wa Papa.

Uhakiki-kinzani sawa na huo wa ukuu mpya wa Papa ukihusishwa na Baraza umekwishachapwa na waandishi wengine wengi wa Kikatoliki. "Concilium-foundation" ya kimataifa, iliweka wakfu toleo la jarida lake lote liitwalo "Concilium", ambalo huchapwa katika lugha mbalimbali kuhusiana na maana ya Baraza la Kikanisa katika Sheria mpya ya Kanoni, likitamka uondoaji wa mamlaka ya baraza.[192] Katika mchango wake, Mkanonia wa Kiitaliano Giorgio Feliciani[193] anaipinga tume ambayo iliandaa madhamirio ya Baraza la Maaskofu, kwa msingi kuwa jukumu kuu la Baraza lilitupiliwa mbali pasipo kutoa halalisho lolote [sababu zozote]. Profesa wa Theolojia wa Kimarekani, Joseph Komochak,[194] alionesha kuwa Sheria mpya ya Kanisa iliharibu madhamirio ya [Mtaguso]

[191] Makala ya K. Walf, „Kollegialität der Bischöfe ohne römischen Zentralismus?“, in *Diakonia: Internationale Zeitschrift für die Praxis der Kirche,* vol. 17 (1986) 3, pp. 167-173, hapa ni kr. 171-172; cf. mifano kr. 172-173.

[192] *Concilium* vol. 19 (1983) 8/9, pp. 499-586.

[193] *ibid.*, pp. 526-530.

[194] *ibid.,* pp. 574-579.

wa Vatican II kwa kupendelea sheria mpya ya kipapa. Anahofu kwamba, hatimaye Maaskofu watashushwa kuwa [watu wa] “ndiyo bwana” kwa Papa, hawatakuwa na mamlaka yao tena.

Uhakiki-kinzani mwingine hujumuisha mtungo wa Papa wa [majina ya] vyeo vipya (mf. “Mwakilishi wa Kristo”), wakati ule ule, orodha ya [majina ya] vyeo yaleyale kwa Baraza hayawezi kuendelea kutumika.[195]

Concilium-Foundation katika haya yote huona maendeleo yanayoelekea kwenye “kulifanya Baraza la Kikanisa kuwa chapwa”. Baraza “halifasiliwi tena kama taasisi binafsi ya kisheria inayojitegemea mbali na mkuu. Kinyume chake, sasa kuna hatari kuwa Baraza litamezwa na ukuu wa kipapa”.[196]

Kimsingi, sikusudii kulitumikia Baraza la Kikanisa la Kikatoliki. Kwa haya yote nitaka tu kuweka wazi yafuatayo:

Ikiwa kuna aina yoyote ya “maendeleo” katika Sheria mpya ya Kanisa Katoliki, basi ni “maendeleo” katika mwelekeo ulio wazi kabisa. Hakuna maendeleo yatakayovumbuliwa katika mwelekeo wa kufungua kweli rahisi za Biblia wala kuelekea katika mafundisho ya Kiinjili. Badala yake, tunaona kupanuka zaidi kwa mamlaka ya upapa: upanuzi ambao unaangukia katika uhakiki-kinzani mkali hata [kutoka] ndani ya Kanisa Katoliki na unaoonekana kama ni jambo liendalo kinyume na mapokeo ya Kikatoliki.

## H: Mifano ya Uhifadhi wa Mafundisho ya Kikatoliki katika Sheria Mpya ya Kanisa

Mifano mingine zaidi itaonesha kuwa Kanisa Katoliki katika Sheria yake mpya ya Kanisa kiuhalisia lilihifadhi mafundisho na vitendo ambavyo Waprotestanti huvipinga na ambavyo haviwezi kupatanishwa na Biblia; kwa hakika ni kwa kiwango ambacho Kanisa limeyachonga mambo hayo. Ukataaji wa mafundisho maalumu kutoka katika mtazamo wa Kibiblia umeondolewa hapa, kwa kuwa jambo hili limekwishafanywa tayari katika vitabu bora vya mwanatheolojia wa kimatengenezo Boettner[197] na Wananyakati Uhlmann na Bühne,[198] pamoja na maandiko mengine.

---

[195] *ibid.,* p. 585.

[196] *ibid.,* p. 586.

[197] L. Boettner, *Roman Catholicism,* (Philippsburgh 1962).

[198] P. H. Uhlmann, *Die Lehrentscheidungen Roms im Lichte der Bibel,* (Berneck 1984); W. Bühne, *Ich bin auch katholisch: Die Heilige Schrift und die Dogmen der katholischen Kirche,* (Bielefeld 1988).

### *1. Utukuzaji wa Mariamu na Watakatifu*

Wokovu wa roho uko chini ya ulinzi wa Mariamu (Apost. Const. 31). Waseminari hawana budi kukuza hususani “uchaji kwa Bikira Mariamu Mbarikiwa”, rozari na matendo mengine (Kan. 246 §3), ambapo [hayo yote] ni njia kwa ajili ya utakaso wao (Kan. 276 §5). Watu wa Mungu wanapaswa “Kukuza uchaji maalumu kwa Bikra Mama wa Mungu, [aliye] kielelezo na mlinzi wa maisha yaliyowekwa wakfu, ikijumuisha rozari ya Mariamu” (Kan. 1237 §4). Masalio [ya vitu vya watakatifu] ni lazima yapatikane kwenye kila altare ya kudumu katika makanisa yote (Kan. 1237 §2), picha takatifu, hata katika ‘idadi ya wastani”, zinapaswa kuwekwa (Kan. 1188), na zaidi sana zinapaswa kutukuzwa kama njia ya utakaso (Kan. 1186-1190; rej. pia Kan. 663 §4).

### *2. Kufanywa Upya kwa Kupitia Ubatizo*

Kufanywa upya kwa njia ya ubatizo kumeshikamanishwa sana na Sheria ya Kanisa. Kwa kupitia ubatizo watu huzaliwa mara ya pili na kuingia ndani ya [kuwa sehemu ya] Kanisa (Kan.11, 96, 111, 112, 204, 205, 217, 787 §2, 849k.).

> “Ubatizo, mlango kuelekea kwenye Sakramenti, kwa kweli ni wa lazima kwa ajili ya wokovu au angalau kwa kukusudia, ambao kwa huo wanaume na wanawake wanawekwa huru kutoka katika dhambi zao, wanazaliwa mara ya pili kama watoto wa Mungu, na wanafanywa kuwa namna ya Kristo kwa kwa tabia isiyofutika... (Kan. 849).

### *3. Roho Mtakatifu Hupokelewa kwa Kupitia Kipaimara*

Kumpokea Roho Mtakatifu kwa njia ya Kipaimara hubaki vilevile:

> “Sakramenti ya Kipaimara huchochea tabia na kwayo waliobatizwa, wakiendelea katika njia ya uigaji wa Kikristo, wanasheheneshwa kwa kipawa cha Roho mtakatifu na kufungwa kikamilifu zaidi katika Kanisa...” (Kan. 879).

### *4. Ekaristi*

Zaidi ya hapo, Ekaristi ni jambo kuu katika kusanyiko la waaminifu (Kan. 528 §2) na ni dhabihu halisi (Kan. 879, 904). Waaminifu wanapaswa kutukuza kipengele cha Ekaristi “wakikiabudu kwa heshima kuu” (Kan.

898). Ekaristi haiwezi kuadhimishwa pamoja na madhehebu mengine (Kan. 908). Makuhani ni lazima waiadhimishe kila siku. (Kan. 276 §2; 719 §2).

### *5. Kutengwa Moja kwa Moja na Mfarakano*

Ingawa "kutengwa moja kwa moja kama adhabu" kumewekewa mipaka kwa mambo machache kuliko mwaka 1917, bado mambo hayo ni mazito kiasi cha kutosha. Kutumia nguvu za mwili dhidi ya Papa (Kan. 1370) husababisha kutengwa moja kwa moja kama inavyokuwa kwa kutolewa kwa mimba (Kan. 1398), lakini kipekee kwa "makosa dhidi ya dini na umoja wa Kanisa" (Kitabu VI, Sehemu II, Mada I). Chini ya mada hii hujumuishwa "mwasi" yaani mtu ambaye amekana moja kwa moja imani ya Kikatoliki kwa ujumla wake (Kan. 1364, 751, 194 §1, 694 §1); "mzushi," ambaye kwa ukaidi hutilia mashaka baadhi ya kweli za Kikatoliki (Kan. 751, 1364); na "Mleta mafarakano" (Kan. 751, 1364):

> "Mfarakano ni ukataaji wa kujinyenyekeza chini ya Pontifa wa Rumi au wa kufanya komunio na washiriki wa kanisa walio chini yake" (Kan. 751).

Kwa hiyo, kushindwa kujinyenyekeza chini ya Papa, inatosha [kwa mtu] kuhesabika kama mfarakishanaji. Kwa nyongeza, yeyote anayetilia mashaka mafundisho ya Kikatoliki, kwa wakati ule ule ni mzushi na kwa urahisi atakuwa mwasi, yaani mtu aliyeanguka. Hivyo basi dhana ya "ndugu waliotengwa" (Kan. 825 §2) na vilevile maelezo yanayorejea kwa Kanisa jingine la Kikristo kiuhalisia hayadhihirishi badiliko lolote. "Ndugu" hao bado wanahukumiwa kama mwanzo kinyume na jina zuri walilonalo sasa.

### *6. Masuala ya Ndoa*

Kanuni kuhusiana na uharamu na ubatilishaji wa ndoa zinashitusha. Ndoa na mtu asiyebatizwa ni bure na haramu tu (Kan. 1086); jambo hilo ni kweli pia kwa mtu hanithi (Kan. 1084). Ndoa inayoshindwa kutimiza tendo la ndoa inaweza kubatilishwa na Papa (Kan. 1142). Kan. 1143-1150, hususani 1146, hujishughulisha na uwezekano wa talaka kutoka kwa mwenza ambaye hajabatizwa. Ndoa na mtu ambaye hajabatizwa ambaye hawezi kuishi ndoani kutokana na kufungwa au mateso inaweza kubatilishwa hata kama mwenza kwa muda huo atakuwa amebatizwa (Kan. 1149).

Kuna kitu kama ndoa ya siri (Kan. 1130-1133). Fasili ya watoto halali iliyokwishanukuliwa hapo juu tayari, hivyo kwa kudhania huiacha kazi ya kukisia iwapo watoto “wanazaliwa angalau siku 180 baada ya sherehe ya ndoa au ndani ya siku 300 kutoka tarehe ambapo maisha ya unyumba yalipokatizwa” hawana budi kuhesabiwa kama halali!?

### *7. Misamaha na Malipizi*

Mada ya misamaha ina sura nzima iliyowekwa wakfu kwa suala hilo (Kitabu cha IV, Sura IV; Kan. 992-997). “Msamaha ni ondoleo la adhabu ya muda kwa ajili ya dhambi mbele za Mungu, hatia ambayo imekwishasamehewa. Mwanachama aliyeondolewa kabisa ndani ya Wakristo waaminifu hujipatia msamaha chini ya masharti fulani na yaliyo wazi kwa msaada wa Kanisa ambalo, kama mhudumu wa ukombozi, hugawa na kutawanya kwa mamlaka hazina ya utoshelevu wa Kristo na ya watakatifu (Kan. 992).

Ni wazi kuwa mada ya misamaha kwa mara nyingine hugawa nafsi [za watu]. Wakati Biblia inatambua tu msamaha mmoja katika Yesu Kristo, ambao hufuta hatia na hukidhi hukumu ya adhabu ya milele, Kanisa Katoliki hutofautisha kati ya ufutaji wa dhambi kupitia tamko la msamaha baada ya toba, na ondoleo la adhabu ya muda linalopatikana kupitia utoshelevu, misamaha, na muda wa [kuwa] pagatori. Kwa hili, kazi ya ukombozi ya Yesu Kristo iliyokamilika inatiwa mashakani, kwa sababu inakubaliwa nusunusu. Kwa Kanisa Katoliki, dhabihu ya Msalaba na maombi ya msamaha pia hayawezi kuleta ondoleo la adhabu ya muda (huko pagatori)! Pia upatanisho hufungamanishwa na ukiri wakati wa toba (Kan. 964 §2). Sakramenti ya malipizi zaidi sana ni njia pekee ya msamaha. “Ukiri binafsi na wa lazima na tamko la msamaha hujumuisha njia ya kawaida tu ambayo mtu mwaminifu aliye na uelewa wa dhambi nzito hupatanishwa na Mungu na Kanisa” (Kan. 960). Dhambi haielekezwi tu dhidi ya Mungu, bali pia dhidi ya Kanisa (Kan. 959, 960), jambo ambalo ni kiburi.

## I. Hitimisho

Mtu anahitaji tu kusoma Sheria mpya ya Kanisa Katoliki kutambua ni wapi ilipopotoshwa kutoka katika Biblia. Katika kurasa za mwisho ni ibara tu kutoka katika Sheria mpya ya Kanisa zilizowasilishwa, hakuna kingine kutoka katika nyaraka zingine. Kanisa Katoliki limeshikilia msimamo wake ule ule kama ambavyo limekuwa; maandiko ni yenye kuvutia tu na yaliyondaliwa kwa ushirikiano zaidi. Kujua Sheria mpya za Kanisa Katoliki kunatosha kuthibitisha kuwa hakuna uwezekano wa ushirika wa kikanisa

kwa mwamini yeyote kwa maana ya Kibiblia ya neno hilo. Ni watu wangapi wanaofikiri bado wako katika Kanisa Katoliki wakati tangu muda mrefu uliopita walishatengwa moja kwa moja kwa mujibu wa Kanoni? Askofu wa kitaifa wa Kiprotestanti Eduard Lohse alipaswa kuwa amesoma Sheria ya Kanisa kwa umakini kabla ya kukitambua cheo cha Papa na kumwita sawia kama "ndugu katika Kristo".

Kwa hiyo, Sheria mpya za Kanisa Katoliki zinaweza kuwa zenye msaada mzuri katika majadiliano kati ya Wakatoliki na wasio Wakatoliki, kuonesha kuwa ndani ya moyo wa Kanisa Katoliki hakijabadilika kitu. Akiwa amepitia tena hoja kwa ajili ya uhalisia wa Sheria ya Kanoni katika sehemu III, mtu anahitaji tu kuchunguza nakala ya Sheria ya Kanoni ili aweze kushawishika na hali ya mambo katika hali isiyo na shaka.

Hususani aya juu ya misamaha (Kan. 992) pamoja na mafundisho yake kuwa msamaha kupitia kwa Kristo hautoi ukombozi kutoka katika hukumu ya malipizi, sambamba na aya zinazomhusu Papa (Kan. 331, 333) zingetoa jukwaa bora kwa uwasilisha wa Injili ya Kibiblia.

## IV. Ibara Muhimu za Sheria Mpya ya Kanisa

Orodha ifuatayo huonesha aya muhimu zaidi za Sheria mpya ya Kanoni pamoja na vifupisho vinavyoonesha yaliyomo. Orodha hii ni sehemu tu inayochaguliwa kutoka katika toleo la Kijerumani la makala haya. *Mambo muhimu zaidi yamewekewa alama ya nyota*; kwa kawaida kuna ubinafsi fulani hapa. Orodha hii imeandaliwa kuwa msaada kwa mtu anayejifunza mwenyewe. Inaweza pia kusaidia kuandaa mazungumzo na Wakotoliki. Napendekeza kutia alama katika maeneo muhimu kwenye nakala ya Sheria ya Kanoni na pia kuchukua nakala ya orodha hii pamoja nawe. Mtu anaweza kuanza na aya ambazo zinathibitisha kuwa mshirika wa mazungumzo ya Kikatoliki kwa muda mrefu ameathirika kutokana na msimamo uwasilishwao na Sheria ya Kanisa. Katika hali nyingine, njia bora inaweza kuwa kuanza na mada ya mamlaka yanayokua ya Papa. Aya zinazoshughulika na wokovu na msamaha wa dhambi kwa kweli ni nzuri kwa kuandaa mazingira ya ujumbe wa Kibiblia, kwa namna iliyo kinyume, pengine [ni vema] kutumia Waraka wa Paulo kwa Warumi.

| | | |
|---|---|---|
| 204 | §1 | Waaaminifu = wale waliobatizwa |
| 204 | §2 | Papa hutawala Kanisa |
| 210 | | Utakaso |
| *212 | §1 | Utii kwa viongozi kama "wawakilishi wa Kristo" |

| | | |
|---|---|---|
| *218 | | Uhuru wa kuuliza iwapo heshima kwa mamlaka (sio Biblia) hutunzwa |
| 223 | §2 | Mamlaka ya kikanisa huratibu haki za waaminifu |
| 245 | §2 | Waseminari kujitoa kwa utiifu kwa Papa |
| 246 | §1 | Ekaristi ni kitovu cha maisha ya seminari |
| 246 | §3 | Uchaji kwa Mariamu na kwa Rozari unatetewa |
| *273 | | Wakleri [viongozi] wa kanisa humtii Papa na Askofu |
| 276 | §3 | Wakleri [viongozi] wa kanisa kutimiza liturujia za maombi kila siku |
| *276 | §5 | Uchaji kwa Mariamu ni njia ya utakaso |
| 277 | §1 | Useja |
| *330 | | Papa+Maaskofu = Petro+Mitume |
| *331 | | Mamlaka ya Papa; mwakilishi wa Kristo |
| *333 | §1 | Mamlaka ya Papa ya kawaida kwa makanisa yote mahususi |
| *333 | §2 | Papa huliongoza kanisa yeye mwenyewe au, kama akitaka na Maaskofu |
| 334 | | Ofisi zote hufanya kazi zake kwa jina la Papa |
| *336 | | Hakuna Baraza la Maaskofu pasipo Papa |
| *341 | §1 | Amri za Baraza la Kanisa hutumika tu iwapo zimeidhinishwa na Papa |
| 337 | §1 | Maaskofu huchukua nafasi za Mitume |
| 400 | | Maaskofu kuyatukuza makaburi ya Petro na Paulo |
| 528 | §1 | Ekaristi kitovu cha “kusanyiko la watakatifu” |
| *663 | §4 | Utukuzaji wa Mariamu na Rozari |
| *749 | §1 | Kutokukosea kwa ofisi ya mafundisho ya Papa |
| *749 | §2 | Baraza la Kanisa hakosei lihusishwapo na Papa |
| *750 | | Maandiko na Mapokeo |
| *751 | | Uzushi, uasi, na mfarakano |
| *752 | | Si imani itokanayo na moyo wa kujisikia, bali ni utii |
| 825 | §1 | Uchapaji wa Biblia kwa kibali cha Papa tu |

| | | |
|---|---|---|
| 825 | §1 | Uchapaji wa Biblia yenye “fasili inayofaa” tu |
| 834 | §1 | Utakaso kupitia liturujia takatifu |
| 847 | | Jinsi ya kuweka wakfu mafuta matakatifu |
| *849 | | Ubatizo huweka huru mbali na dhambi |
| *879 | | Kipawa cha Roho Mtakatifu hupokelewa kupitia Kipaimara |
| *897 | | Ekaristi ina Kristo [ndani yake] na ni dhabihu |
| *898 | | Ekaristi kuabudiwa kwa heshima kuu |
| *899 | §2 | Makuhani hutenda “katika nafsi ya Kristo” |
| *901 | | Misa kwa ajili ya Wafu |
| *904 | | Dhabihu ya Ekaristi kama kazi ya ukombozi |
| 932 | §2 | Dhabihu kufanyika kwenye altare iliyowekwa wakfu au iliyobarikiwa |
| 947-51 | | Kanuni kwa ajili ya kupokea malipo ya misa |
| *959 | | Sakramenti ya malipizi |
| *959 | | Upatanisho na Mungu na Kanisa |
| *960 | | Kukiri [toba], njia pekee ya upatanisho |
| 964 | | Kukiri, kawaida kwa kutumia kiti maalum cha kutubia tu |
| 978 | | Baba msikiliza toba ni hakimu na mponyaji |
| 981 | | Matendo ya malipizi |
| *992-6 | | Misamaha |
| *1084 | | Ndoa na ambaye hajabatizwa ni batili |
| *1149 | | Talaka yawezekana ikiwa mwenzi atafungwa [jela] |
| *1186 | | Utakaso kupitia kutukuzwa kwa Mariamu |
| 1187 | | Kutukuzwa kwa watakatifu |
| 1188 | | Sanamu (picha) takatifu katika hali ya wastani |
| 1190 | | Mabaki ya watakatifu |
| 1235-39 | | Altare [madhabahu] |
| *1237 | §2 | Kila altare iliyowekwa imesisimamshwa juu ya mabaki ya watakatifu |

| | | |
|---|---|---|
| 1251 | | Kujitenga na nyama siku za Ijumaa |
| 1251 | | Kila mmoja kufunga siku ya Jumatano ya Majivu na Ijumaa Kuu |
| 1256 | | Mamlaka makuu ya Papa yakihusishwa na umiliki wa mali zote |
| 1264 | | Malipo kwa ajili ya upendeleo na uhudumiaji wa Sakramenti |
| *1273 | | Papa mtawala wa mali zote za kanisa |
| 1365 | | Ushiriki unaokatazwa katika ibada za madhehebu mengine |
| 1367 | | Kutengwa moja kwa moja kwa ajili ya matumizi mabaya ya elementi za ekaristi |
| 1370 | | Kutengwa moja kwa moja kwa ajili matumizi ya nguvu dhidi ya Papa |
| 1371 | | Adhabu kwa sababu ya kufundisha kinyume na fundisho lolote lililolaaniwa na Papa au Baraza la Kanisa |
| *1372 | | Hakuna rufaa kwa Baraza la Kanisa au Maaskofu dhidi ya Papa |
| 1388 | §1 | Kutengwa moja kwa moja kwa kuvunja usiri wa toba |
| *1398 | | Kutengwa moja kwa moja kwa sababu ya utoaji mimba |
| *1404 | | Papa hawezi kuhukumiwa na mahakama yoyote |
| *1442 | | Papa hakimu mkuu |

Nukuu kutoka katika Sheria ya Kanoni, zinazofuata baada ya kanoni (Kan.) ni aya ("§"), zimechukuliwa kutoka katika tafsiri ya Kiingereza, The Code of Canon Law – A Text and Commentary, New York: Paulist 1985. Fahamu kwamba, toleo la Kilatini tu, ambalo limekuwa likitumika kuandika makala haya, linakubalika kisheria. The Apostolic Constitution [Katiba ya Kitume] (iliyonukuliwa "Apost. Const.") ni dibaji ya kipapa kuhusu Sheria ya Kanoni na inaweza kupatikana kwenye toleo hilo hilo.

Toleo la Kijerumani (refu kidogo) la makala haya ni:

> "Hat sich die katholische Kirche geändert? Zum neuen katholischen Kirchenrecht". Bibel und Gemeinde 89 (1989) 2: 181-207

Hat sich die katholische Kirche geändert? Zum neuen katholischen Kirchenrecht. Schriften des Bibelbundes. (Sonderdruck aus: Bibel und Gemeinde 89 (1989) 2: 181-207). Verlag des Bibelbundes: Waldbronn, 1990

Makala fupi zilizoandikwa na DK. Schirrmacher katika wakati wa toleo la kwanza na la pili la Sheria mpya ya Kanoni ni:

"Das neue katholische Kirchenrecht". Licht und Leben 95 (1984) 9: 198-200

"Das neue katholische Kirchenrecht". 2. überarbeitete Ausgabe. Gemeinde Konkret Nr. 16 Juli 1985: 15-16

"Das römisch-katholische Kirchenrecht". Bekennende Kirche (Neuhofen) (1993) Null/1 (20.2.): 5-6+14-15

# Visawe na Maelezo ya Maneno

**Adhabu (Penance):** Malipizi afanyayo mtu kutokana na makosa au dhambi alizozifanya. Yana sehemu muhimu sana katika Ukatoliki kwani ni mojawapo ya njia ya utakaso.

**Ainisha (Classify):** Weka katika aina, makundi au madaraja.

**Anabaptisti (Anabaptist):** Kundi au dhehebu la Kikristo lenye kusisitiza ubatizo kwa watu wazima tu.

**Andragoji (Andragogy):** Mfumo wa elimu kwa watu wazima wenye kuzingatia mbinu na utendaji mbadala.

**Anuai (Diversity):** Aina mbalimbali.

**Asili (Adoption):** Kukubaliana na mazingira mapya na kuishi kama ni mazingira yako asilia.

**Bizantini (Byzantine):** Dola iliyoimarika baada ya kusambaratika kwa dola ya Kirumi. Ni sehemu za mashariki za iliyokuwa dola ya Kirumi. Mji mkuu wake ulikuwa Konstantinopo ambao kwa sasa ni Istanbul.

**Chapwa (Neutral):** -enye hali isiyoegemea upande mmoja [hali ya kuwa katikati].

**Fasili (Definition, Interpretation):** 1. Maana ya kitu, jambo au maelezo fafanuzi juu ya kitu hicho. 2. Toa maana, maelezo au ufafanuzi juu ya jambo husika. (Tofautisha na **Tafsiri**: toa katika lugha moja na kupeleka katika lugha nyingine).

**Fasili-chimbuzi (Exegeses):** Ufafanuzi wa kina wa kifungu au vifungu vya maandiko [hususani Maandiko Matakatifu].

**KA (Kiwango Akili) = (Intelligent Quotient):** 1. Uwezo wa kiakili alionao mtu. 2. Kipimo kinachoonesha kiasi cha akili za mtu.

**Kanisa-mtaa (Congregation/Local Congregation):** Kanisa la mtaa.

**Kanoni (Canon):** 1. Kipimo au kanuni.

**Katalogi (Catalogue):** Chapisho au kitabu chenye orodha au maelezo ya vitu kwa mujibu wa mpango fulani maalumu.

**KH (Kiwango Hisi) = EQ (Emotional Quotients):** 1. Uwezo wa kihisia alionao mtu. 2. Kipimo kinachoonesha kiasi cha hisia za mtu.

**Kinzani (Critical):** 1. -enye kwenda kinyume, -enye mawazo pinzani au mawazo tofauti.

**Kisawe:** Neno hilo hilo katika lugha nyingine. 2. Neno lenye kufanana na hilo au kukaribiana nalo kimaana.

**Kitenzi (Verb):** 1. Neno linaloelezea tendo au kitendo.

**Konsevativu (Conservative):** 1. Mtazamo wenye kushikilia imani au mafundisho asilia ya dini au nadharia fulani. Kwa kawaida haupokei mabadiliko kwa urahisi. 2. Mlengo wa kulia.

**Kuweka Wakfu (Ordain):** 1. Kumweka au kumtenga mtu au kitu rasmi kwa ajili ya kazi fulani maalumu. Kwa kawaida huambatana na imani au matakwa ya kidini. 2. Kumwekea mtu mikono ikiwa ni tendo la kiimani la kumtenga rasmi kwa ajili ya kazi ya Mungu [mf. kumweka wakfu mchungaji au padri kazini].

**Liberali (Liberal):** 1. Mtazamo wa kimageuzi au uendao kinyume na hali ya kawaida iliyozoeleka na kukubalika. 2. Katika Ukristo, uliberali huenda kinyume kabisa na misingi mikuu ya Biblia na Ukristo kwa ujumla wake.

**Liturujia (Liturgy):** Utaratibu rasmi wa kiibada kwa mujibu wa dhehebu husika.

**Mashiko:** Jambo linalokubalika sana kwa wakati husika.

**Matengenezo (Reformation):** Kipindi maalumu katika kanisa kilicholeta mageuzi makubwa ya kurudi katikamsingi wa neno la Mungu kutoka katika mwelekeo uliokuwa ukifuatwa na Kanisa Katoliki la Rumi. (**Reform**): mabadiliko, mageuzi, marekebisho au hali ya kufanya jambo liwe bora zaidi.

**Mawanda (Scope):** Upana wa eneo au jambo

**Mfumo msonge (Hierarchical System):** Mfumo wa ngazi ambao huwa na watu wa kawaida chini, na kadri unavyokwenda juu ndivyo madaraka na mamlaka huongezeka.

**Misamaha (Indulgences):** Ruhusa inayotolewa na Papa ya mtu kusamehewa au kuondolewa adhabu yake ya muda huko pagatori. Kwa kawaida ruhusa hii huendelea kufanya kazi hata baada ya mtu kufanya malipizi.

**Msongo (Depression):** 1. Hali ya kuzidiwa na mawazo mazito kiasi kwamba mtu hawezi kuwa katika hali ya kawaida tena. 2. Sononeko zito la moyo.

**Muktadha (Context):** 1. Mazingira mahususi 2. Vifungu vinavyotangulia na vinavyofuatia kifungu mahususi cha Maandiko Matakatifu [hata maandiko mengine].

**Muundo unaovuka mipaka ya kikanda (Supraregional Structure):** Mfumo wa utawala ambao unakuwa na ngazi kubwa ya uongozi uvukao mipaka ya maeneo rasmi yatambulikanayo kama kanda.

**Mwako (Enlightenment):** Mfumo au vuguvugu katika karne ya 18 hivi ambapo matumizi ya fikra yalipewa uzito mkubwa sana kuliko imani.

**Pagatori (Purgatory):** Mahali ambapo mtu aliyefariki hupelekwa kwa muda ili kutumikia adhabu yake kutokana na makosa au dhambi alizozifanya hapa duniani kabla ya kuruhusiwa kuingia paradiso. Hili ni wazo la Kanisa Katoliki.

**Pangilivu (Systematic):** -enye kufuata mpangilio maalumu.

**Pedagoji (Pedagogy):** Mfumo wa elimu hususani kuhusu mbinu na matendo ya ufundishaji. Kwa kawaida mfumo huu huzingatia kanuni za ufundishaji zinazoelekezwa hasa katika shule za watoto na vijana.

**Pontifa (Pontiff):** Kiongozi mkuu wa Kanisa Katoliki duniani yaani Papa.

**Saikolojia (Psychology):** Elimu ya sayansi ihusikayo na akili au utendaji wa mtu kiakili.

**Shaghalabaghala (Haphazard):** 1. Hovyo hovyo 2. Bila mpangilio unaoeleweka.

**Udogmatiki (Dogmatism):** 1. Ububuso. 2. Mfumo wa imani ulioimarishwa upaswao kufuatwa bila kuulizwa au kutiliwa mashaka.

**Udugu (Brethren):** Kundi au dhehebu la Kikristo linaloamini katika hatua bora zaidi ya ukweli wa kibiblia kuliko ile ya Matengenezo.

**Uekumenika (Ecumenicity):** 1. Dhana ya kanisa kwa ujumla wake. 2. Umoja wa makanisa duniani kote.

**Uepiskopo (Episcopalianism):** Mfumo wa utawala wa kanisa unaozingatia mamlaka ya kimsonge na ambao hasa ni wa kiuaskofu.

**Ukengeuko (Deviation):** Kutoka katika hali asilia na kushika mwelekeo mwingine. Kwa kawaida, mwelekeo huo mwingine huonekana kuwa ni upotokaji.

**Ukiri (Confession):** 1. Tamko rasmi la kiimani au kidhehebu mf. Imani ya Mitume n.k. 2. Tamko la kukubali jambo 3. Toba

**Upresbaiteria (Presbyterianism):** Mfumo wa utawala wa kanisa unaweka mamlaka takribani yote mikononi mwa wazee wa kanisa ambao wote huwa sawa kihadhi na kimamlaka.

**Uprotestanti (Protestantism):** Mfumo wa Ukristo ambao haukubaliani na ule wa Kikatoliki wa Rumi. Kwa kawaida mfumo huu hufuata misingi ya Matengenezo kama ilivyoasisiwa na Luther na Calvin.

**Usuli (Background):** Chanzo, asili au msingi wa kitu, hali au jambo.

**Utengenezi (Reformed):** Mfumo wa kikristo unaofuata hasa dhana ya Matengenezo katika kanisa. Nao hujikita zaidi katika mlengo wa Ki-Calvin.

**VH (Viwango Hisi) =EQ (Emotional Quotients):** Wingi wa KH (yaani, Kiwango Hisi).

**Wahakiki-chimbuzi (Exegetes):** Wasomi wafanyao uhakiki wa kina katika neno au maneno ya kifungu, hasa katika maandiko [hususani Maandiko Matakatifu].

**Wakleri (Clergies):** 1. Viongozi walio watumishi wa kanisa. 2. Kinyume cha walei.

**Walei (Lay people):** Waumini wasio viongozi katika kanisa.

**Wamonofisti (Monophysites**): Kundi la Kikristo liaminilo kuwa Yesu yuko katika asili moja tu isiyotenganishwa ambayo imegawanyika katika maeneo makuu mawili: kwanza, uungu wake – unaotawala; na pili, ubinadamu wake – unaotawaliwa.

**Wananyakati (Dispensationalists):** Wakristo waaminio kuwa mfumo mzima wa kihistoria umewekwa na Mungu kwa kuzingatia nyakati au vipindi maalumu kwa makusudi maalumu.

**Wanasihi (Mentors):** Wakufunzi au washauri watoao nasaha na ushauri kwa wale wanaowaelekeza.

**Weledi (Profession):** Utaalamu aupatao mtu kutokana na mafunzo ya kina katika utalaamu husika.

**Zama za Kati (Middle Ages):** Kipindi cha kihistoria katika Ulaya cha miaka ya kuanzia 1000 B.K. hadi 1450 hivi B.K.

## Vifupisho vya Maneno

| | |
|---|---|
| k. (f) | – na kuendelea |
| uk. (p.) | – ukurasa |
| kr. (pp.) | – kurasa |
| K.K. (B.C.) | – Kabla ya Kristo |
| B.K. (A.D.) | – Baada ya Kristo |
| Rud. (Ibid.) | – Rudia rejea hapo juu |